ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32 Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50. Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa
51.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni

52.Mhe. Mgeni Hassan Juma Nafasi za Wanawake

53.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma Jimbo la Bumbwini

54.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

55. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

56.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

57.Mhe. Mohammed Said Mohammed Jimbo la Mpendae

58. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak Nafasi za Wanawake

59.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

60.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

61.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

62.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

63.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

64.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Rashid Seif Suleiman Jimbo la Ziwani

66.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

67.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

68.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

69.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

70.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

71.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

72.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe

75. Mhe. Shawana Bukheti Hassan Jimbo la Dole

76.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni

77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde

78.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani

79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake

80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Tatu – Tarehe 19 Juni, 2012

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

KIAPO CHA UAMINIFU

Mhe. Marina Joel Thomas: Mimi Marina Joel Thomas naapa kwamba nitakuwa muaminifu kwa Zanzibar katika kazi zangu za Uwakilishi, na nitaitumikia kwa moyo wangu wote na kwamba nitaihifadhi, nitailinda na kuitetea kwa dhati Katiba ya Zanzibar, nakuomba Mwenyezi Mungu unisaidie. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nawashukuru sana, na makofi yote hayo ni ya kumkaribisha rasmi Mhe. Marina Joel Thomas, ambaye ameteuliwa juzi na leo hii tumemuapisha rasmi katika Baraza letu la Wawakilishi hapa Zanzibar. Niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wote pamoja na mawaziri, mumpe mashirikiano ndugu yetu Mhe. Marina, ili na yeye amudu kufanya shughuli zake kama vile inavyotakiwa kwa mujibu wa Kanuni, Katiba na Sheria ya Haki, Fursa za Wajumbe.

Mhe. Marina karibu sana, makofi yaliyopigwa kwa ajili yako ni uthibitisho wa kukubali na kukukaribisha rasmi katika Baraza hili, nakwambia watakupa mashirikiano ya kutosha katika shughuli zako. Tayari nimemkabidhi nondo za kufanyia kazi ambayo ni Katiba ya Zanzibar, Sheria inayohusu Haki za Wajumbe pamoja na Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la karibuni tu hivi mwaka 2012.

Mhe. Marina karibu sana.

Waheshimiwa Wajumbe, mbali na kazi moja hiyo kubwa tuliyoifanya hivi punde, katika ukumbi wetu wa juu pale ukumbi wa wageni kuna wageni waliokuja kushuhudia tukio la kuapishwa Mhe. Marina Joel Thomas, nao ni kati ya familia ya Mheshimiwa wetu Marina Joel. Waliohudhuria katika ukumbi huu kwa ajili ya kushuhudia tukio hili ni pamoja na ndugu **Harg Robert Muwendo,** Mume wa Mhe. Marina namuomba asimame. *(makofi)*

Vile vile amefuatana na Cristopher Muwendo ni mtoto wa Mhe. Marina, Maryam Muwendo pia naye ni mtoto wake, wamefuatana pia na ndugu yetu Denis Muwendo ni mtoto vile vile, amefuatana na Christina Joel Thomas huyu ni dada. Naomba nitoe taarifa kuwa Christina ni mwanafunzi wangu. Wamefuatana pia na ndugu Monica Mpanda huyu ni dada namuomba asimame. Pia yupo ndugu Merry Mpanda na huyu pia ni dada.

Ndugu zetu, wageni wetu mume wa Mhe. Marina, watoto pamoja na dada zake basi tunashukuru na karibuni sana katika ukumbi wetu huu, na nakushukuruni kwamba mmeshuhudia tukio la kuapishwa ndugu yetu Mhe. Marina. Lakini pamoja na wageni wengine wote pia wanakaribishwa sana katika shughuli zetu hizi. Waheshimiwa Wajumbe ahsanteni sana.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 44

Suala la Mafuta na Gesi Asilia ndani ya Muungano

Mhe. Ismail Jussa Ladhu – Aliuliza:-

Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipatia fursa hii na naomba nianze kwanza kwa kumpongeza dada yetu Mhe. Marina Joel Thomas kwa kuteuliwa na leo kuapishwa kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi hili. Tunamkaribisha sana na tunamhakikishia kwamba tutampa mashirikiano kwa kikamilifu.

Baada ya pongezi hizo Mhe. Spika, sasa naomba nijibiwe swali langu nam 44.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia kwa aliyekuwa Waziri Kiongozi aliandika barua rasmi mbili kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Waziri Mkuu kuiarifu uamuzi wa Baraza la Wawakilishi wa kuliondoa suala la mafuta na gesi asilia kutoka katika orodha ya mambo ya Muungano, ili Serikali ya Muungano nayo ichukue hatua za kupeleka Mswada wa Marekebisho ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano kwa

madhumuni ya kutekeleza uamuzi huo. Hatua hiyo haijatekelezwa hadi sasa na badala yake Serikali ya Muungano inaendelea kusaini mikataba ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia na kampuni za kigeni, mikataba ambayo inajumuisha maeneo ya Zanzibar.

(a) Je, tokea kuingia madarakani Serikali ya Awamu ya Saba yenye muundo wa Umoja wa Kitaifa, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ambayo ndiyo iliyochukua nafasi ya iliyokuwa Ofisi ya Waziri Kiongozi imechukua hatua gani kufuatilia majibu ya barua zilizoandikwa.

(b) Nini msimamo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhusiana na hatua ya Serikali ya Muungano kusaini mikataba ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia na kampuni za kigeni inayojumuisha maeneo ya Zanzibar.

(c) Baada ya miaka mitatu kupita tokea kuandikiwa barua na kutokana na Serikali ya Muungano kutoonesha mashirikiano katika kupeleka marekebisho ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano kuliondoa suala la mafuta na gesi asilia katika orodha ya mambo ya Muungano, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haioni kuwa wakati umefika wa wenyewe kuchukua hatua za kulirejesha suala hilo katika mamlaka yake kama ilivyofanya kwa mambo mengine yaliyomo kwenye orodha ya mambo ya Muungano na ambayo hayakuwahi kutekelezwa Kimuungano.

(d) Je, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haioni kuwa kuendelea kukaa kwake kimya bila ya kuchukua hatua zinazokwenda sambamba na matakwa ya wananchi wa Zanzibar kunawafanya wananchi wa Zanzibar wapoteze imani na viongozi wao.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwanza na mimi naomba uniruhusu nimpongeze Mhe. Marina Joel Thomas kwa kuchaguliwa kuwa Mwakilishi, anaonekana kabisa kama ni mwanamama shupavu, aliye tayari kutetea nchi yake na wananchi wa Zanzibar. Kwa hivyo, nachukua fursa hii kumkaribisha katika Baraza letu tukufu la Wawakilishi ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika, baada ya hayo kwa ruhusu yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 44 lenye vifungu (a) (b) (c) na (d) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia kwa aliyekuwa Waziri Kiongozi alimuandikia barua Mhe. Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kumuarifu azimio la Baraza la Wawakilishi kwa kuliondoa suala la mafuta na gesi asilia katika orodha ya mambo ya Muungano.

Aidha, Mhe. Makamo wa Pili wa Rais mara tu baada ya kuingia madarakani naye aliandika barua ya kukumbushia kwa Waziri Mkuu juu ya suala hili. Katika kikao cha kamati ya pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kushughulikia kero za Muungano kilichoongozwa na Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kilichofanyika tarehe 28 Januari, 2012 ajenda ya suala la utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia lilikuwa miongoni mwa ajenda zilizojadiliwa.

Jambo hili lilizungumzwa kwa kina na tulikubaliana lipatiwe ufumbuzi haraka iwezekanavyo, hasa ukitilia maanani kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilikuwa tayari imetoa mapendekezo yake kama yalivyo katika azimio la Baraza hili tukufu na sasa tunasubiri maoni ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ili taratibu nyengine zifuate kwa nia ya kulitoa jambo hili katika mambo ya Muungano.

Mhe. Spika, hivyo ni dhahiri kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haijalinyamazia kimya suala hili, bali linalifanyia kazi kwa mujibu wa sheria zilizopo na wala hatutolifumbia macho bali tutazidisha kazi ya kulipatia ufumbuzi suala hili.

Mhe. Spika, kuhusu utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia kwa kampuni za kigeni, msimamo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuwa utaendelea kuwa pale pale kuheshimu na kutekeleza azimio la Baraza la Wawakilishi. Hivyo haitaruhusu kwa kampuni yoyote ile ya kigeni kutafuta au kuchimba mafuta katika maeneo ya Zanzibar bila ya maamuzi ya Wazanzibari wenyewe.

Mhe. Spika, nataka nilihakikishie Baraza hili kuwa hivi karibuni jambo hili litapata ufumbuzi kama yalivyo matarajio ya Wazanziabari na hasa ukizingatia kuwa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika matamko yake alisema, haoni tatizo kwa suala hili kutolewa katika orodha ya mambo ya Muungano.

Mhe. Spika, ni kweli kuchelewa kutolewa suala hili katika orodha ya mambo ya Muungano kumesababisha kero kubwa na malalamiko kwa wananchi. Hivyo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itafanya kila jitihada kutimiza matakwa ya Wazanzibari na kuleta mabadiliko makubwa ya kimaendeleo ili kuzidisha imani ya wananchi wa Zanzibar kwa serikali yao.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nakushukuru Mhe. Spika, na namshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Moja, kwa sababu katika majibu yake Mhe. Waziri amesisitiza msimamo wa serikali kwamba inaheshimu maamuzi ya Baraza hili, na kwa hivyo haitaruhusu utafutaji na uchimbaji wa mafuta kwa maeneo ya Zanzibar. Je, anaiambia nini Serikali ya Jamhuri ya Muungano kupitia Baraza hili kwa kusaini kwake mkataba ambao sasa umeruhusu Kampuni ya ***Petro Brass*** kufanya kazi ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta katika kitalu Nam. 8 ambacho kipo katika eneo la Zanzibar.

Pili, ni kwamba kwa sababu ni muda mrefu tangu Azimio la Baraza la Wawakilishi lilipopitishwa mwaka 2009, siamini kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano inahitaji miaka mitatu na zaidi katika kufanya maoni yake, lakini mbinu kama zilizotumika katika mambo mengine mengi ambayo hadi leo hayajapatiwa ufumbuzi likiwemo suala la *Joint Financial Commission* ambayo lina zaidi ya miaka sita bila ya kupata ufumbuzi.

Je, waziri katika kusimamia wanachokitaka wananchi wa Zanzibar, atakubaliana na mimi kwamba sasa wakati umefika ile ahadi waliyoichukua serikali mwaka wakati wa kikao cha bajeti kama hichi, kwamba wapewe mwaka mmoja na kwamba katika kikao kilichofanyika alichokitaja cha mashauriano alitoa miezi minne kulimaliza suala hili ambalo limemalizika mwezi wa tano huu uliomaliza. Haoni sasa wakati umefika serikali ilete mswada wa sheria ya mafuta Zanzibar na sheria ya kuanzisha Shirika la Mafuta Zanzibar ili kazi hii iweze kusimamiwa na Zanzibar yenyewe.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa ufupi kabisa tulishakubaliana katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwamba maeneo yote ya Zanzibar kwa sasa hayatoruhusiwa kuendelea na suala la utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia. Kwa maana hiyo, taarifa hii tuliwaandikia rasmi wenzetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wao hivi sasa wanatakiwa kuendelea na mapendekezo yetu hayo, ili tuweze kupata jawabu lililo sahihi na tuweze kuendelea na suala zima la kuyatoa mafuta katika mambo ya Muungano.

Kama nilivyosema, katika matamko yake mbali mbali Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameliona hili na kusema kwamba kulitoa suala la mafuta na gesi asilia katika mambo ya Muungano haoni kuwa ni tatizo. Kwa hivyo, mkataba wowote ule utakaofanyika ukaingiza maeneo ya Zanzibar tunawahakikishia Waheshimiwa wa Baraza hili tukufu na wananchi wa Zanzibar kwamba maeneo ya Zanzibar hayatoguswa kufanyiwa shughuli hizo. Tutafanya kila jitihada kuhakikisha kwamba hayaguswi na hakuna atakayefanya shughuli za utafutaji au uchimbaji mafuta katika maeneo ya Zanzibar na suala hili litafanywa na Wazanzibari wenyewe wakati utakapofika.

Mhe. Spika, kuhusu suali la pili katika kuhakikisha kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatekeleza maazimio yanayotolewa na Baraza hili tukufu, kama nilivyosema hapa kwamba katika muda usio mrefu suala hili Mheshimiwa litapata ufumbuzi. Ni kweli katika kikao chetu cha pamoja kilichokuwa chini ya Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kikao cha Waziri Mkuu na Makamo wa Pili wa Rais tulikuabaliana kabisa kwamba jambo hili ndani ya miezi minne lipate ufumbuzi. Kwa sababu jambo hili lina taratibu kidogo za kisheria ambazo tunahisi inabidi zifuatwe, hivyo nataka niwahakikishie Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba, muda usio mrefu kuanzia sasa jambo hili litapata ufumbuzi rasmi kwa maslahi na manufaa ya Wazanzibari na kwa matakwa ya Wazanzibari wenyewe.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kwa kumuuliza Mhe. Waziri swali moja dogo tu la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa suala la mafuta na gesi asilia kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni suala la Muungano. Na kwa kuwa wenzetu wa upande wa Jamhuri ya Muungano wamekuwa kwa muda mrefu wakifaidika na faida inayotokana na gesi asilia. Je, katika kipindi chote hicho Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefaidika na nini.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kuwa jambo hili ni suala la Muungano na Zanzibar inayo haki ya kupata mapato yanayotokana na gesi, mazungumzo yamefanyika na nataka nilihakikishie Baraza lako hili tukufu kwamba Zanzibar itapata haki yake kutokana na gesi ambayo ilichimbwa kwa mujibu wa makubaliano.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nashukuru kunipa nafasi ili nimuulize Mhe. Waziri swali dogo la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza lililopita katika mwaka 2009 tulikubaliana pamoja na serikali kwamba iwasilishe Mswada binafsi katika Baraza juu ya Uundwaji wa Shirika la Mafuta Zanzibar. Na kwa kuwa hadi sasa serikali haijawasilisha mswada huo wa sheria ili tuunde Shirika la Mafuta hapa Zanzibar, na kwa kuwa jana nilitangaza nia ya kuwasilisha kwa mujibu wa taratibu zetu za Kanuni niwasilishe mswada binafsi, nilitangaza nia hiyo ya kuwasilisha mswada binafsi kuwa tukubali kuwa serikali ianzishe shirika hilo. Je, nitakapowasilisha serikali itaniunga mkono.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, serikali inaongozwa kwa Katiba na Sheria, na siku zote serikali inatizama maslahi na manufaa ya wananchi wake, lolote lenye maslahi na manufaa ya wananchi wake litapewa kipaumbele na serikali yetu.

Nam. 12

Ufuatiliaji wa Utendaji wa Wizara za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar

Mhe. Ali Salum Haji – Aliuliza:-

Mhe. Spika, nami kabla ya kuuliza swali naomba nichukue nafasi hii kumpongeza ndugu yangu Mhe. Marina Joel Thomas kwa uteuzi alioupata wa uwakilishi, na nikimfahamu vya kutosha wakati wa uongozi wangu wa Udiwani walinipa mashirikiano ya kutosha katika nafasi hiyo.

Mhe. Spika, baada ya kutoa pongezi hizo sasa naomba kujibiwa swali langu Nam. 12.

Mhe. Rais wa Zanzibar amekuwa na utaratibu mzuri wa kukutana na watendaji wa wizara mbali mbali kila baada ya muda maalum, kwa ajili ya kutathmini na kuzingatia utekelezaji wa malengo maarufu kwa jina la "bango kitita".

Je, Mhe. Waziri huoni kuwa kuna haja ya kuundwa chombo maalum cha kufuatilia yanayoelezwa na watendaji hao ili kujua utekelezaji wake.

Mhe. Spika: Kabla sijamruhusu Mhe. Waziri kujibu naona wajumbe walikuwa wamefurahi sana maana Mhe. Waziri Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais majibu yake yamekuwa yanateleza kuliko pweza. (*Kicheko*)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na mimi naomba niungane na wenzangu kumpongeza sana Mhe. Marina Joel Thomas kwa uteuzi wake wa kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi. Mhe. Spika, baada ya pongezi hizo naomba kwa ruhusa yako kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 12 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, utaratibu aliojipangia Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein wa kupokea taarifa ya utekelezaji wa mpango kazi sio bango kitita, zile ni taarifa za utekelezaji wa mpango kazi kwa mwaka na huwa tunazigawa katika robo nne za kila mwaka, lakini labda ule uwasilishaji wake unakuwa katika ***metrix*** zile ndio tume-*nickname* 'bango kitita'. Lakini jina sahihi ni mpango au Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango Kazi.

Mhe. Spika, kama nilivyosema kwamba huu ni utaratibu wa kawaida ambao Mhe. Rais amejipangia wa kupata taarifa za utekelezaji wa mpango kazi kuweza kutathmini utekelezaji wa shughuli za serikali kwa kuzingatia malengo, vipaumbele na bajeti ya kila wizara kama ilivyoidhinishwa na kikao chako cha Baraza la Wawakilishi. Ufuatiliaji huu Mhe. Spika, wa utekelezaji wa shughuli za serikali wizarani ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa mipango na ahadi za bajeti na maagizo ya Mhe. Rais katika taasisi mbali mbali za serikali, unafanywa na watendaji mbali mbali na anayebainika huwasilishwa kwa Mhe. Rais kwa maandishi. Utaratibu huu umebainisha faida kadhaa muhimu kama ifuatavyo:-

(a) Watendaji wa wizara na taasisi zake kupata fursa ya kujitathmini katika utekelezaji wa majukumu yao na kubaini matokeo ya jitihada zao.
(b) Kuhamasisha watendaji kufanya kazi kwa pamoja na kuongeza kasi ya uwajibikaji wao ili kuongeza ufanisi makazini.
(c) Watendaji wa wizara na taasisi zake hupata fursa ya kuwasilisha hatua za utekelezaji, mafanikio na changamoto wanazokabiliana nazo katika utekelezaji wa majukumu yao mbele ya Mhe. Rais, Makamo wa Kwanza wa Rais, Makamo wa Pili wa Rais na Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi.
(d) Mhe. Spika, utaratibu huu umeweza kuimarisha nidhamu ya matumizi ya pesa za serikali.

Mhe. Spika, naomba nioneshe tu kwamba hii kazi kwa kweli ni kubwa na nzito na lazima tuwapongeze watendaji wetu katika maandalizi. Nitatoa mfano mimi wizara yangu tu ilipata siku tatu ya kuwasilisha huu mpango kazi. Siku ya kwanza tulikuwa na Makao Makuu ya Wizara na tukawasilisha kitabu mfano wake hiki, halafu tukaja Tawala za Mikoa, Tawala za Mikoa sote tunafahamu ukubwa wake tukaja na buku kubwa tu, halafu siku ya mwisho tukaja Idara Maalum ya Vikosi vyote.

Sasa hii kwa kweli inafaa tumpongeze sana Mhe. Rais, Makamo wa Kwanza, wa Pili kwa sababu muda wote wanakuwepo na wanahoji yale mambo yote tuliyoyapitisha kwenye bajeti, tunakwenda kifungu kwa kifungu na katika kila kifungu tunaonesha bajeti iliyotengwa, fedha iliyotengwa (bajeti yote kwa mwaka) fedha iliyotengwa kwa robo ile, fedha iliyopatikana kwa robo ile yaani kwa asilimia, shughuli iliyopangwa na utekelezaji wake na asilimia ya utekelezaji wake.

Kwa hivyo, huu mpango unatusaidia sana Mhe. Spika katika utekelezaji na usimamizi wa bajeti yetu. Mhe. Spika, nakuahidi Kamati ya Mhe. Omar Ali Shehe ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika basi mwakani kutakuwa na mabadiliko makubwa sana baada ya zoezi hili. Ahsante sana.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza na mimi nimpongeze Mheshimiwa mpya Marina aliyeteuliwa leo Mwenyezi Mungu amjaalie kila la kheri na tutamsaidia katika kazi zake asikie vitu ambavyo tunavyovitoa sasa hivi. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza maswali mawili.

Mhe. Waziri utakubaliana na mimi ripoti zenu mlizompelekea Rais mna mdanganya na kama ni hivyo ni kweli je, Waziri akigundulikana kama kweli kafanya kitu cha kumdanganya Rais yuko tayari kujiuzulu mwenyewe kabla kutangazwa na Rais.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kumradhi naomba kumjibu Mhe. Makame Mshimba Mbarouk swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Ninakuhakikishia Mhe. Spika, hakuna Waziri yeyote na wala hathubutu kumdanganya Mhe. Rais, kwa sababu pale kama nilivyosema Mhe. Spika, pale sisi tunakwenda na yale ambayo tumewasilisha kwenye kikao chako, tunachambua pale ule utekelezaji tu katika robo ile umetekeleza vipi ki pesa na kiutendaji sasa utamdanganya vipi. Na halafu watu wanafatilia kuona huko umetenda vipi. Sasa utamdanganya Rais mimi sifikiri kama kuna Waziri yeyote kwa hili hapadanganyiki, utakuja utakamatwa kama unazembea kwa hili zoezi lilivyokuwa.

UTARATIBU

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Waziri yuko tayari kujiuzulu kabla Rais kumtangaza.

Mhe. Spika: Unajua tunamwachia ajibu lakini ukitizama majibu yake kalijibu hili lakini hebu jibu Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Ninakushukuru sana kwa kunisaidia kujibu, haya majibu yangu niliyosema peke yake yana jawabu. Lakini nasema wewe umepewa uwaziri ukubali wakati wowote kuondoka umpishe mwenzio hakuna wasiwasi wowote.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ninakushukuru sana Mhe. Spika, kwa asubuhi ya leo kunipa fursa hii kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

Kwanza hakuna wasiwasi wowote ni kwamba sisi tunapongeza sana ziara za Rais katika kuwaona watendaji moja kwa moja. Lakini kama *position* ya Waziri huyu, Ofisi ya Rais Baraza la Mapinduzi naomba nimuulize

kutokana na majibu yake aliosema uzito wa ziara na faida zake. Ni changamoto gani kubwa tatu ambazo yeye mwenyewe ameshuhudia katika mawizara tofauti ambazo zinawakwaza watendaji katika kufuatilia shughuli zao.

Pili, baada ya ziara hii Wizara yake inafanya tathmini yoyote ya mabadiliko katika haya mawizara au ndio ziara imekwisha aje adanganywe tena siku nyengine.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mheshimiwa Rashid Seif Suleiman wa Jimbo la Ziwani swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, kwa kweli baada ya Wizara zote kuwasilisha ripoti zao mbele ya Mhe. Rais, Makamo wa Kwanza, Makamo wa Pili pamoja na Katibu Mkuu Kiongozi, hufanyika kikao cha tathmini na Wizara ya Fedha. Maana yake Wizara ya Fedha wao hasa ndio wenye mambo yote tuseme wenye mshiko na wenye mipango. Sasa kufanywa tathmini na wao na yale yote ambayo Mhe. Rais, Makamo wa Kwanza, Makamo wa Pili, Katibu Mkuu Kiongozi waliyoyapata kutoka Wizara mbali mbali wanaambiwa Wizara ya Fedha na wao sasa wanaelekezwa mapungufu na changamoto zote na jinsi ya kupata *the way forward*, ninafikiri nimejibu hivyo.

UTARATIBU

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, swali langu namba (a) halijajibiwa.

Changamoto tatu kubwa ambazo kutokana na Wizara yake ilivyo mawizara inawakwaza katika kutekeleza kazi zao.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Ninamshukuru sana Mhe. Rashid Seif. Kwa kweli Wizara yangu changamoto niliyoipata ni ukubwa wa Wizara yangu na utekelezaji wake kidogo ni suala gumu linatupa kazi katika utendaji wa Wizara yetu, ukubwa na ufatiliaji na zile *ceiling* ya pesa tulizopewa ninashukuru pesa zote tulizotaka tunapewa na tumefika asilimia thamanini kwa kweli. Lakini kwa shughuli zilivyo za ukubwa wa Wizara yangu hazitoshi hiyo ndio changamoto kubwa ambayo nimeipata kwa Wizara yangu.

Nam. 37

Umuhimu wa Elimu kwa Watumishi wa Umma

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-

Kwa kuwa Elimu ni njia moja inayomfanya mtumishi wa umma kuwa mbunifu, makini na mahiri katika shughuli zake za uytendaji. Na kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na taasisi ake na zile zisizokuwa za Kiserikali huwalipa watumishi wao mafao pamoja na stahiki nyengine za utumishi kwa mujibu wa taaluma walizonazo. Na kwa kuwa watumishi hawa hupata elimu zao katika vyuo vya ndani na nje ya nchi kwa njia ya moja kwa moja madarasani, elimu madarasani, elimu masafa au kupitia mitandao.

Je ni sababu gani za msingi zilizopelekea serikali kutotambua shahada, stashhada, na vyeti vinavyotolewa na Chuo Kikuu cha ST. CLEMENT UNIVERSITY cha Italy chenye matawi yake katika nchi mbali mbali.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake nambari 37 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, napenda kumjumlisha mwakilishi kwamba kila nchi imejiwekea utaratibu wake katika mfumo wa elimu sio vyuo vyote vinavyotoa mafunzo nje vinavyokuja Tanzania vinakubalika kutoa mafunzo. Lazima kwanza vyuo hivyo visajiliwe na kuhakikisha kwamba mafunzo watakayoyatoa yanakubaliana na mfumo wetu wa elimu.

Aidha ili vyuo vikuu vikubalike kufanya kazi Tanzania vyeti vyake lazima vitambulike kukubaliwa na kupata usajili wa kamisheni ya vyuo vikuu vya Tanzania yaani TCU. Mhe. Spika Kamisheni hii imeanzishwa rasmi kwa mujibu wa sheria za vyuo vikuu vya Tanzania namba 7 ya mwaka 2005 na kukabidhiwa jukumu la

kutathmini na hatimae kutambua au kutotambua shahada zinazotolewa na vyuo vya elimu ya juu kutoka nje ya nchi.

Kazi ya kutathmini shahada hizo ni mchakato uanofanywa kwa lengo la kuhakikisha kwamba shahada zinazotolewa na vyuo kutoka nje ya Tanzania ni ithibati kwamba ujuzi, maarifa na elimu inayotolewa na vyuo hivyo inalingana na vipimo vilivyowekwa nchini kwetu.

Mhe. Spika, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora inazo taarifa rasmi kutoka TCU kwamba Chuo Kikuu cha ST. CLEMENT ni miongoni mwa vyuo visivyotambuliwa na kwa hivyo shahada, stashhada na vyeti vyote havitambuliwi. Ili kuepusha usumbufu kwa watumishi wetu wanaotaka kujiendeleza, Wizara yangu imeto orodha ya vyuo vikuu vyote vinavyotambuliwa na TCU na NACTE na kuwaomba watumishi wavitumie vyuo hivyo katika kujiongezea elimu.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, napenda nimpongeze sana Mhe.Waziri kwa majibu yake yenye ufasaha wa hali ya juu. Sasa naomba nimuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa vijana wetu inawezekana sana ambayo Mhe. Waziri kaitoa hawanayo je haoni kuna haja ya orodha hiyo kuipeleka katika ofisi zote za elimu ili vijana wetu wawe na *awareness* ya kutosha kuhusu orodha hizo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, nakualiana nae kweli vijana wetu wengi hawana uwelewa huo, lakini hatua ya mwanzo ya Wizara yangu ilipeleka taarifa kwenye Wizara na taasisi zote za Serikali ili kuwatanabahisha watumishi wa umma. Hata hivyo nakubaliana nae kwamba Wizara kwa kushirikiana na wizara ya elimu na mafunzo ya amali itafanya kazi hiyo ya kupeleka taarifa hizi kwenye taasisi za elimu.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Ninakushukuru sana Mhe. Spika, kunipa fursa na mimi nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza. Kwa kuwa chuo hichi kipo hapa Tanzania na kinafanyakazi na kwa kuwa Serikali ndio yenye milki ya kuzuia au kuruhusu na wakati wanaona chuo hiki kinachosomesha hakitambulikani na hawakijui kwa shahada zake, kwa nini chuo hichi kikaachiwa kikaendelea kusomesha. Na je kuachiliwa kikawa kinaendelea kutoa hiyo elimu kwa watu wetu, hatuoni kama watu wetu wanaona kama chuo hichi kinatambulikana na ndio maana wakafuata. Kama ni hivyo ni lini serikali itazuia hicho chuo kusomesha ili wanafunzi wetu au watumishi wetu wasende kujifunza katika chuo hicho.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Subeit mwakilishi wa wananchi jimbo la Micheweni suala lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Kwa kuwa Mhe. Subeit amesema mbele ya Baraza lako tukufu kwamba chuo hiki kinaendelea na kutoa mafunzo hapa nchini petu, basi Serikali itafuata ushauri wake wa kuweza kuchukua hatua kama kweli chuo hicho kinatoa mafunzo basi hatua za kisheria zitachukuliwa ili kudhibiti tatizo hilo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kuweza kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kuna chuo ambacho kimeshafanyiwa usajili kutoka Dar es Salaam mpaka hapa kwetu Zanzibar kwa mujibu wa sheria yetu, lakini Wizara yako ambayo imekataa shahada zake ili kuzipokea kutokana na wale, je Mhe. Waziri kama ni kweli uko tayari hawa watu mimi nikuletee mwenyewe uone ili tatizo hili kulitatua.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Makame Mshimba swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe.Spika, kama kweli kipo chuo ambacho kimepatata usajili kupitia taasisi husika na bado Serikali imezuia mimi siamini hivyo, lakini kama kipo ninamuomba akilete ili tuone hicho kibali cha usajili wao tuweze kufanyia kazi.

Nam. 58

Mgombea Urais wa Muungano

(Mheshimiwa Mwakilishi aliyetaka kuuliza swali hili ameliondoa)

Nam.8

Ukarabati wa barabara za mjini Zanzibar

Mhe. Ali Salum Haji - Aliuliza:-

Kwa bahati nzuri Serikali yetu imekuwa ikijitahidi kuzifanyia ukarabati barabara mbali mbali za Mjini.

a) Je Mhe. Waziri ni sababu gani zilizopelekea kwa muda mrefu kutokamlizwa barabara ya Mikunguni Shell, Mwembenjugu na Kwaalimsha – kwa Jumapweza.

b) Je, huoni kitendo cha kufikia kutia roj ya lami barabara hizo na kuziacha mpaka lami hiyo kupotea na kuchimbuka upya ni kuitia hasara Serikali zisizokuwa na ulazima.

c) Je, Mhe. Waziri kuziacha barabara hizo katika kiwango cha lami rojo kwa muda wa miezi 4 na baadae kuziacha na kuanza barabara ya Kinazini – Malini huni kama Wizara yako haina mpangilio mzuri wa kazi za ukarabati wa barabara.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi wa Jimbo la Kwahani swali lake kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, Barabara inayotoka Mikunguni Sheli hadi Mwembenjugu na ile inayotoka Kwaalimsha mpaka kwa Jumapweza zimekusudiwa kufanyiwa matengenezo ili barabara hizo ziweze kupitika kwa urahisi kwa wakati wote. Ni kweli barabara hizo zimechelewa kumalizwa matengenezo yaliyokusudiwa ambayo barabara ya Mikunguni hadi Muembenjugu tayari imeshajengwa kwa tabaka la mwisho la kifusi (base course) na kuwekwa lami ya maji ili isichimbuke wakati ikisubiri kuwekwa lami ngumu. Uwekwaji wa lami kwa barabara hiyo na ile ya Kwaalamsha hadi kwa Jumapweze imechelewa kutokana na kuharibika kwa mtambo wa kupikia lami ya zege yaani *asphalt plant*. Hata hivyo maandalizi ya ukamilishaji wa barabara hiyo yalifanywa ambayo kwa sasa itawekewa lami ya *surface dressing* kwa barabara zote mbili. Na utaratibu huo tuna matarajio utafanyika katika kipindi cha wiki mbili.

Mhe. Spika, haikuwa azma ya Wizara kuziacha barabara hizo kwa kutia lami ya rojo kwa muda mrefu isipokuwa kuharibika kwa mtambo ndio kulikopelekea kukaa kwa muda huo mrefu pasi na kukamilisha kwa kazi hiyo.

Kuanza kwa kazi za matengenezo ya barabara ya Kinazini – Malindi haimaanishi kuwa kutokuwa na mipango mizuri na endelevu ya Wizara yangu.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, nimshukuru sahiba wangu kwa majibu mazuri tu aliyonieleza na pia nimepata matumaini ya kunambia kwamba barabara hiyo itamaliza katika kipindi hiki kwa haraka sana kwa sababu tayari imeleta usumbufu na kuathiri afya za watu na kuleta kadhia kufikia hadi barabara hiyo kuifunga katika kipindi cha karibuni kwa kuweka mawe makubwa kutokana na watu wengi kuanza kukohoa na kupata maradhi ya kifua.

Lakini Mhe. Spika, swali langu lipo hapa, kwamba barabara hiyo katika jitihada nzuri za Serikali walizozifanya iliparwa ikatiwa kifusi ikafika kutiwa lami, tatizo lipo hapa ambalo linasema kwamba wanatia gharama Serikali. Sababu gani zilizopelekea baada ya kutiwa rojo kuja kuichimbua tena upya na kuitia kifusi.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, ni kweli kwamba barabara hiyo ilikuwa ni ya lami mwanzo na ilikuwa ishakuwa mbovu na sehemu nyingi zilikuwa na mashimo ikenda ikaburugwa ikawekwa kifusi tabaka la kwanza, tabaka la pili, tukaweka praim, lakini kwa bahati mbaya wakati inawekwa praim ni kipindi cha mvua. Baadae ikaonekana kwamba haikukaa vizuri na kwa sababu tunataka kujenga barabara yenye kiwango itakayokuwa madhubuti tukaona tuongezee kifusi cha juu ili sasa mipango yetu baada

ya kukamilika kwa mtambo ule uliokuwa umeharibika, mategemeo yetu katika kipindi cha wiki mbili, barabara hii ya Mikunguni mpaka Muembenjugu, Kibonde mzungu, Kikwajuni na Kihinani Bububu zote tutakuwa tumeshazikamilisha kwa ujenzi wa lami.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, Mhe. Naibu Waziri utakubaliana nami kwa hivi sasa Wizara yako imekuwa ni kilema na sijui kwa makusudi inafanya utaratibu huu. Barabara ya Kinazini Malindi barabara ilikuwa ni nzima na uliivunja karibu siku kumi watu wa maduka ya Mchangani wakawa wanachezea mavumbi tu. Ulipokuja kujibu katika kikao kilichopita ulisema *disel* imekwisha, leo unakuja kutwambia mtambo wa kupikia lami umeharibika mtambo wenyewe ni mmoja. Ni lini utakuwa muwazi katika jawabu zako unazotoa hapa mbele ya wananchi wanaotusikiliza huko.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, hapa ninachukua nafasi kidogo kumueleza Mhe. Jaku kwa mapana. Mhe. Spika, suala alilouliza Mhe. Jaku katika Baraza lililopita aliuliza kuhusiana na barabara ya Kinazini. Barabara ya Kinazini alikuwa na madai kwamba muda mrefu inarusha vumbi watu wa mjini hawajazoea kuingia vumbi yeye akiwa miongoni mwao. Sasa Mhe. Spika, tulichomueleza kwamba barabara ya Kinazini tunajenga na tunajenga kwa fedha za Serikali, kulikuwa kuna mapungufu ya fedha yaliyopelekea barabara ile kuchelewa katika muda ule. Lakini pia mtambo wetu ambao tulikuwa tukifanyia kazi uliharibika, tukamueleza sababu hali ilipotengamaa ya fedha, mtambo uliporudi katika hali ya kawaida tukamaliza kazi.

Kinachozungumzwa barabara ya Mikunguni ni kwamba tulikuwa tumefikia hatua nzuri kikwazo kilikuwa nini kilichopelekea tusimalize barabara ilikuwa tatizo la mtambo na mtambo umerudi katika hali yake ya uzima. Tumeshamuahidi Mheshimiwa kwamba katika kipindi cha wiki barabara tulizozitaja ikiwemo ya Kikwajuni, Kibondemzungu Kihinani na hii ya Mikunguni pamoja na kwa Jumapweza zitakuwa zimetengenezwa. Sasa kama Mhe. Mwakilishi atakuwa na jengine la ziada ambalo halihusiani na fedha nitakuwa silifaham. Lakini sababu za msingi ambazo tumeelezwa na watendaji wetu ambazo sisi tumeridhika baada ya kuziona ni hizo.

Nam. 6

Utoaji wa Risiti baada ya kulipia huduma za Afya

Mhe. Mussa Ali Hassan - Aliuliza:-

Pamoja na jitihada za Serikali ya Mapinduzi, Zanzibar kuwashajihisha wananchi kuomba risiti endapo watapatiwa huduma yoyote, bado kuna baadhi ya Taasisi za serikali ambazo hutoza malipo kwa hudum wanazxitoa vila ya kutoa risiti.

a) Je, Mhe. Waziri unafahamu kuwa baadhi ya vitengo kwenye Wizara yako zikiwem,o sehemu za kliniki ya wajawazito. Sehemu ya Masikio, Pua Mdomo na kadhalika hazitoi risiti kwa malipo wanayopokea.

b) Je, Wizara yako ina mpango gani wa kulittua suala hili ili kuziba mainya ya upotevu wa fedha za wavuja jasho wan nchi hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Spika,napenda kukushukuru kwa kunipa tena fursa hii lakini kwanza napenda nitoe shukurani zangu kwa Mhe. Rais kutuongezea nguvu za wanawake katika Baraza letu kwa kumteua Mhe. Marina kuja kuungana nasi karibu sana Marina.

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi wa Jimbo la Koani swali lake namba sita kama hivi ifuatavyo:-

a) Idara ya hospitali ya Mnazi mmoja ina vitengo kadhaa ambavyo hutoa huduma za kuchangiwa. Huduma ambazo huchangiwa na vitengo mbali mbali vikiwemo vya pua, koo, masikio, macho pamoja na kliniki za wajawazito hutolewa risiti. Kama kuna kitengo ambacho kinapokea fedha bila ya kutoa risiti Wizara haina taarifa na wala haijapokea malalamiko kuhusu suala hilo.

b) Wizara ya Afya kwa kushirikina na Wizara ya Fedha tumekubaliana kuwe na utaratibu maalum wa ukusanyaji wa fedha utakaowezesha kuwa na sehemu kuu mja malipo (*centralized collection*

point). Utaratibu huu utasimamiwa na wahasibu ambapo mfanyakazi wa afya hatahusika na ushikaji wa fedha.

Ili kuweza kufanyakazi kwa masaa 24 tunahitaji wahasibu 8 kwa sasa tuna wahasibu watatu na upungufu wa wahasibu watano. Kwa hivyo hao waliopo wamewekwa kwenye zile sehemu nyeti tu. Hata hivyo Wizara inatoa wito kupitia Baraza lako tukufu na kwa kuwatahadharisha wananchi na wafanyakazi wa afya kwa yeyote ambaye anachangia huduma lazima atoe risiti.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante ninashukuru kwa majibu mazuri ya Mhe. Waziri, nataka kujua ni lini sehemu zote za vitengo zitakuwa na risiti za kuwapa wananchi na kama mwananchi hakupata risiti ya malipo hatua gani itachukuliwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kama nilivyoeleza kwamba ili tuweze kukikamilisha hicho kitengo ambacho kitafanya kazi ya kukusanya mapato ya hospitali ya Mnazimmoja tunahitaji wahasibu wanane kwenye mzunguko wa masaa 24. Hatutoweka kila kitengo mtu isipokuwa wale watu watakuwepo katika sehemu maalum na mtu yoyote atakayekwenda katika sehemu husika atapewa kile cheti cha maombi. Kwa mfano kama anakwenda maabara ataandikiwa basi *form* ya maabara. Akishaandikiwa *form* ya maabara atakwenda kwenye ile sehemu ambayo anatakiwa kulipa atalipa pale. Pale atapewa risiti na *form* yake ndipo atapokwenda maabara akapewe huduma inayostahiki.

Kwa hivyo sitegemei kama hayo yatatendeka kutakuwa na haja ya kuchukuliana hatua kwa sababu kila jambo litakwenda kwa utaratibu wake.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, kama swali la msingi lilivyojielekeza ziko taarifa kwamba kuna uvujaji mkubwa wa mapato kupitia katika hospitali za serikali hasa hospitali ya Mnazimmoja na kwamba kwa mapato yanayopatikana pale yanatosheleza kabisa kuendesha hospitali hii bila kupata ruzuku yoyote kutoka serikalini.

Sasa kwa sababu taarifa hizi zinaripotiwa, wizara iko tayari kuruhusu ukaguzi maalum kwa mkaguzi wa nje wa hospitali nzima ya mnazimmoja na mapato yake ili kujiridhisha kiasi gani cha fedha kinaingia na kiasi gani kinapotea ili kuzinusuru pesa za walipa kodi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, sina hakika ya kwamba kuna mapato yanavuja, kama tulivyosema hatuna taarifa wala hakuna aliyekuja kushtaki, lakini taratibu za *audit* hizo sizifahamu kwamba kama inaweza kutoka *audit* nje ikaja pale ikafanya mambo, labda Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo unisaidie kwa sababu masuala ya fedha si yangu.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri labda nisaidie kidogo Mhe. Ismail Jussa. Kwanza katika suala zima la *audit* kuna hatua mbili, hatua ya kwanza ni kwa *Internal auditor* ambaye kila taasisi wanaye mkaguzi wa ndani. Huyu yeye anapaswa kuzipitia hesabu zote pamoja na matumizi yote yaliyofanywa na taasisi ile na yeye kama anaona kuna dosari basi kabla ya mkaguzi wa nje hajafika anatakiwa amuafrifu Katibu Mkuu ili Katibu aweze kuchukua hatua na tahadhari.

Lakini katika hatua ya pili kuna mkaguzi wa nje ambaye ni *external auditor* anatoka katika Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu. Kwa hivyo, nadhani katika hatua hizi zinatosha kuweza kujua kwamba kama kuna upotevu au hakuna upotevu na hatua kamili zinaweza kuchukuliwa pale ambapo *external auditor* amebaini kuwa kuna upotevu wa fedha katika taasisi ile.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, wananchi wa Zanzibar wamekuwa wakilalamika sana pale wanapotoa michango yao katika Hospitali ya Mnazi Mmoja na baadae wakiona hatua za mafanikio hazipatikani. Hivyo wamekuwa wakidai kwamba kuna upotevu mkubwa wa fedha za umma pale katika Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Kwa mafano, mwaka jana wizara yake Mhe. Naibu Waziri ilitukisia makisio ya shilingi 57 milioni, lakini ilivyokwenda kamati iligundua kwamba kuna makusanyao ya shilingi 500 milioni, mwaka huu shilingi 190 milioni hawakuleta kwenye Kamati ya Maendeleo ya Ustawi wa Jamii hadi pale kamati ilipoomba ndio baadae wakatuletea orodha na wakakiri kwamba wanao uwezo wa kukusanya shilingi 190 milioni kwa pale tu katika Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Je, kwa nini Mhe. Naibu Waziri kitengo chake cha fedha kimekuwa na tabia ya kuficha mahesabu ya umma na hivyo je, watu hawa wana sifa ya kuwa wahasibu

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, tuliyoyasema kwa taratibu za mahesabu ni kweli, labda nikubaliane naye kwa uelewa wangu mdogo nilionao. Lakini wahasibu sisi Wizara ya Afya tunaletewa kutoka Wizara ya Fedha. Sasa kama wana kiwango kidogo mimi sina mamlaka ya kusema kwa sababu kama kitu hukijui utasemaje? Huyu ana kiwango kidogo au kikubwa? Kwa hivyo, kama mna mashaka nao tafuteni utaratibu unaokubalika muulize wanaohusika waje wawaangalie kama hawafai waondoshwe, mimi hizo pesa nazitaka kuliko unavyozitaka wewe sina la kufanya kwa mhasibu atakaeletwa ndiye tutakayempokea.

Nam. 133

Wanawake Kujiunga katika Vikundi vya Ushirika

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa – Aliuliza:-

Kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2002, idadi ya wanawake kwa Mkoa wa Mjini/Magharibi ni kubwa zaidi kuliko wanaume. Imebainika kuwa wanawake wako mstari wa mbele katika shughuli mbali mbali za nchi ikiwemo kujitokeza kwa wingi wakati wa kupiga kura, wadumishaji wakubwa wa amani na wapenda maendeleo.

Mwanzoni mwa Serikali ya Awamu ya Saba wizara yako iliwahimiza wanawake wajiunge katika vikundi vya Ushirika ili serikali iweze kuwapa elimu na mikopo katika juhudi za kuwapunguzia umasikini.

(a) Je, Mhe. Waziri mpango huo umekwamia wapi.

(b) Je, Mhe. Waziri unaweza kulieleza Baraza hili ni vikundi vingapi vya kinamama ambavyo vimeshapatiwa mikopo tangu kaulimbiu hiyo ilipotolewa.

(c) Je, Mhe. Waziri unawapa matumaini gani wanawake wa Mkoa wa Mjini/Magharibi ambao tayari wameshasajili vikundi vyao vya ushirika na bado havijapata mkopo.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika – Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa swali lake lenye vifungu a, b, na c kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, mpango huo haujakwama na bado unaendelea.

(b) Hadi hivi sasa kikundi kimoja cha Mkoa wa Mjini/Magharibi ambacho kimeomba mkopo katika Idara ya Mikopo na ambacho kimepewa taaluma na kufanyiwa uhakiki kipo katika hatua ya kufunga mkataba na kupewa mkopo huo.

(c) Kwa wale ambao tayari wamesajili vikundi vyao vya ushirika na bado havijapata mikopo nawashauri wapeleke maombi yao ya mikopo katika Idara ya Mikopo iliyopo Vuga kwa kufanyiwa kazi.

Mhe. Nassor Ali Salim: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Katika majibu yake Mhe. Waziri amesema kwamba ni kikundi kimoja tu ambacho kimefaidika. Je, ni sababu zipi zilizofanya kikundi kimoja tu ndio kifaidike.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, kama nimemfahamu vizuri Mheshimiwa anauliza kwa nini kimekuwa ni kikundi kimoja tu. Kama ni hivyo basi niseme waliopata mikopo katika Mkoa wa Mjini Magharibi jana nilieleza Mhe. Spika, wanawake ni 176 kwa mmoja mmoja, lakini kwenye kikundi cha ushirika ambacho kimesajiliwa ni hiki kikundi kimoja ambacho kimeomba na kimepatiwa na vyengine ambavyo havijaomba waombe ili wapatiwe mkopo huo Mhe. Spika.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, namuuliza Mhe. Waziri kwa kuwa vikundi hivi vya wanawake vimeenea Unguja na Pemba. Ni sifa gani zinazotakiwa zaidi za vikundi ili waweze kupata mikopo.

Lakini swali la pili ni baada ya mwaka mzima sasa hivi tangu kuingia bajeti iliyopita Mhe. Waziri anajibu kuwa kikundi kimoja tu ndicho chenye matumaini ya kupata mkopo. Je, hali hii inaridhisha kwa wizara yake.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, ningemuomba Mhe. Rashid Seif akafanya ziara katika Jimbo lake la Ziwani, kwa sababu kuna vikundi vingi sana vimesajiliwa na vipo ambavyo vimepata mikopo katika hilo eneo ninalolizungumza la Jimbo la Ziwani. Lakini vikundi ambavyo vimepata mikopo jana nilivisema hapa hadharani Mhe. Spika, vikundi vya *SACCOS* ni 10, wananchi mmoja mmoja (wajasiriamali) karibu 720 na mikopo hii ni kwa kipindi cha miezi tisa tu, lakini huko nyuma mikopo hii imetolewa kwa vikundi vingi sana.

Tumejaribu kutafuta vikundi vyote vya ushirika sasa hivi, tunaviangalia utaratibu na uhalali wake tumegundua kwamba vikundi vingi vimekufa kwa sababu hawakufuata zile taratibu zilizowekwa huko nyuma. Sasa hivi tumevisajili tena na karibu vikundi 1200 tumeshavihakiki na tayari sasa hivi tumevielekeza viombe mikopo kwa utaratibu wa kupatiwa mikopo. Kwa vilivyopatiwa mikopo ni vingi lakini hiki ni kikundi maalum cha Mkoa wa Mjini Magharibi ambacho kiliomba haina maana kwamba ni kikundi kimoja tu ambacho kimepata mkopo, kwa hiki ni *particularly* ambacho kiliuliziwa swali.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri anambie katika Wilaya ya Kusini Pemba ni vikundi vingapi ambavyo vimefaidika na mikopo na vingapi ambavyo katika wilaya hiyo havijafaidika. Vile vile kuna vikundi vingapi ambavyo vimeomba mikopo katika wilaya hiyo.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, namuomba swali lake hilo alilete kwa maandishi na mimi nimjibu kimaandishi kwa sababu sasa hivi siwezi kuwa na kumbukumbu hiyo, lakini vikundi viko vingi na kama nilivyomshauri Mhe. Rashid Seif nadhani na yeye Mheshimiwa angefanya ziara ya kwenda kuvikagua vikundi na vingi tumevisajili na katika eneo ambalo tumesajili vikundi vingi hasa ni ile mikoa miwili ya Pemba Kusini na Kaskazini.

Nam. 20

Ukosefu wa Nishati ya Umeme Pembeni Mtemani

Mhe. Hassan Hamad Omar – Aliuliza:-

Watu wa kijiji cha Pembeni Mtemani, katika Jimbo la Kojani walikatiwa miti yao kama vile minazi, miembe, mikarafuu na miti mingine kwa ajili ya kupatiwa huduma muhimu ya Nishati ya Umeme na mpaka sasa ni miaka minne (4) imepita na huduma hiyo haijapatikana.

(a) Mhe. Waziri ni sababu gani mpaka kufikia leo hii wananchi wa vijiji hivyo hawajapatiwa huduma hiyo ya umeme na kuweza kufaidika.
(b) Ni lini wananchi hao watarajie kuipata huduma hiyo ya umeme, ukizingatia muda umekuwa mrefu sasa tangu hatua za ukataji wa miti zilipoanza.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:-

Ahsante Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 20 lenye vifungu a na b kama hivi ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, kijiji hicho cha Pembeni Migurani tayari kimeshavutwa laini ya Umeme mkubwa (*H.T.*) kilomoita 1.2 na laini ya *L.V.* mita mia tatu, lakini kutokana na uhaba wa transfoma kazi hiyo haikukamilika kwani kulijitokeza kuungua kwa transfoma zaidi ya nane katika vijiji mbali mbali. Kwa hivyo, Shirika la Umeme lililazimika kushughulikia transfoma hizo kwanza.

b) Kwa kuwa mahitaji ya transfoma ni makubwa kwa vijiji vingi, shirika litazingatia uwezekano wa kuweka transfoma katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa sababu jambo hili ni la muda mrefu na anasema *process* zimeshaanza ni lini wananchi wa Pembeni watarajie shughuli hiyo muhimu ya nishati ya umeme itawafikia na kutumika.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kama nilivyojibu katika swali mama kwamba katika kipindi cha bajeti cha 2012/13 tutawasilisha transfoma na tutahakikisha kwamba kijiji hicho tunakipatia umeme na wananchi wananufaika na umeme huo. Na sio kijiji hicho tu, pamoja na vijiji vyengine ambavyo vimebakia.

Lakini vile vile Mhe. Spika, nina masikitiko makubwa sana na baadhi ya wananchi wanaodharau miundombinu, ningewaomba waelewe kwamba serikali inapojenga miundombinu katika kijiji chochote basi malengo ni kuwanufaisha wananchi wenyewe. Nasikitika na wananchi wa Kijiji cha Pembeni Migurani, kwamba kuna mwananchi kakata mfenesi na mfenesi huo ukaangukia kwenye laini yetu ya umeme ya *LV* na laini hiyo hatimaye ikaanguka chini yote. Mwananchi huyo bila ya kutoa taarifa Shirika la Umeme basi laini hiyo imekaa chini kwa muda mrefu mpaka nilipotembelea mimi mwenyewe na nikenda nikaiona iko chini ndipo nikafanya juhudi pamoja na watu wangu wa Shirika la Umeme siku ya pili wakenda kuishughulikia laini hiyo.

Kwa hivyo, ningeomba sana wananchi wajaribu kuthamini miundombinu yetu kwa sababu haya yote ni maslahi kwa wananchi si kwa maslahi ya watu wengine. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Mhe. Hassan Hamad Omar kazi hiyo sasa mpira uko kwako. Tunaendelea.

Nam. 93

Ushiriki wa ZFA katika Shirikisho la Soka Duniani (*FIFA*)

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Mhe. Spika, kabla ya kuuliza swali naomba kumpongeza waziri dhamana wa wizara hii kwa vitendo alivyofanya juzi kwa Timu ya Taifa kumkabidhi kila mchezaji shilingi laki mbili na nusu nimpe hongera sana. Vile vile kwa kukutana na maulamaa jana kujadili mustakabali wa nchi yetu hii. Mhe. Waziri hongera sana.

Mnamo mwezi wa Juni 2011 Shirikisho la Soka Duniani (*FIFA*) lilitoa msimamo kuwa Zanzibar haiwezi kuwa mwanachama kwa vile sio taifa na kuendelea kutambulikana kuwa mwanachama kupitia Shirikisho la Soka Tanzania (*TFF*) kama sehemu ya Jamhuri Muungano wa Tanzania.

(a) Je, ni lini Katiba ya *ZFA* na *TFF* itafanyiwa marekebisho ili uongozi wa *TFF* uwe na viongozi kutoka Zanzibar ili kuleta sura nzuri ya Muungano.

(b) Kwa kuwa lengo la kupata Uanachama wa *FIFA* halijafikiwa ni lini Ligi Kuu ya Muungano itarudishwa ili kufufua hamasa ya mchezo wa soka kama ilivyokuwa miaka ya nyuma.

(c) Endapo *FIFA* itatoa Ruzuku ya Dola 250,000 kila mwaka kwa maendeleo ya mchezo huo kwa nchi wanachama. Je, *ZFA* itanufaika vipi kwa fedha hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 93 lenye kifungu a, b na c kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, napenda kukiri kwamba Shirikisho la Soka Duniani (*FIFA*) limetoa msimamo kuwa Zanzibar haiwezi kuwa mwanachama wa shirikisho hilo kwa kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo ni mwanachama wa *FIFA* ndio inayojulikana kuwa ni Taifa na Chama cha Soka cha Tanzania (*TFF*) ndicho kinachowakilisha taifa hilo.

Mhe. Spika, baada ya kutoa ufafanuzi huo, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, hivi sasa hakuna juhudi zozote zinazofanywa za kurekebisha katiba ya Chama cha Soka cha Zanzibar (*ZFA*) na Chama cha Soka cha Tanzania (*TFF*) kwa lengo la viongozi wa Zanzibar kuwa ndani ya Chama hicho cha *TFF* ili kuleta sura nzuri ya Muungano. Juhudi hizo hazijachukuliwa kwa sababu michezo si miongoni mwa taasisi za Muungano na pia Zanzibar ingali inapendelea kuendesha shughuli za michezo kwa kujitegemea yenyewe.

b) Hakuna mpango wa kurejesha Ligi Kuu ya Muungano, kurejesha ligi hiyo maana yake ni kupata bingwa wa Tanzania atakayeshiriki katika mashindano ya Klabu Bingwa na Mshindi wa pili

kushiriki katika Kombe la Washindi Barani Afrika. Zanzibar tayari inashiriki katika mashindano hayo, hivyo kuwepo kwa ligi kuu ya pamoja kati ya Zanzibar na Tanzania Bara kunaweza kuipotezea fursa ya Zanzibar ya kushiriki kwenye michuano hiyo. Hata hivyo, kwa kuwa kinachotafutwa ni kufufua hamasa ya mchezo huo, tayari juhudi zimeanza kuchukuliwa na kuanzisha mashindano mbali mbali yanayozijumuisha timu za Tanzania Bara zinazosifika. Michuano hiyo ni pamoja na mashindano ya Kombe la Mapinduzi na Kombe la Urafiki litakalokuwa likizishirikisha pia timu kutoka Misri.

c) Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo inajitahidi kuwasiliana na wizara inayohusika na michezo Tanzania Bara kwa ajili ya kubuni na kuweka utaratibu utakaoifanya Zanzibar kunufaika endapo *FIFA* itatoa ruzuku ya fedha au vifaa kwa *TFF*.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Spika, ninavyofahamu mimi katika mgao huu wa *FIFA* Zanzibar tunaneemeka na kitu kimoja tu, nyasi za bandia katika uwanja wa Gombani na uwanja huo haujamalizwa mpaka hivi sasa sehemu ya tatani ya kukimbilia riadha na mchezo huo una umuhimu wake. Je, utamalizika lini.

Pili, kwa kuwa waziri wetu mpya ni mpenda michezo na matunda yake tumeyaona, kuna fununu kuwa kuna timu zilizoshuka daraja ikiwemo Kiski Kikwajuni, Mundu na Polisi kuna msamaha huo. Je, ni kweli Mhe, Waziri suala hilo ili michezo ipate kuendelea.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, Mhe. Jaku kwa kweli suala hili kipindi kilichopita japokuwa hakuliuliza yeye lakini tulitoa ufafanuzi wa kutosha. Nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi kwa heshima na taadhima tunapoliuliza swali kipindi kinachokuja tutafute maswali mengine ya kuuliza, sio kama nawasimbulia waheshimiwa, lakini nawaomba sana maswali yasijirejee ni bora kutuuliza masuala yenye umuhimu mkubwa sio kurudia maswali yale kwa yale. Kwa sababu maswali haya tumeshatoa ufafanuzi wa kutosha na tukatoa ufafanuzi wa kina na kueleza kwa ufasaha zaidi Mhe. Spika.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, hapa tumekuja kuwawakilisha wananchi na wananchi wanatusikiliza swali kama halijajibiwa itabidi tuliulize. Mhe. Waziri wa Afya aligaragara hapa na *ICU* na tukafika pahala pazuri Mhe. Spika. Kwa hivyo, ninachosema kwamba sisi tumetumwa na wananchi na tumekula viapo kutumikia wananchi.

Mhe. Spika: Mimi nafikiri alichosema Mhe. Naibu Waziri ni sawa, hatuwezi tukarejea maswali hayo hayo kila wakati si utaratibu. Na kweli hata katika orodha ya maswalia wakati mwengine unakuta swali limejibiwa leo kwa mfano la Mhe. Jaku Hashim lakini katika kioo kile kile kuna mwengine naye anauliza swali hilo hilo. Sasa si utaratibu kwa kweli, nadhani tukubaliane na kile alichokisema na twende hivyo. Kwa mfano, kulitajwa muda na ule muda sasa umepita kwamba kitu hiki kitamalizika tarehe fulani na bado ikawa hakijamalizika hapo unaweza ukarudia kuuliza swali lile lile vipi muda mbona umepita.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu aliwahi kuuliza hapa nimesahau kidogo kwamba kwa muda wa miezi minne jambo fulani litekelezwe muda ukapita. Sasa anauliza tena lini litamalizika suala hilo kwa sababu kulikuwa na muda maalum. Kwa hivyo, kitu cha aina hiyo unaweza ukauliza tena kwa sababu ule muda uliokuwa umeahidiwa umekwishapita. Kwa hivyo nadhani ni utaratibu kwamba huwezi ukauliza swali hilo hilo wakati wote na majibu yakawa ndio hayo hayo.

Hata hoja zetu kama kuna hoja ilizingatiwa basi hoja hiyo haitakiwi kurudiwa tena labda kwa hoja maalum kutaka kufuta uamuzi ule hivyo ndivyo kanuni inavyoruhusu. Nadhani tukubali kwamba hilo limeshajibiwa.

Mhe. Nassor Ali Salim: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza nichukue fursa hii ya kumpongeza Mhe. Naibu Waziri kujibu majibu mazuri, lakini kwa kuwa katika majibu yake ameeleza kwamba vyama vyetu vya michezo (*TFF* na *ZFA*) vilabu vyake ambavyo vinashiriki katika mashindano ya mataifa ikiwemo Klabu Bingwa ya Afrika Mashariki. Lakini mbali na maelezo yake haioni kwamba ipo haja katika kudumisha Muungano wetu katika vyama hivi viwili kwa kushirikiana na Mabaraza ya Michezo ya pande zote mbili kuunda mashindano maalum ya kuwaenzi viongozi wetu wakuu ambao wameleta Muungano huu.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kwa kweli wazo lake si baya wizara italichukua na italifanyia kazi tukiona kwamba ni kwa maslahi ya kuendeleza mchezo wa mpira wa miguu hapa Zanzíbar basi shauri lake tutalifanyiwa kazi.

Nam. 24

Udhibiti wa Uvujaji wa Mitihani ya Taifa

Mhe. Hassan Hamad Omar – Aliuliza:-

Kwa kuwa Mitihani ya Kitaifa ya Kidato cha Nne (*Form IV*) huwa inasimamiwa na Taasisi ya Muungano ambayo ndio yenye wajibu wa kutunza siri na kuhakikisha kuwa maswali ya mitihani hayawezi kuvujishwa.

(a) Ni kwa nini serikali haiwaagizi wahusika kufanya uchunguzi wa kina ili kubaini sababu za kuvuja kwa mitihani hiyo na kuweza kudhibiti suala hilo.

(b) Ni kwa nini Baraza la Mitihani huwaadhibu zaidi wanafunzi wa Zanzibar kwa uvujaji huo.

(c) Ni lini serikali kupitia wizara yako inatarajia kulifanyia uchunguzi suala hilo ili wanaohusika kuweza kuadhibiwa badala ya kuwaadhibu wanafunzi pekee.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Nakushukuru sana Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kwanza kumkaribisha mwanamke mwenzetu Mhe. Marina Joel Thomas, namjua Mhe. Marina ni mwanamke msomi, jasiri na anayejituma na naamini kwa uwezo wake huo tutashirikiana naye pamoja wanawake wa Baraza hili kuondoa matatizo mengi ambayo wanayo wanawake wenzetu wa Zanzibar. Karibu sana.

Mhe. Spika, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 24 lenye sehemu (a) (b) na (c). Kwanza Mhe. Spika, naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama hivi ifuatavyo:-
Baraza la Mitihani la Tanzania ndio lenye wajibu wa kutunga, kusimamia, kutangaza na kutunuku vyeti vya Kidato cha Nne, cha Sita na Mafunzo mbali mbali ya Ualimu. Baada ya maelezo hayo sasa napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi kama hivi ifuatavyo:-

a) Wizara haikupata taarifa rasmi ya kuvuja kwa Mitihani ya Taifa ya Kidato cha Nne. Kulikuwa na madai ya baadhi ya wazazi ambao watoto wao walifutiwa matokeo yao kuwa mitihani imevuja, lakini madai hayo yametolewa baada ya Baraza kuchukua hatua ya kuwafutia matokeo hayo na kwa hivyo haukupatikana ushahidi wowote.

b) Baraza la Mtihani hutoa adhabu kwa watahiniwa wote waliobainika kufanya udanganyifu katika mitihani bila ya kujali sehemu wanazotoka au imani za watahiniwa za kidini. Mara hii ndio kumekuwa na idadi kubwa ya watahiniwa waliofutiwa matokeo yao kutoka Skuli za Zanzibar, lakini hatua kama hizo zimekuwa zikichukuliwa siku za nyuma kwa watahiniwa wa sehemu nyengine za Tanzania.

c) Wizara imewaandikia barua za kujieleza wasimamizi wa mitihani walioshukiwa kuwa walihusika katika kuruhusu watahiniwa kufanya udanganyifu. Barua za kujieleza za wasimamizi hao zimeanza kupokelewa na wizara na wizara itachukua hatua kwa kila mmoja kulingana na uzito wa kosa lake.

Pia, wizara imemwandikia Kamishna wa Polisi wa Zanzibar kumtaka kufanya uchunguzi juu ya kutopelekwa kwa karatasi za majibu kwa watahiniwa wa somo la *"Fine Arts"* kwa skuli tatu za Mkoa wa Mjini Magharibi. Pindipo polisi watapata ushahidi wahusika watashtakiwa kwa mujibu wa sheria. Baraza la Mitihani la Tanzania kwa upande wake liliunda Kamati ya Kuchunguza Udanganyifu katika Mitihani. Kamati hiyo imeshawasilisha ripoti yake kwa Baraza la Mitihani na wizara yetu imepokea ripoti hiyo hivi karibuni na inaifanyia kazi mapendekezo yaliyomo katika ripoti hiyo. Nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kwa kuwa tumeshuhudia mitihani hii ya kitaifa kuchapishwa kwake na mpaka kusambazwa kwake kufikia katika

vituo vya mitihani kunakuwa na ulinzi mkali kupita kiasi. Je, ni sababu gani zilizofanya kuvuja kwa mitihani hiyo na mpaka kumfikia mwanafunzi, kwa nini waadhibiwe waanafunzi na kuna mtu aliyeanza.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ninakushukuru sana Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Spika, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi kuwa, wizara haikuwa na taarifa kama kuna mitihani ambayo imevuja. Na kama Mhe. Spika, nimezungumza jana, hivi sasa kwenye nchi yetu kumekuwa na wimbi la matapeli wa mitihani ambao hukaa na kuumiza vichwa vyao, wakatunga mitihani na ndio mitihani ambayo inayovuja.

Mpaka hivi sasa hatujakua na ushahidi wowote Mhe. Spika, kama mitihani hii imevuja. Lakini kama ambavyo nilizungumza awali kuwa licha ya hawa wanafunzi wamepewa hii adhabu wizara imeunda kamati, Baraza limeunda kamati na nimesema awali hapa yeyote ambaye atahusika na kadhia hii basi si wanafunzi tu watakaochukuliwa hatua na walimu, wasimamizi na yeyote atakayehusika na kadhia hii hatua itachukuliwa Mhe. Spika.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri kwa kuwa Zanzibar ni nchi ni lini hasa Wazanzibari wataweza kufanya mitihani yao ya taifa inayotoka ndani ya nchi yao.

Mhe. Spika: Hili swali lipo nje lakini unaweza kumsaidia mheshimiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ninakushukuru Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Spika, kwa sababu suala hili ni suala la muungano itakapokuja Tume ya Katiba na tukaona hii kero kwa Wazanzibari, basi tutoe maoni yetu ili kuhakikisha suala hili linabakia Zanzibar na lisiwe la muungano.

HOJA ZA SERIKALI

Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi Ya Zanzibar Kwa Mwaka 2012/13

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, ninakushukuru sana kwa busara zako naomba univumilie nimalize dakika saba kama ulivyoniagiza.

Mhe. Spika, na yale majibu ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Makamo wa Pili Mhe. Waziri Mohamed Aboud baada ya kuulizwa maswali ya Mhe. Jussa na Mhe. Salmin Awadh. Mhe. Waziri kwa niaba ya serikali hadi asubuhi anatwambia kwamba serikali inaendelea na mazungumzo na wenzetu Tanzania Bara kwa ajili ya kupata maslahi, gesi, mapato ya Zanzibar yatazingatiwa. Lakini Mhe. Spika, mimi nimetishika, nimekwenda kwenye mtandao tena, nimeona majibu ya Mhe. Waziri ambayo mimi ninayaamini na Wazanzibari wanayaamini wamekwenda tofauti kidogo na majibu ya Ofisa mmoja wa TBC.

Mhe. Spika, naomba ninukuu haya maelezo ya huyu Afisa wa TBC. *There have been a number of meetings, and a committee as being set at those the issues but there are no meetings any more all have going tired. Said Elias Kiembe, a Senior Journalist TBC,* kwa ufupi anasema kwamba hiyo kamati imechoka hakuna kinachoendelea.

Mhe. Waziri asubuhi anatwambia kwamba serikali inaendelea. Mimi ninaamini kwamba kwa niaba ya Wazanzibari kuwa maneno yake sahihi, sasa kama huyu ofisa anasema uongo maana yake lazima aombe radhi au achukuliwe hatua.

Sasa kama sisi tunataka kupima nani kasema kweli, Wazanzibari wanamuamini Mhe. Mohamed Aboud kwamba ndiye aliyesema kweli, lakini kwenye mtandao hii tayari kutokana na kauli ya ofisa huyu wa TBC kwamba hakuna kikao kinachoendelea na watu wote wamechoka, kama wamechoka maana yake wanakwenda kula posho ambazo hazitusaidii Wazanzibari.

Sasa naomba nipate ufafanuzi jee, ofisa huyu ni mkweli na kama si mkweli ni hatua gani serikali itachukua kwa ajili ya kupata ufafanuzi huu.

Mhe. Spika, jengine ambalo ningemshauri Mhe. Waziri tumekuwa tukiingia katika mikopo mbali mbali kama SMZ, mimi ninashauri mikopo hii hivi sasa ije Baraza la Wawakilishi ili ipate ridhaa ya wananchi ili wananchi wajue nini wamekopa na deni la taifa ni kiasi gani.

Kuliko kukaa maofisa fulani kukopa kwa niaba ya serikali baadae wananchi wakapewa *number* ya madeni kwa kweli hayalipiki. Kwa hivyo ninashauri Mhe. Spika, Mhe. Waziri akubaliane na sisi kwamba kuanzia utaratibu wa mikopo hii ije Barazani na Wawakilishi waridhie kwa niaba ya wananchi kwamba sasa tukope kwa niaba ya Wazanzibari.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri ametushawishi kwamba tumruhusu kwamba sasa tuuze majengo ya serikali kwa ajili ya kujenga ofisi za serikali. Ni wazo zuri ambalo kila mtu halipingi. Mhe. Spika, mimi binafsi nina wasi wasi tutakapokuwa na ruhusa hii kwa serikali kwa kuuza, ile ahadi ya kupata kibali cha wananchi watendaji watauza majengo bila ya idhini yetu. Kwa msingi huo Mhe. Spika, Mhe. Waziri hebu kidogo atueleze hivi karibuni wameuza maghala ya Wizara ya Biashara pale Mtoni na kiwanja, atwambie basi serikali imepata shilingi ngapi ili Wazanzibari wajue.

Mhe. Spika, hata katika ujenzi wa hizo ofisi za serikali kuna tofauti kubwa. Kimsingi sisi tunaangalia *value for money*, Mhe. Waziri anisaidie hebu tumejenga jengo zuri la *ZRB* kwa shilingi 8.4 bilioni lakini tumejenga jengo zuri la Shirika la Bima kwa shilingi 2.9 bilioni. Maana yake jengo moja la *ZRB* ni sawa sawa na majengo matatu ya Bima. Maana yake mukigawa mmoja apate jengo moja, mmoja apate majengo matatu. Mimi hivi nilivyo nimekubali tupate majengo matatu. Sasa atwambie hebu thamani ya jengo lile la *ZRB* la 8.4 bilioni na thamani ya jengo la Bima la 2.9 bilioni kuna uhusiano gain. Kwa msingi huu jengo la *ZRB* limekula thamani kubwa, lina kiwango, hadhi kuliko lile la Bima ambalo ni matatu kwa jengo moja la *ZRB*.

Mhe. Spika, eneo jengine ambalo Mhe. Waziri ametuomba kwamba kuna mpango wa kubadilisha sheria ya mgawanyo wa mapato yanayotokana na *skill development levy*. Mhe. Spika, Mhe. Waziri ametushauri kwamba asilimia 60 ya mapato hayo yatakwenda katika elimu ya juu, ni jambo zuri na asilimia 40 iliyobakia itaenda mafunzo ya amali. Lakini Mhe. Spika, sheria hii imepita toka mwaka 2006 na fedha hizi zimekuwa zikikusanywa, Mhe. Waziri atwambie kwa hivi sasa kuna shilingi ngapi na kwa nini haziendi kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na badala yake wanatuletea sheria tubadilishe bila ya kujua hatma ya fedha zilizokusanywa miaka mingi.

Mhe. Spika, pia kwenye bajeti hii ametuomba kwamba tumpe fedha kwa ajili ya kuendelea mahusiano na sekta binafsi. Mhe. Spika, inasikitisha hapa Zanzibar imeteuliwa kampuni ya *ZAT*. Kampuni hii tumefanya utafiti imeajiri Wazanzibari 160. Kati ya ajira hizo Mhe. Spika, ni watu 3 tu ndio wageni, tena ni maofisa wenye elimu zao maalum lakini wafanyakazi 157 ni Wazanzibari.

Lakini tumeona barua ya serikali kwamba wanakusudia kukatisha mkataba, mkataba ambao *ZAT* na serikali wameingia miaka 30 wanataka kuukatisha njiani. Hasara yake ni nini? Athari yake maana yake ule mkataba ukikatishwa, maana yake watu watakwenda mahakamani. Wakenda mahakamani wakishinda serikali italipa fidia lakini hivyo hivyo wale Wazanzibari walioajiriwa watakosa ajira. Kwa nini serikali iamue kukatisha mkataba kwa kampuni ya kizalendo ambayo imeajiri watu wengi, na zipo taarifa kwamba kuna kampuni inayotaka kupewa jambo ambalo sisi kama Wazanzibari hatuungi mkono hoja hiyo.

Mhe. Spika, ninadhani mkataba wa *ZAT* ungeendelea na wenzetu hawa wakapewa kipaumbele. Mhe. Spika, Mhe. Waziri amekusudia kukusanya mapato kutokana na meli. Mimi ninajiuliza Mhe. Waziri amegeuka wale watu wa Ole. Maana yake watu wa Ole Mhe. Spika, hukodisha embe kwa maua, kwamba maua haya nitapata embe elfu na nitapata shilingi milioni kumi, fedha hizi baadae nitajenga skuli.

Mhe. Spika, Mhe.Waziri anakusudia kutafuta fedha za meli lakini hana meli. Sasa hebu atwambie Mhe. Waziri fedha hizi utazipata wapi au kwa matishali haya mawili yaliopo hapa Unguja ya Bravo na Serengeti. Kwa hivyo mimi ninadhani Mhe. Spika, Mhe. Waziri kama yupo serious na jambo hili, mwanzo angetafuta uwekezaji wa meli na fedha ipo. Tumeuza meli ya MV. Mapinduzi fedha zipo kwenye mfuko wa serikali. Kwa nini kama wana nia ya kutafuta uongezaji huu wa meli na kupata fedha kwa ajili ya kodi, kwa nini wasitoe kipaumbele ununuzi wa meli na hatimae wakaipangia mapato haya. Lakini leo mapato haya Mhe. Spika, akitwambia tumruhusu akusanye fedha, fedha ambazo hana hata kianzio cha meli, sidhani kama hesabu hizi zitakuwa sawa sawa.

Mhe. Spika, mwisho kabisa nikupongeze sana kwa kupata Mwakilishi mpya chini ya Mnadhimu wa serikali wa Baraza la Wawakilishi, nina hakika pale atapata mafunzo mazuri na ataelimika haraka sana. Ahsante sana.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Spika, sina budi kukushukuru na mimi kunipatia nafasi ya kuweza kutoa mchango wangu muhimu kabisa kwa Waziri wa Fedha ambao kitabu chake tumepewa kwa muda mrefu, na tumekitalii vya kutosha, kwa hivyo tunatakiwa tutoe maoni yetu kwenye bajeti yake. Hilo la kwanza.

Lakini la pili ninataka nichukue fursa hii kumshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar kwa uteuzi wa mwenzetu aliyefika leo asubuhi Mhe. Marina Joel Thomas kwamba tutakuwa naye katika Baraza na tunamwambia karibu katika Baraza. Pana kazi nzito ya kufanya, hivyo angalia wenzako wanafanya nini na wewe uingie katika kazi.

Kwa hivyo Mhe. Spika, ninapenda niseme tu kwamba baada ya kupata maelezo ya Mhe. Waziri katika kitabu chake chenye maelezo mengi, lakini ninasema tunazungumzia juu ya suala zima la bajeti, ambayo ni bajeti ni nzuri au bajeti yote ni nzuri iliyopangika vizuri.

Mhe. Spika, tumeona bajeti yake ilivyopangika ingawa katika kupanga hakukosi kasoro. Vile vile tumeona hali ya malengo yake ya uchumi ni yale yanayokwenda sambamba na mpango wa maendeleo. Kwa hivyo tumeona hali gani malengo yake ya uchumi yanavyokwenda sambamba.

Vile vile kwenye bajeti hii itakuwa ni bajeti inayokwenda na fedha za mgao wa wakati. Ile bajeti nzuri ni bajeti inapopangwa mgao, kwa hivyo ule mgao wake uende kwa uzuri. Hapa Mhe. Spika, ninataka nizungumzie pamoja na bajeti iliyopangwa vizuri lakini kunaekwa utaratibu kipindi cha kila miezi mitatu taasisi kupewa mgao. Lakini inasikitisha Mhe. Spika, kuona kwamba pamoja na mpango mzuri uliowekwa inafika wakati mgao huu haufiki kwenye taasisi kwa muda ambao umepangwa. Hii ni kasoro ambayo taasisi au wizara imeshakuwa imejipangia na inahitaji kuona fedha zake kwa mujibu wa malengo yanakuja kwa wakati uliokuwa umepangwa.

Kwa hivyo ningemuuliza Mhe. Waziri kwa nini iwe hivyo wakati fedha ipo tayari imeshawekwa, kwa nini mgao huu uchelewe kufika katika sehemu husika. Mhe. Spika, maendeleo mazuri ya nchi yanategemea ukuaji wa kiuchumi unalenga kukuza hali ya nchi na wananchi wake kwa jumla.

Tunaambiwa hapa nchi inakua vizuri kiuchumi Mhe. Spika, lakini vile vile inatakiwa kama uchumi unakua mzuri inategemea na hali za wananchi nazo zitakuwa nzuri kwa kipato. Lakini mara zote tunasikia uchumi umekua lakini hali ya kipato kwa wananchi imekuwa ni ndogo. Kwa hivyo atakapokuja Mhe. Waziri ninamuomba suala hili kwa nini iwe hivyo kuwa ukuaji umekuwa lakini kipato cha mwananchi kinakuwa kidogo.
Vile vile Mhe. Spika, ningelipenda kumuuliza Mhe. Waziri kwamba jee wananchi wanatarajia nini kwenye bajeti hii? Pili bajeti hii itasaidia kiasi gani kutatua matatizo ya maendeleo ya wananchi, kwa sababu wana matatizo mengi. Jee bajeti hii itawasaidia kiasi gani kutatua matatizo yao.

Pia ningelipenda Mhe. Spika, bajeti hii kwa kiasi gani itasaidia kutuliza kilio cha vijana na umri wa kati kuhusu ajira kama sehemu ya maisha yao. Mhe. Spika, hili suala ni muhimu kuona kwamba vijana wamezagaa ndani ya nchi hii hawana la kufanya, ni wengi kabisa hawana kazi. Ijapokuwa tunasema kazi ni kitu muhimu basi uko wapi utaratibu wa vijana hawa katika kuendeleza maisha yao. Kwa sababu ajira hazipatikani, ajira katika nchi hii zina utata.

Hali halisi ya ajira haijajitokeza kwa vijana wetu na wananchi wote kwa jumla, kwa sababu katika ajira tunaweza tukasema kwamba ajira ambazo baada ya vijana kusoma, kuna ajira ambazo wale ambao wameshamaliza kusoma, na wengine kuna wale ambao hawakusoma wote wanategemea kupata ajira. Ni juu yake yeye Mhe. Waziri kuwapangia vijana hawa ajira zao.

Mhe. Spika, niingie katika sekta ya kilimo. Mimi ninasikitika katika sekta hii ya kilimo, kipindi kilichopita Mhe. Waziri alikijenga sana kilimo lakini katika kipindi hiki cha mwaka huu 2012/13, naona kilimo hakikupata fursa kamili, hakikupewa mchango mkubwa unaostahiki ambao tunasema kilimo kwa nini kisipewe mchango mkubwa sana ambao asilimia 80 au 90 ya wananchi wanategemea kilimo.

Kwa hivyo kama Mhe. Waziri hakuweka mipango na utaratibu mzuri wa kukisaidia kilimo vipi anategemea. Kilimo kinachotegemewa na Wazanzibari si kilimo cha muungano, ni kilimo chetu wenyewe Wazanzibari. Sasa kuna sababu zipi za msingi kuona kwamba kilimo kimepungua kiasi ambacho matararijio yetu hayajafikia mpaka leo.

Kwa ufupi mchango wa wizara ni mdogo sana na tunaamini kwamba kila tukizalisha zaidi ikiwa ni chakula au chochote, kila tukizalisha ndio pale matarajio mazuri ya wananchi wetu na kuona wanaepukana na suala la mfumko wa bei. Kama tutajipanga vizuri katika kilimo basi nina hakika kwamba mfumko wa bei unaweza ukatoweka.

Lakini sasa kutokana na mwelekeo wa kifedha ambao haukuwezesha vizuri bado ninaamini mfumko wa bei utakuwa upo juu. Kama uzalishaji utakuwa ni mdogo, ina maana *exportation* itakuwa hatuna. Hatuwezi kuagizia vitu kutokana Dar es Salaam au nchi nyengine kuja hapa au kutoka hapa kwenda nchi za nje.

Uingizaji na utoaji wa bidhaa. Sasa kama uzalishaji ni mdogo ina maana hatutoweza kusafirisha kitu chochote kupeleka nje ya nchi. Ina maana itabidi tutegemee fedha za ndani tulizonazo, ndio tuagizie vitu. Sasa hizi pesa zinazotolewa kila siku katika kuagizia vitu kutoka nje ya nchi, ikiwa ni nchi jirani au nchi yoyote, hatuoni kwamba tunasababisha mfumko wa bei kuwa juu.

Hii ina maana usafirishaji na uagiziaji wa bidhaa italeta matatizo makubwa sana. Tunachosafirisha ni kidogo na tunachoingiza ndani ya nchi ni kingi sana, fedha nyingi sana zinatumika katika fedha za kigeni. Kwa hivyo kama tutajipanga vizuri kwenye kilimo na wananchi wakafaidika na uzalishaji ukawa mkubwa, ninaamini mfumko wa bei utapotea. Kwa hivyo nimuulize Mhe. Waziri mara hii kwa nini hakupeleka fedha za kutosha katika kilimo.

Mhe. Spika, ukiangalia hata kwenye kilimo kidogo kidogo, vitu vidogo vidogo ambavyo ndani ya Zanzibar tunaweza tukazalisha kama matunda pamoja na nafaka za viungo, ambapo hapa pana hoteli za watalii, kama hizi pilipili, mbogamboga, viungo na vitu kama hivi vinahitajika, na Zanzibar ina uwezo wa kufanya hivyo. Lakini utaona hiki chote tulichonacho hatuwezi kusaidia katika hoteli na inabidi kuagizia nje ya Zanzibar, jambo ambalo sio zuri.
Mhe. Spika, niingie katika suala zima la vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi. Mhe. Spika, mimi katika suala hili ninahisi kwamba halikupewa uzito katika bajeti yetu ya Zanzibar. Halijazungumzwa chochote kuhusu kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi. Jambo ambalo mimi ninasikitika kwamba katika suala la vitambulisho ni sisi wenyewe Wazanzibari tuliomo ndani ya nchi bado suala hili lina vikwazo vikubwa sana, bado hapa vitambulisho vinakwenda zaidi kwa njia ya siasa kuliko tunavyoamini ni haki yake mtu, kama ilivyokuwa pasipoti mtu ni haki yake na kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi ni haki yake.

Lakini kinafanywa Mhe. Spika, na vikwazo vikubwa sana kiasi ambacho watu wengi na vijana wetu wengi bado wameshindwa kupata kwa urahisi kabisa vitambulisho vyao vya Mzanzibari Mkaazi. Kwa hivyo, kinachojitokeza hivi sasa kitambulisho cha Mtanzania kimepewa umuhimu zaidi kuliko kitambulisho cha Mzanzibari. Jee hatuoni hii si nzuri, jambo lako mwenyewe la ndani ya nchi, ni haki yao watu kupata linaekwa kwa nyuma kuliko kitambulisho cha Mtanzania ambapo *process* ya kitambulisho cha Mtanzania ni nzuri na inakwenda vizuri bila ya tatizo, lakini chetu sisi kimekwaza sababu haijulikani ni nini ikawa hivyo.

Mhe. Spika, hivyo hili suala halikupewa kipaumbele, halikuzungumzwa na kwa hivyo tunahisi kwamba hii sio haki. Kwa hivyo tuone kwamba Wilaya pamoja na kuweka vikwazo vyao kuwasaidia na kuwapatia wananchi hivyo vitambulisho. Vitambulisho vimo vingi sana katika maeneo ya Wilaya, lakini bado wananchi kutokana na ugumu wa kimaisha wanashindwa kufika kwenye maeneo yao ya Wilaya wakachukua vitambulisho vyao.

Mimi ninataka nimwambie Mhe. Waziri hatuoni kuwa suala hili ni muhimu kwamba kesho kutwa tunakabiliwa na kura ya maoni. Kura ya maoni ambayo tunahitaji Wazanzibari waliokuwa tayari na vitambulisho, watu wetu hawana vitambulisho, kila tukipiga kura ya maoni utakuta idadi ni ile ile haiongezeki kwa sababu ya kukoseshwa watu haki zao za vitambulisho.

Mhe. Spika, ninaingia katika suala jengine la kodi ya ushuru na ada. Mhe. Spika, hivi sasa kodi ya ushuru na ada zimekuwa nyingi sana. Kuna kodi za simu ambazo hizi zinaingia sana kwa wafanyabiashara sana na watalipwa wenyewe kwa hiyari zao. Lakini kuna suala jengine la ushuru wa mafuta ambapo katika kila lita inaongezwa shilingi hamsini petroli pamoja na dizeli. Jee, tunapoongeza kila siku hatuoni tunaleta matatizo kwa wananchi wetu. Unapopandisha mafuta tujue hiyo itakuwa ni kero ya nchi, kwa sababu unapopandisha mafuta bei na gari itaongezeka, na kila kitu na gharama chungu nzima zitazidi kuongezeka.

Sasa tunaona hatuna namna nyengine ya kutafuta vianzio vya mapato tutegemee kwenye mafuta. Ni mara ngapi nimuulize Mhe. Waziri kwa mwaka anaongeza ushuru wa mafuta? Tunaomba tujue angalau tujue mara ngapi ushuru wa mafuta unapanda na kwa nini unapanda?

Tunasikia kwa wenzetu kila bei zinapoteremka basi Zanzibar bei ya mafuta inakuwa kubwa. Kisiwa chetu watu wake ni wanyonge. Mimi ninafikiri suala hilo angelifikiria zaidi kwa kupandisha ushuru wa mafuta ambao uliokuwa hauna malengo maalum ingawa yeye anategemea kupata bajeti yake.

Halafu hii sheria ya ushuru wa mafuta na nishati, lakini kuna suala zima la leseni ya njia ambapo gari itabidi zipimwe kutokana na uzito wake au ukubwa wa injini. Mimi sijui hata mambo haya yamekwendea vipi hata kufika ndani kwenye uzito wa gari na ukubwa wa injini, hii inahusiana na nini? Mimi ninahisi hapa tujipange vyengine, hili suala halina mwelekeo kwamba tutoe katika leseni ya barabara watozwe hivyo. Zamani walikuwa wanatoa shilingi ishirini na nne elfu, sasa sijui zitakwenda kutokana na uzito pamoja na ukubwa wa injini.

Lakini ninasema hili suala bado utaona ni muhimu sana kwa upande wa wizara, lakini kwa upande wa wananchi hili litakuwa ni tatizo. Halafu kuna suala zima ushuru unaotokana na usafiri wa bahari wa Zanzibar, kwa Unguja na Pemba hivi sasa ni shilingi elfu moja na kwa Tanzania Bara ilikuwa ni shilingi elfu mbili.

Mimi ninasema Mhe. Spika, hapa tuondoshe kabisa kwa kuwasaidia wananchi kwamba kila mwananchi utamtizama, hebu mpangie kodi anazotoa kwa siku ana kodi ngapi mwananchi huyu zinazomlazimu kutoa. Mwananchi anayesafiri kwa Unguja na Pemba, haji kibiashara anakuja kimatembezi tu na anayekwenda Dar es Salaam vile vile.

Mimi nafikiri hapa tutafute mbinu nyengine za kupata vyanzo vya mapato, lakini kuna nyengine kama hizi zinaleta kero kwa wananchi. Mhe. Waziri suala hili liangalie sana au tunahitaji maelezo zaidi utupe. Kwa hivyo, hizo zilikuwa ni ada za bandari kwa Unguja, Pemba na Dar es Salaam.
Halafu kuna suala jengine la ushuru wa stempu ambalo hili tunaliona, zamani ilikuwa inatoza asilimia moja na nusu na sasa hivi inatoza asilimia 3. Hii kwa watu maalum wa wawekezaji au kwa watu wa mahoteli au kwa hao wenye mikopo, hii inakwenda kwa watu maalum.

Mhe. Spika, niendelee na suala jengine ambalo tunaliita *local government reform.* Suala hili Mhe. Spika, kwa kukuambia kweli linatupa *headache*. Suala hili hata kuzungumzwa halikuzungumzwa, halikupewa kipaumbele. Kwa nini sasa hivi hizi serikali za mitaa mpaka leo bado sio chini ya miaka 10 tunazungumza juu ya *local government reform*, hakuna lolote isipokuwa maandishi ya ndani ya makaratasi, hakuna hatua yoyote inayochukuliwa. Yaani tuna *buy time* na wananchi wanajua kwamba hili suala mpaka leo serikali haijasimama sawa sawa. Ni utendaji wa maandishi ya karatasi tu, taarifa za karatasi zinabakia ndani ya ofisi, lakini kwa hatua rasmi hazijawekwa bado.

Huu mimi nasema ni ukandamizaji ni lazima niseme kwenye suala hili la *local government* serikali za mitaa huu ni ukandamizaji wa maendeleo au kuvizwa kwa maendeleo ya wilaya pamoja na vijiji vyake. Kwa nini ifike mpaka leo bado tumeshindwa kuamua kwamba serikali zetu za mitaa, bado utaratibu uliopo hivi sasa ni *centralized system of government*, kutoka juu kwenda chini, kwa nini iwe hivi mpaka leo, tunaogopa nini, kuwa mpaka miaka 10 bado sera hii imeshindwa kutekelezwa hatuna wataalam wa kuifanya hii kazi, kama hatuna wataalam basi tutafute wataalamu tuweke.

Mhe. Spika, mimi ninachojua sasa hivi kinachoendelea ni kwamba *collection* zote zinakwenda kwenye *central government* na baadae ndio inaingia mgao. Kwa nini hatutowi dhamana tukaweka serikali za mitaa, shughuli zote zika malizia katika wilaya zao badala ya kuwa serikali kuu ndio inajihusisha na mambo hayo. Ningemuomba Mhe. Waziri hili suala la *local government* alitilie mkazo na tuone nini hasa itakuwa.

Mhe. Spika, suala jengine nilitaka nizungumzie sekta ya nishati, ambapo mpaka sasa hivi suala hili tumeshawahi kulizungumza mara nyingi suala la sekta ya nishati. Tunahitaji tupate nishati mbadala na mpaka leo nishati mbadala imeshindikana, sijui kwa nini ikashindikana hivi. Mimi ninavyohisi saa nyengine sisi Wazanzibari tunajitia vitanzi wenyewe, kwa sababu wafadhili tunao wa kutusaidia kwa wingi, sidhani kama *proposal* hii tumeipeleka mbele kwamba Wazanzibari wanahitaji wapate umeme mbadala, kwa sababu ziko sababu kwa nini Wazanzibari wanahitaji, hata kama wao vile vile wanazitaja, wanasema kuna njia nyingi za kupata umeme, kwa njia ya upepo, kwa njia ya *solar energy* na kwa njia ya mawimbi ya bahari. Mhe. Spika, kama ikiwa mawimbi ya bahari, upepo na *solar energy*, kwa nini hili suala limeshindikana mpaka leo kutekelezwa, kwa nini imekuwa hivyo.

Sasa Mhe. Spika, hii ni kuikwaza Zanzibar katika masuala mengine, kwa sababu tuangalie hali halisi hivi sasa inavyojitokeza umeme unaendelea kuwa ghali sana kwa wananchi na mimi nathubutu kusema Mhe. Spika, hii ni kauli ambayo na wewe nakupa kwamba wananchi wanaanza kupiga kelele hivi sasa kwamba umeme umepanda, hali ambayo sio ya kawaida, hatujui kwa nini na ifanyiwe utafiti kwa nini umeme umepanda kwa kiasi hiki,

maana ule umeme upande *gradual*. Lakini mtu wa chini hivi sasa hana uwezo wa kununua umeme wa Shs. 3,000 hana haki hiyo, tunamnyima haki na sisi tunasema tunataka watu wote wafaidike na matunda ya Mapinduzi. Mhe. Spika, maskini ana mambo mangapi ya kutwa nzima ya kutumia fedha ile, lakini ikifika usiku kama hana Shs. 5,000/- hawezi kununua umeme. Mhe. Spika, hili suala ni kubwa sana, kuongeza namna hii ni hatari, hebu tujaribuni jamani kuongeza kidogo kidogo, tusiongeze sana, wananchi wanaanza kupiga kelele. Au kama tunataka kufanya hivi basi tufanye moja kwa moja bila ya mwananchi kujua kwamba anatoa kitu.

Mhe. Spika, zamani unanunua shati, shati lile *tax* yake imo ndani ya shati bila wewe kuhisi kwamba *tax* ile umeitoa. Lakini leo kila kitu tunaambiwa wazi na kila mtu anasikia. Mtu ukimwambia mbele ya macho yake anasikia basi anaogopa, anaona hapa inakwenda vipi serikali hii, mbona ushuru umekuwa mwingi sana. Kwa hivyo, ningemwambia Mhe. Waziri hili suala halikupewa kipaumbele.

Mhe. Spika, kwenye hii sekta ya nishati ningependa vile vile Mhe. Waziri aitolee maelezo, kwa nini imechelewa mpaka leo hatukupata maelezo yoyote ya umeme mbadala, kuna sababu zipi za msingi.

Mhe. Spika, nataka nizungumzie suala la michango ya viwanda. Mhe. Spika, nchi hii kwa kweli tumeinukia mambo mengi kuyaona, lakini kila Zanzibar inapotaka kupiga hatua ndio sisi Zanzibar tunaporudi nyuma. Mimi nakumbuka hapo zamani tulikuwa na viwanda kadhaa Zanzibar ambavyo vinahitajika na vina zalisha kila kitu. Mhe. Spika, tulikuwa na Kiwanda cha Sabuni kimekufa, tulikuwa na Kiwanda cha Soda kimekufa, tulikuwa na Kiwanda cha Makumbi na tulikuwa na Kiwanda cha Sukari kimekufa.

Mhe. Spika, mimi kwa mawazo yangu na fikra zangu, kwa makusudi kabisa Zanzibar inafanywa isiendelee na viwanda, inauliwa kwa makusudi kabisa kwamba Zanzibar tusiwe na viwanda. Hatutaki sisi, binadamu yeyote ni maendeleo au sivyo, katika maendeleo makubwa ni viwanda. Hapa wananchi tunafanya ajira nyingi zinapatikana, uzalishaji wa bidhaa unapatikana kwa wingi, kuna sababu zipi za msingi kwamba Zanzibar viwanda vimekufa, kwa nini iwe hivi na sisi tumenyamaza kimya, ina maana tunawapa wenzetu majirani nguvu za kuwa na viwanda, wakati sisi hatuna nguvu za kufanya viwanda, mbona zamani viwanda tulikuwa navyo na vilikuwa vinafanya kazi. Hili ni suala ambalo Mhe. Waziri aje kutupa maelezo, kwa nini viwanda Zanzibar vimekufa na hajatilia nguvu katika bajeti yake katika suala la viwanda Zanzibar kwa nini.

Mhe. Spika, hapa tunasema kuna zogo la watu, kwa sababu hawana kazi, ajira hamna, unaonaje kutakapokuwa na viwanda, uzalishaji utapatikana na bidhaa kadhaa zitapatikana. Kwa hivyo, kazi yake kubwa Mhe. Waziri, nimpe kazi yake, yeye labda ni kushajihisha wawekezaji wa ndani na wawekezaji wa nje ili wawekeze viwanda Zanzibar, ili turudie kama hali yetu ya asili ya zamani. Viwanda vyote vimekufa Zanzibar, kiwanda cha maziwa kiko wapi, kiwanda cha sigara kiko wapi, hii ni aibu jamani, angalia nchi.

Mhe. Spika, zamani katika karne ya 18 katika nchi za Europe zilikuwa zimekufa kimaendeleo, lakini baada ya kutafuta *raw materials* katika nchi za Afrika, unawaona wao sasa wameendelea kwa viwanda. Angalia Japan hivi sasa ni moja katika *industrial country*, inafanya maendeleo ya viwanda vidogo vidogo na viwanda vikubwa. Leo tunafanya ufahari hapa magari yanatoka Japan, Japan inasafirisha magari mengi kwa sababu ya viwanda. Kwa nini hii Zanzibar tunaitupa kwa kiasi hichi, kwa nini hatutaki kijiona na sisi tuna maendeleo, kwa nini na sisi hatutaki tutajike kama ni Wazanzibari ambao tunastahiki kuwa na viwanda vikubwa na viwanda vidogo vidogo ni suala la kuamua tu, Mhe. Waziri *that is a home work for you*.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe bado dakika tano.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Inshaallah. Mhe. Spika, nitamalizia kwa hilo kama ulivyosema, lakini niingie katika suala la mwisho, kwa sababu Mhe. Spika, anaanza kunipa *time* ya kumalizia, lakini nina mengi. Lakini hata hivyo nitamalizia kwenye mabenki ya Zanzibar. Mhe. Spika, hapa Zanzibar sasa hivi kuna mabenki chungu nzima yaliopo hapa Zanzibar, hebu tuulizane mabenki yote hayo ni ya nini na ni kwa ajili ya kitu gani au kwa maslahi gani.

Mhe. Spika, mimi nikichambua kidogo tu maslahi ya benki labda nikuweza uka-*deposit* pesa zako zisije zikaibiwa, lakini katika kuweka hiyo pesa na wewe unaliwa asilimia nyingi sana, kila siku pesa zile zinaliwa, ukikopa pale na kulipa. Tunakopa na tunaweka, lakini hii kukopa na kuweka kweli inasaidia, lakini kiasi gani ambacho wanakopa ni asilimia ngapi wanakatwa. Hii PBZ inakata pesa chungu nzima za mikopo, tuna kopa kweli kwa sababu hatuna namna ni lazima tukope, lakini asilimia ambayo PBZ inatukata sisi ni pesa chungu nzima, kiasi ambacho Mhe. Waziri ningekuomba uangalie Wazanzibari kutokana na umaskini wao. Mikopo ambayo wafanyakazi wako wanakopa PBZ na benki nyengine ni kubwa sana, kiasi ambacho unamfanya yule mtu ashindwe kukopa kwa mara ya pili.

Mhe. Spika, ingawa tunatafuta fedha za kusema mwaka huu nimekusanya kiasi kadhaa zinaingizwa. Mimi naona ni kuingizwa kwa fedha tu, lakini kwa nini watu waje kwa wingi Zanzibar kuweka mabenki, ni lazima kutakuwa kuna kitu kimo ndani watu wanainyonya hii Zanzibar. Mimi kwa kifupi niseme, kama ikiwa tunataka tuwe na mabenki basi tuwe na *share* katika mabenki, hiyo itakuwa ni vizuri zaidi, kwa nini wao hawataki sisi tuwe na *share*. Suala hili Mhe. Waziri nakuachia wewe kwamba sisi tuwe na *shares* katika mabenki, isiwe tu kwa kuweka na kukopa ambapo na sisi tunaumia na wewe mwenyewe unajua, tunakwenda kukopa lakini hali ni mbaya.

Mhe. Spika, la mwisho la kumalizia ni sera ya madeni haipo, hatukuiona sera ya madeni. Mhe. Spika, kwa vile umenipa dakika kidogo za kumalizia maelezo yangu. Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nimejitahidi kutoa angalau yale niliyokuwa nayo. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kuweza kunipa nafasi ya kuweza kuchangia bajeti yetu hii ya serikali. Mhe. Spika, kwa kuanza naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais anayeshughulikia Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo katika nchi yetu, yeye pamoja na wafanyakazi wake katika wizara yake kwa kazi kubwa na nzito ambayo wameifanya ndani ya ofisi yake hadi leo hii tukaweza kuletewa vitabu ambavyo tunavijadili pamoja na kutoa maelezo na michango yetu kwa ujumla.

Mhe. Spika, mimi kwa kuanza ningeanza na kitabu chetu hiki cha mapitio ya hali ya uchumi na utekelezaji wa mpango wa maendeleo Zanzibar. Naomba kunukuu baadhi ya maeneo Mhe. Spika.

Katika ukurasa wa 8 aya ya 3 inasema kwamba:

> "Mwenendo wa hali ya uchumi wa Zanzibar. Pato la taifa, kama inavyoeleweka kuwa pato la taifa ni tathmini ya bidhaa na huduma ambazo zinaundwa na zinabadilishwa kwa fedha, ingawa kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia pamoja na nchi zinazoendelea inaonekana kuzorota. Bado kasi ya ukuaji uchumi wa Zanzibar mwaka 2011 inaonesha matumaini mazuri".

Mhe. Spika, haya maelezo ni mazuri na ni maelezo ambayo yana mwanga mzuri katika kutufanya sisi tuweze kushwarika na kuona kwamba uchumi wetu umeweza kunyanyuka kwa asilimia fulani na kuona kwamba na sisi tumo katika mchakato wa kunyanyua uchumi katika nchi yetu.

Mhe. Spika, mimi mara nyingi sana nikisimama hapa huwa napenda kuuliza swali, kwamba mara nyingi tunaambiwa uchumi unakua katika nchi. Lakini vile vigezo hasa vya kukua kwa uchumi, mimi bado vinanipa mashaka. Mhe. Spika, hali ya wananchi wa Zanzibar kwa kweli bado iko duni sana. Mara nyingi nikisimama naendelea kusisitiza suala hili kwamba uchumi huu unakua vipi mbona hali za maisha bado ni duni sana.

Mhe. Spika, zamani ilikuwa Wazanzibari wana uwezo wa kumiliki angalau milo miwili kwa siku, lakini kwa hivi sasa Mzanzibari yule yule anamiliki mlo mmoja kwa siku nao una mashaka. Sasa ukiambiwa kwamba uchumi unakua, mimi naendelea na utaratibu wangu ule ule wa kila siku wa kutokufahamu namna gani na vigezo gani vinatumika katika kutupa muelekeo na mustakabali wa kutuambia kuwa uchumi unakua.

Mhe. Spika, nilipokaa na baadhi ya wataalamu katika kulizungumzia suala la uchumi hili, wao wakanipa maelekezo kama ambayo nimeyaona katika kitabu hiki kwa sasa ambayo nimeyanukuu hapa. Lakini Mhe. Spika, mimi napatwa na mashaka, na mashaka yangu yanakuja hususan tunapoona.

Kwa mfano, Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alikuwa na nia njema kabisa ya kuwasaidia wananchi katika visiwa vya Pemba kwa mfano, hususan ukitilia maanani suala la kuongeza bei ya karafuu kwa Zanzibar. Lakini Mhe. Spika, kinachonipa mashaka na kinachonitatiza katika kichwa changu mpaka dakika hii ni hawa wana uchumi, ambao huchukua yale mapato yanayopatikana katika nchi kuhakikisha kwamba inakuwa ni vigezo kwao kuweza kuoanisha na kufanya mahesabu yao, ili kuweza kupata pato la taifa linakua kwa namna gani katika nchi husika.

Kwa mfano, Mhe. Spika, fedha ambazo zimeweza kuingia katika visiwa vya wenzetu Pemba kule. Hapa katika maelekezo ambayo tumeyapata, kuna bilioni kama 71 ziliingia Pemba katika mavuno ya karafuu kwa mwaka uliopita. Lakini fedha hizi Mhe. Spika, matarajio yetu ni kwamba tumewasaidia wananchi wetu katika maeneo yanayohusika, hususan katika visiwa vile vya Pemba, lakini pesa hii mbona haionekani Mhe. Spika. Pesa hii Pemba haionekani na hakuna mabadiliko ambayo yametokea katika visiwa vya Pemba kwa pesa ile milioni 71

ambayo imeingia. Lakini watu wa mahesabu wanachukua kuwa ongezeko lile kama ni sehemu ya kuweza kuona kwamba mapato ya nchi yamekua kutokana na wingi ule wa fedha.

Mhe. Spika, mimi nahisi kwamba katika eneo hili tuna tatizo kidogo, na mimi mwenzenu nimeanza kupatwa na wasi wasi kuona kwamba zile fedha zimekwenda wapi, kwa sababu shilingi milioni 71 sio mchezo, tunashindwa kuona hata ongezeko la majengo katika Pemba hatuoni, tunashindwa kuona kama ule utaratibu wa zamani na angalau magari kuongezeka Pemba hatuoni. Lakini baya zaidi tunashindwa kuona hata uwekaji wa zile fedha katika mabenki yetu tuliyonayo kule Pemba. Mimi nimeanza kupatwa na mashaka. Sasa ukiangalia huku wenzetu wanachukua kama ni kigezo kwamba uchumi umekua na wananchi wana uwezo wa kuweza kufanya mambo yao fulani fulani katika kuendeleza maisha yao. Hapa ningeomba kupata ufafanuzi zaidi ni namna gani na vigezo gani hasa vinatumika katika kuhakikisha kwamba nchi yetu uchumi wake unakua na vigezo vyake ni namna fulani na fulani tunachukua kupata uthibitisho huo.

Mhe. Spika, nikiondoka huko, nikija katika hatua nyengine ya deni la taifa. Mhe. Spika, katika bajeti iliyopita ya mwaka 2011/2012. Deni la taifa lilikuwa ni shilingi bilioni 144 na nukta fulani. Lakini katika mwaka huu deni la taifa ni bilioni 209. 9 vile vile. Tukiangalia tunakuta kwamba tuna ongezeko la mkopo la bilioni 65, lakini uchumi wetu umekua Mhe. Spika. Sasa hapa mimi nashindwa kufahamu na ninashindwa kuelewa, vile vyanzo vyetu vya ndani vya mapato tunavidhibiti kiasi gani, hata tukaweza sasa kupata uchumi wa kweli ulioendelevu ndani ya nchi yetu.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atusaidie na atueleweshe namna gani tunachukua mahesabati haya ya kuweza kusema kwamba uchumi wetu umekua, wakati hali za wananchi wetu bado ni duni na ziko chini kabisa.

Mhe. Spika, katika suala la kukua kwa uchumi vile vile kuna eneo ambalo linategemewa sana juu ya suala la uzazi na vifo. Katika bajeti ambayo imesomwa hapa na Mhe. Waziri, naomba kunukuu inaelekeza kwamba ukuaji wa uchumi pekee haitoshi, kinachotakiwa ni kuwa na ukuaji ambao unaoleta manufaa kwa wananchi walio wengi. Ukuaji wa uchumi utafsirike katika maendeleo ya watu kwa upande wetu. Juhudi mbali mbali zinaendelea kuchukuliwa na serikali kupitia utekelezaji wa MKUZA, zikisaidia sana katika kuimarisha kwa hali ya ustawi wa kimaisha kwa wananchi wa Zanzibar. Miongoni mwa manufaa hayo haya yafuatayo.

Kupungua kwa kiwango cha uzazi wa kinamama, wenye umri wa miaka 15 hadi miaka 49, kutoka wastani wa watoto 5.4 mwaka 2004/2005 hadi kufikia watoto 5.1 mwaka 2009/2010. Kupungua kwa vifo vya akinamama na uzazi kutokana na vifo 473 mwaka 2006 hadi 279 mwaka 2009 kwa kila mama laki moja 100,000. Hili ni eneo la kuangaliwa sana Mhe. Spika, katika namna ya kuweza kukuza uchumi wetu.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo ili nisiweze kuchukua muda wako mwingi sana. Nije katika namna ya vipaumbele vya serikali. Mhe. Spika, tukiangalia vipaumbele ambavyo vimetolewa katika serikali kwa mwaka huu wa fedha. Mwaka 2011 na mwaka 2012 hakuna tofauti. Vipaumbele vile vile vilivyochukuliwa mwaka 2011 ndivyo vipaumbele vilivyochukuliwa mwaka 2012, ina maana hakuna hatua tulizokua tumepiga Mhe. Spika, katika mambo yetu, imekuwa kama hadithi ya Mr. Been, anakopi mpaka lile jina la mtu siku ya mtihani.

Mhe. Spika, mimi naanza kupata mashaka na kuona kwamba bajeti yetu hii imekosa ubora wa utafiti na kuweza kujua kitu gani hasa kinatakiwa kupewa kipaumbele na kitu gani kinatakiwa kifuate baada ya kitu fulani. Badala yake kinachoonekana hapa ni kuona kwamba watu wamechukua ile bajeti ya mwaka jana, wakaja wakaiweka katika bajeti ya mwaka huu twende mbele.

Mhe. Spika, ukiangalia katika mambo ambayo yanakera wananchi kwa sana katika visiwa vyetu vya Zanzibar kwa sasa. Nilitarajia suala la maji litapewa kipaumbele nambari moja, lakini kutokana na utaratibu wa mwaka jana bado tumeendelea na utaratibu ule ule wa kuweka kipaumbele cha kwanza ni afya. Sio mbaya, kwa sababu bila ya afya hata huo uwezo wa kuyatafuta maji hatutoupata. Lakini shida kuu ya maji. Mhe. Spika, tulitarajia mwaka jana tulikua na kipaumbele cha afya, kisha mwaka huu tukaanza na maji ili tuweze kuendelea pale ambapo tulikuwa tumepaacha mwaka jana Mhe. Spika. Lakini maji pamoja na kero na adha kubwa iliyokuwepo katika visiwa vya Zanzibar. Mhe. Spika, mimi bado nina wasi wasi mkubwa sana kwa suala la maji, hususan tukitilia maanani Ramadhani imetufikia mbele yetu Mhe. Spika.

Mhe. Spika, bado tuna tatizo la maji katika visiwa na mji wa Zanzibar, lakini kipaumbele hiki bado kipo nambari 4 kama kilivyokua mwaka jana. Sasa naanza kupatwa na mashaka Mhe. Spika. Kweli tumeamua kusaidia katika suala hili au tunaendelea na utaratibu wetu *business as usually.* Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atusaidie katika hilo.

Jengine ambalo nimeliona Mhe. Spika, nilipokuwa nikisikiliza bajeti ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa vile kuna utaratibu wa mawaziri wa fedha, baina ya Zanzibar na Bara kwenda kukaa pamoja na kuzungumza mambo ambayo ni kero kuu kwa wananchi katika nchi husika, nilitarajia na suala la ajira nalo litachukua nafasi. Lakini katika utafiti wangu humu katika vipaumbele suala la ajira ya vijana hamna kabisa humu katika nchi ya Zanzibar. Sasa na hili nalo Mhe. Spika, ni tatizo.

Mhe. Spika, katika Zanzibar yetu tuna vijana wengi sana ambao wanazurura na hawana kazi. Vijana hawa wako baadhi yao wamesoma na wengine wana taaluma ya namna mbali mbali, lakini serikali haijajipanga kwa namna gani inaweza kuwasidia vijana. Isipokuwa Mhe. Waziri alipokuwa akiwasilisha bajeti yake hapa aligusia kwamba kila vijana watano basi kijana mmoja ndiye aliyekuwa hana kazi. Mimi naona utaratibu huo wa mahesabu umekwenda kinyume nyume, vijana wanne hawana kazi labda mmoja atakuwa na kazi.

Mimi nahisi tulitarajia tuweze kupata bajeti ya kuweza kuona ni namna gani serikali imejipanga kuhakikisha kwamba vijana wetu hawa ambao wanazurura majiani wanatafutiwa utaratibu ulio bora wa kuweza kupata kazi za kufanya katika maeneo yetu. Sasa badala yake basi, vijana hawakuwemo katika bajeti na matokeo yake halisi vijana hawa sasa wanarubuniwa, wanachukuliwa kujiingiza katika mambo mbali mbali yasiyofaa, lakini kama haitoshi vijana hawa wanajiingiza katika madawa ya kulevya. Katika bajeti hii vile vile sikuona mikakati ya serikali katika kupambana na madawa ya kulevya, nalo hili ni tatizo sugu, hususan katika majimbo ambayo yapo karibu yetu na ambayo tunayaongoza.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo nije katika namna ya kuangalia vyanzo vya mapato. Bado wataalamu wetu hawa katika Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo hawajajipanga katika kuangalia namna gani ya kuanzisha vyanzo vipya vya mapato katika serikali yetu ya Zanzibar.

Mhe. Spika, vile vile tukija katika eneo la kuzidishiwa baadhi ya kodi ndani ya serikali. Mhe. Spika, mimi niungane na wenzangu ambao wamenitangulia. Mimi nahisi Zanzibar kwa sasa, hatujawa na sababu bado za msingi za kuweza kupandisha baadhi ya kodi ambazo zitaleta kadhia zaidi kwa wananchi. Nasema hivi kwa sababu, nahisi tuna kila sababu ya kuweza kusaidiana na waziri mwenzetu wa fedha katika kuhakikisha kwamba tunaziba mianya inayopoteza kodi na mapato ya serikali. Eneo hili Mhe. Spika, nahisi kwamba tusimwachie Mhe. Waziri peke yake. Eneo hili tunapaswa kulitumikia sote kwa umoja wetu kama viongozi tuliochaguliwa na wananchi ili kuhakikisha kwamba tunafanya kazi ya ziada kuziba mianya ya mapato ili tuone kwamba pato la taifa letu la Zanzibar linanyanyuka zaidi.

Mhe. Spika, sio siri kuna taarifa mbali mbali ambazo zimekwisha kusomwa hapa tumezisikia sote, na kuna maelekezo mbali mbali ya wajumbe waliokwishatangulia tumezisikia sote. Bado kuna matatizo ya ukusanyaji wa mapato katika Zanzibar na hili linatakiwa lifanyiwe kazi maalum na kwa utaratibu maalum. Kama ambavyo tuliweza kufanya operesheni ya kuweza kuzuwia karafuu Pemba ili zisiweze kutoka kimagendo kwenda Kenya, basi na suala la uvujaji wa mapato hatuna budi kujipanga upya, ili tuhakikishe kwamba tunaziba mapato na kuzidisha mapato ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, wakati nilipokuwa nikisoma kwenye taarifa hii niliona kuna ongezeko la watalii Zanzibar. Vile vile jana nilipokuwa nikisikiliza hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar nilimsikia akisema kwamba tunayo malengo ya kuwa na watalii 500,000 katika mwaka 2020.

Mhe. Spika, rai yangu si kuangalia ongezeko la watalii tu ndani ya Zanzibar tukatoka 132,000 na tukenda 175,000 kwa mwaka huu hapana. Kwa kweli nahisi tuangalie *quality* ya watalii wenyewe ambao wanakuja Zanzibar, kwa sababu kuangalia *quantity* tu haitusaidii sisi kama Wazanzibari, kwani mapato mengi ya nchi yanapotea katika sekta hii. Mhe. Spika, mwelekeo wa serikali na tumeshakubali kwamba eneo la pili la kunyanyua mapato ya Zanzibar ni Sekta ya Utalii, lakini mapato haya yanapotea kwa wingi sana.

Mhe. Spika, mimi ni Mjumbe katika Kamati yako ya Fedha, Biashara na Kilimo katika ziara yetu ambayo imemalizika juzi tulikwenda kwenye hoteli moja ya kitalii pande za kaskazini na tumefika kwenye hoteli ile ni mpya, yaani inaendelea kujengwa lakini tayari kuna baadhi ya shughuli zimeshaanza na zinaendelea.

Kwa kweli tumefika katika hoteli ile na tumekuta kuna baadhi ya vyumba ambavyo wanaviita *Sweftecy*, chumba kimoja kinakodishwa kwa usiku mmoja kwa zaidi ya dola 6,000. Sasa Mhe. Spika, sijui katika mchakato wa kodi ambazo tunakusanya kupitia kwenye vyombo vyetu huku kwamba kuna hoteli ambayo angalau inafikia dola 3,000. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, ndio maana tukasema kwamba kuna uvujaji mkubwa wa mapato ya serikali, hivyo ni vyema tujipange vizuri zaidi ili tuhakikishe kwamba mapato ya serikali yanazidi kuimarishwa zaidi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nataka kulichangia kuna sheria nyingi sana katika masuala ya fedha, lakini utekelezaji wa sheria hizi naona bado kwa Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar katika Sekta hii ya Wizara ya Fedha na Uchumi.

Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja hapa atusaidie pamoja na kutuelekeza namna wizara yake ilivyojipanga katika kuzitumia sheria tulizozitunga wenyewe katika Baraza hili kwenye vipindi tofauti, na namna ambavyo hazifanyi kazi katika wizara yake.

Mhe. Spika, hii ni moja kati ya maeneo ambayo kama sheria hizi zitafanya kazi, basi mapato ya nchi yatanyanyuka na wananchi wetu watafaidika pamoja na uchumi utakuwa unakua katika mazingatio sote ambayo tunayategemea, na wala sio katika utaratibu ambao tunao hivi sasa. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu nilijaribu kuangalia katika kitabu hiki cha uwasilishaji wa hotuba hii ambacho kimeletwa na Mhe. Waziri, sikuona utaratibu wa misamaha ya Kodi ya Forodha.

Mhe. Spika, nimejaribu sana kuangalia humu, lakini hakuna maeneo ambayo tunafahamishwa kwamba serikali ilisamehe kiasi gani cha kodi kwa wawekezaji pamoja na watu ambao walikuwa wanapewa kodi mbali mbali katika Wizara ya Fedha ndani ya nchi yetu. Lengo tuweze kujua ni kima gani cha ushuru ambacho kimesamehewa katika mwaka uliopita na matarajio yetu tunataka kufanya nini kwa mwaka unaofuata.

Mhe. Spika, suala jengine ni kuhusu sheria pamoja na utaratibu ambao umepangwa katika mabadiliko wa umiliki wa hoteli. Mhe. Spika, katika eneo hili Mhe. Waziri alipokuja kuwasilisha hapa alisema kwamba kuna utaratibu ambao unatengenezwa kwa ajili ya kupambana na wale ambao wanabadilishana hoteli kiholela na baadae hoteli inaondoka kwa mmiliki mmoja na kwenda kwa mwengine bila ya taratibu za kisheria kufuatwa. Sasa Mhe. Waziri alipokuja hapa alisema kwamba sheria inataka kubadilishwa.

Kwa hivyo, nichukue fursa hii kupitia kwako Mhe. Spika kumuomba Mhe. Waziri kwamba sheria hii ibadilishwe haraka, kwa sababu hawa wenzetu ambao wanaokuja kuwekeza hapa wengi wao ni wajanja mno. Kwa mfano, hoteli moja inatembea katika mikondo sita mpaka saba katika kipindi kile cha *tax holidays*.

Kwa maana hiyo, tunaliomba hili lisichukue muda na kipindi kinachokuja mbele ya Baraza hili tuweze kuona utekelezaji wa suala hili kwa ajili ya kuweza kudhibiti mapato yetu katika nchi yetu ya Zanzibar.

Mhe. Spika, kwenye kile kitabu kikubwa kuhusu muhtasari wa makadirio ya mapato na matumizi yamekuja kwa ujumla sana, yaani kile kitabu kikubwa ambacho tulichokuwa tukikisoma kwenye ukurasa wa 59.

Kwa kweli suala hili hata tulipokuwa kwenye kamati tuliwaambia wenzetu mbona haya mambo yenu mnayoyafanya mnayafanya kwa kujumuisha sana, kwa sababu kuna mambo ambayo mumeyafunga mno, kwani hata tunapotaka kuja kufanya uchambuzi yanakuwa yanatushinda.

Mhe. Spika, suala lile pia likaja kuibuliwa na ndugu yetu Mhe. Ismail Jussa Ladhu hapa, na kwa kweli katika utaratibu kama huu unatunyima fursa ya kutambua uhalisia wa bajeti jinsi ya maidhinisho na matumizi yake katika vipindi vilivyopita na vile vinavyokuja.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo machache kwa sababu wenzangu wameshachangia sana na maeneo mengi wameyazungumzia. Kwa hivyo, niseme mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kikwajuni nachukua fursa hii kuiunga mkono bajeti hii. *(Makofi)*

Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia Hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Mhe. Spika, kwa kuwa watu wengi wameshaanza kuchangia na kuna wengine bado wanakuja ambao wanahitaji wachangie hotuba hii, basi na mimi nitakuwa na mchango wangu mdogo, lakini namuomba Mhe. Waziri aweze kuufahamu.

Nianze mchango wangu katika Sekta ya Kilimo. Mhe. Spika, sekta hii haikupewa kipaumbele kabisa na wala haikupewa uzito wakati sekta hii ni mama kwa wakulima pamoja na wafanyakazi kwa ujumla. Lakini hao Wazanzibari wanayoitegemea na huko nje wanavyosikiliza Baraza lako hili tukufu sijui watasemaje.

Kwanza Wazanzibari walio wengi ni wakulima na wakwezi wa nchi hii. Lakini hadi hii leo ninavyozungumzia bajeti hii nadhani Wazanzibari sijui watasemaje, kwa sababu kwanza wakulima wanahitaji wapatiwe pembejeo kama vile zana za kilimo pamoja na mbolea, ili waweze kulima mazao na yawe juu zaidi.

Sasa naomba nizungumzie kuhusu suala la ukuaji wa uchumi. Mhe. Spika, ni kweli uchumi wa Zanzibar umekua, lakini kwa baadhi ya watu tu na wala haukunufaisha wananchi walio wengi wa Zanzibar hii, kwani uchumi huu haukuweza kutoa ajira kwa wananchi na wala hakuweza kutoa nakisi ya biashara, isipokuwa uchumi huu umenufaisha watu wa juu tu, kwa mfano benki na hoteli. Je, Mhe. Waziri suala hili unatuambia nini wananchi wako? *(Makofi)*

Vile vile nizungumzie kuhusu Vyanzo vya Mapato vya Serikali. Mhe. Spika, tunavyo Vyanzo vingi tu vya Mapato vya Serikali, na wananchi wengi walitegemea kwamba vyanzo hivi vitakuwemo, yaani kutajwa katika bajeti yako hii. Kwa mfano, Mhe. Spika tunayo mafuta kwa kweli hiki ni chanzo kikubwa kwa hapa Zanzibar, ambapo hapo nyuma Mhe. Spika ilikuwa tayari kimeshatajwa na kimeshakuwa ukingoni.

Lakini hivi sasa Mhe. Spika tunaona kimya je, Mhe. Waziri kuna nini? Wananchi wako wanasubiri saula hili kwa hamu zaidi kulisikia. Kwa hivyo, Mhe. Spika namuomba Mhe. Waziri atueleze.

Pamoja na hilo kuna vyanzo mbali mbali kwa mfano ukusanyaji wa kodi kama vile Daladala, *taxi* ziliopo Darajani Mhe. Spika vyanzo hivi vinapelekwa wapi vya mapato. Wakati ukipita Darajani mpaka uzibe pua kutokana na ile harufu ndio upite pale na ule Mji Mkuu wa Zanzibar, hata mwenye daladala pamoja na gari nyengine inabidi waondoke kwanza na kukaa sehemu na kungojea abiria waingie na halafu wao ndio waje waendelee na safari kwa harufu iliopo pale. Je, Mhe. Waziri fedha hizi zinatumika ipasavyo?

Nikiendelea na mchango wangu sasa nizungumzie kuhusu matumizi ya serikali. Mhe. Spika, matumizi ya serikali yanawanufaisha wananchi ikiwa mapato hayakupatikana na ikiwa yatatumika ipasavyo ama ikiwa serikali itasimamia vyanzo vya mapato au kodi, basi serikali inaweza kukusanya mabilioni ya fedha. Lakini Mhe. Spika, hivi vyanzo kwa kweli havitumiki kihalali wala ipasavyo, je Mhe. Waziri anatueleza nini katika suala hili? *(Makofi)*

Mhe. Spika, ahsante sana nakushukuru.

Mhe. Ali Abdalla Ali: Mhe. Spika, ahsante kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima na tunachangia Bajeti yetu ya Serikali.

Pili nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi na mimi niweze kutoa mchango wangu japo mfupi kwa sababu tayari wenzangu wameshazungumzia maeneo mengi sana.

Tatu nimpongeze Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ambaye ni swahibu wangu, wataalamu wake pamoja na watendaji wake wote kwa jitihada kubwa anazofanya na kuweza kuleta bajeti kama hii na sisi tunaichangia leo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, wenzangu wengi wamezungumza juu ya tatizo kubwa la ukuaji wa uchumi. Kwa kweli kitabu kimeeleza kwamba uchumi wetu umekua na wataalamu ndio waliotuandikia hivyo, lakini naomba ningelishauri sisi ambao si wachumi na jamii kubwa ilioko katika mazingira yetu huwa wanashindwa kulifahamu suala hili, na mwenzangu aliyeondoka hivi punde ameligusia.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, wakati atakapokuja kufanya majumuisho, basi atupe japo kwa ufupi kwamba uchumi unakua vipi na pato la mtu mmoja mmoja linaongezeka vipi, ili wale wananchi waweze kujua. Kwa kweli mimi nina mashaka tokea majuzi ninaulizwa kwamba tunasikia uchumi umekua na pato la mtu mmoja mmoja limezidi mbona mimi tokea majuzi nimelala na njaa. *(Kicheko/Makofi)*

Sasa jawabu la haraka nashindwa kulipata, lakini kwa kuwa mtaalamu yupo basi tungeomba atatufafanulia, ili angalau yale maswali mengine yakatupungukia katika mitaa yetu.

Mhe. Spika, nije kwenye suala la Ongezeko la Pato la Taifa pia nalo limeongezeka, lakini hapa ametaja maeneo yaliyoongeza pato hilo. Sasa mimi naomba nieleze maeneo kama mawili pamoja na kutoa ushauri wangu.

Eneo moja amesema Sekta ya Huduma za Jamii na hiyo sio sehemu ambayo ninayotaka kuchangia, lakini sehemu ya biashara hasa Zao la Karafuu na pili baadae nielezee juu ya utalii.

Mhe. Spika, tunashukuru kwamba safari hii serikali imetoa bei kubwa kwa walimaji wa zao la karafuu, na mpango wake serikali imependekeza kuongeza miche ya mikarafuu kwa ajili ya kupanda wananchi, ili baadaye tupate mazao katika zao hili.

Kwa hivyo, tunashukuru na hiyo ni *process* ndefu, kwa sababu mkarafuu tangu kuupanda mpaka kuanza kuzaa si chini ya miaka minne na kwenda mbele. Mhe. Spika, tunashukuru kwamba miche mingi imetolewa na kwa bahati na mimi nimepata miche hamsini na nimeiwekeza katika shamba langu, hivyo nategemea kama sikuwahi mimi basi wanangu wapo watarithi.

Mhe. Spika, naomba kutoa ushauri kwamba bado mikarafuu katika uotaji wake una shida kubwa. Kwa hivyo, ni vyema wataalamu wakapita mashambani kwa ajili ya kuelekeza, ili mkarafuu umee kwa uhakika je tutumie njia gani, kwa sababu kama utaupanda mkarafuu leo masika yakimaliza tu na unyevu umeondoka sijui unyevu ule utaurudisha vipi, wengine wanasema uweke majani makavu yalinde unyevu, lakini ukiweka majani makavu wanaingia mchwa na kuula mkarafuu.

Kutokana na hali hiyo, ni dhahiri kwamba taaluma bado inahitajika katika malengo ya serikali katika kukuza zao la karafuu. Kwa mfano, tumepanda mikarafuu 5,000 na ife 1,000 na 4,000 ije juu, basi inaonesha tumepiga hatua, lakini nina wasi wasi wa kufikia kiwango hicho. Kwa hivyo, nashauri serikali itoe utaalamu zaidi kwa wakulima, ili tuweze kuongeza mapato yetu.

Vile vile limegusiwa suala zima la utalii. Mhe. Spika, tumeambiwa kwamba utalii umeongezeka na tumetajiwa idadi ya kipindi kilichopita na hivi sasa na tunakubali hivyo. Jambo la msingi ambalo ninalotaka kushauri ni kwamba hivi sasa kwanza ujenzi wa mahoteli yameshakuwa mengi sana. Kwa mfano, anakuja mwekezaji kutoka nje anajenga *Bungalow* tatu au nne, yaani inakuwa tunatumia maeneo makubwa lakini kipato ni kidogo.

Sasa naomba kumshauri Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba hivi sasa hao wanaokuja kuwekeza kwa upande wa utalii, basi tutafute wenye mtaji mkubwa na zijengwe hoteli za daraja la kwanza na la pili, kwa sababu hoteli za kawaida zimeshatosheleza maana ukienda Nungwi utaona vile zilivyokaliana ukienda Kiwengwa hali kadhalika.

Kwa maana hiyo, maeneo yaliyobakia ni vyema kujaribu kutafuta wawekezaji ambao wanaweza kujenga hoteli za daraja la kwanza, na ukiweka hoteli ya daraja la kwanza basi na mtalii atakayekuja pale lazima awe daraja la kwanza na ukiweka daraja la pili na mtalii atakuja wa daraja la pili, lakini ukianza *Bungalow* ndio unakuja kwenye vishuka. Sasa kama hili lingesaidiwa basi lingeweza kutuendelezea mapato yetu.

Lakini suala moja ambalo linalonishinda tafsiri na pia linaulizwa sana na Mhe. Waziri amesema katika bajeti yake kwamba hivi sana tunataka kufanya utalii kwa wote.

Mhe. Spika, ukisema utalii kwa wote si wengi wanaofahamu, kwa sababu mimi kwa upande wangu ukisema utalii kwa wote naona labda kama ni mwenye familia, basi siku moja niondoke na familia na kwenda Kizimkazi na kuangalia sehemu ya Mwanamize kwa nini akageuka jiwe pengine pale nitalipa kidogo, *Jozani Park* kwa ajili ya kuangalia Kima Punju na kulipia kidogo na inakuwa si mtu wa kutoka nje tu bali na mimi ndani ya nchi nachangia pato la taifa.

Kwa hivyo, naomba kupata taarifa ya uhakika au sahihi ya kusema kwamba utalii kwa wote umekusudiwa nini, ili na wananchi waweze kujua kama kuna mchango wao waweze kuongeza.

Suala jengine tumeona katika kuvuja mapato sehemu ya *VISA* ingefuatiliwa, kwa sababu utakuta watalii wanaweza kuwa idadi kubwa, lakini *VISA* zikawa chini ya hapo, na *VISA* inatia fedha nyingi katika Mfuko wa Serikali.

Mhe. Spika, kwenye hoteli pia kuna ujanja wa kuwekwa vitabu viwili na kimoja cha uhakika na chengine cha kufanyia biashara wanayoijua wenyewe. Kwa hiyo, ninashauri na hilo likafuatiliwa na ikawa kila hoteli inacho

kitabu chake kimoja tu na hiki cha pili kikatafutiwa utaratibu wa kuondoshwa, kwa ajili ya kupata mapato ya kutosheleza.

Nikiendelea na mchango wangu sasa nizungumzie kuhusu suala la viwanda ambao wenzangu pia wamelizungumzia. Mhe. Spika, nadhani tatizo la viwanda kwetu kufa jambo kubwa sana ni umeme, kwa sababu viwanda vingi vinatumia umeme na gharama ya umeme ni kubwa, ambapo mpaka hivi sasa majumbani mwetu tunapata matatizo hayo. *(Makofi)*

Kwa hivyo, Mhe. Spika naishauri serikali kwanza tungetafuta umeme wetu wenyewe na halafu tukawaita wawekezaji wa viwanda kwa sababu kiwanda kinachukua idadi kubwa ya wafanyakazi. Kwa mfano, Kiwanda cha Sukari cha Mahonda wakati kilipokuwa kikifanya kazi hasa na kuzalisha, basi ilikuwa mashambani tu wanaajiri watu 3,000 mbali kwenye kiwanda chenyewe, madereva pamoja na wataalamu. Kwa maana hiyo, kama tungepata viwanda kama 10 tu ya idadi kama hiyo hapa kwetu nafikiri hakuna zogo la ajira.

Mhe. Spika, naiomba serikali ikatizama umuhimu na wenzetu wanazalisha umeme kwa maji ya bahari na sisi bahari tunayo, pia wanazalisha kwa upepo na upepo tunao, vile vile wanazalisha kwa jua na jua tunalo. Sasa naiomba serikali ikaangalia katika fani hizo, baada ya kupata umeme basi matatizo mengi yataondoka.

Suala jengine ambalo wamelizungumzia wenzangu kuhusu Uvuvi wa Bahari Kuu. Kwa kweli bahari imetuzunguka lakini hivi sasa zinakuja meli za nje na kuchukua angalau leseni ya kuvulia tu. Kwa hivyo, ni vyema kufanya utaratibu na kuja wawekezaji na kuvua Bahari Kuu na kufanya viwanda na kuweza kuuza nje, na sisi kupata tija kwa mara mbili. Mhe. Spika, suala hili naiomba serikali pia ilipe kipaumbele kwa kuweza kuongezea wigo wa mapato yetu.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nataka kulizungumzia ni juu ya kuimarisha mapato. Kuna Mheshimiwa Mjumbe amezungumza hapa kwamba kumebainika kuna magendo ya mafuta, lakini nadhani magendo yako mengi isipokuwa yameonekana mafuta kwa sababu ndiyo yanayotumia fedha nyingi katika nchi yetu, na imeelezwa kwamba mafuta haya wanabadilishana watu baharini baina ya meli na meli sasa imeondoshwa hivyo.

Mhe. Spika, lakini nataka nimwambie Mhe. Waziri kwamba mafuta hayauzwi magendo baharini tu, hivi sasa hata nchi kavu mitaani watu wanauza kwa mageloni na mapipa. Kwa hivyo, nadhani na hili tungeweza kulifuatilia na kuweza kupata kwa sababu haba na haba hujaza kibaba, kwa sababu tayari meli tumeshazibaini na utaratibu umeshawekwa na KMKM ushahidi wamekamata lita zimeandikwa hapa.

Sasa naomba na haya mafuta ya mitaani yangepigwa marufuku, ili mfuko wote ule unaokuja ukapatikana na serikali kwa uhakika. Vile vile akitaka msaada kwa sehemu hizo zinazouzwa mafuta basi mimi leo nikitoka nitampeleka sehemu baada ya nyengine kwa zile ambazo ninazijua, pamoja na wenzangu wengi nadhani wanazijua kwa ajili ya kuondosha hili tatizo la magendo ya mafuta.

Mhe. Spika, niende kwenye ukurasa wa 28 kifungu cha 55 kuhusu maeneo yanayopewa kipaumbele na serikali, imeelezwa katika bajeti hii kwamba sehemu ya mama na watoto, ili kupunguza vifo pamoja na maradhi. Kwa kweli ni jambo zuri, kwa sababu watoto ndio wanaorithi baadae katika harakati mbali mbali kama vile wataalamu, wawakilishi, mawaziri, marais sasa kama hatukumuandaa mtoto baadae urithi utakuwa haupo.

Katika suala naomba kutoa ushauri Mhe. Spika, kwamba pamoja na jitihada hizo lakini bado kuna tatizo kubwa ambalo serikali haijalifanyia utafiti na ninaomba lifanyiwe utafiti, ili kupunguza vifo hivyo. Kwanza hivi sasa kama watakwenda wajawazito 1,000 kwa ajili ya kujifungua, basi ni asilimia 30 tu, ndio watakaojifungua kwa njia ya usalama na waliobakia wote itabidi wafanyiwe *operation*, sasa hilo moja ni tatizo.

Kwa maana hiyo, tutizame kitu gani kinachosababisha kwamba *operation* unakuwa mkubwa zaidi kuliko mtu kuzaa salama mwenyewe, itakapojulikana hili basi itasaidia katika kumkuza huyu mtoto wetu pamoja na mama anayejifungua. Kwa hiyo, hii itasaidia kuondosha vifo.

Sambamba na hilo nimpongeze Mhe. Rais juzi nilisikiliza hotuba yake pamoja na kwenye bajeti kwamba, zile fedha ambazo alizokuwa akilipa mama mjamzito shilingi 40,000/= ameziondosha ijapokuwa itaanza mwezi wa Julai, lakini nashukuru kwamba tatizo hilo lilikuwa na muda mrefu na hivi sasa limepatiwa ufumbuzi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba hilo lifanyiwe utafiti. Lakini kubwa jengine katika sehemu ya afya kwa hivi sasa ambalo linajitokeza ni kuhusu maradhi yasiyoambukiza. Kwa mfano, ukienda hospitali hivi sasa katika wagonjwa wanaokuja basi nusu yake wanayo maradhi yasiyo ambukiza na serikali hapo nyuma ilikuwa inapiga hatua na

kutafuta nyanja nyingi za kuzuia maradhi ya kuambukiza kama vile *TB* na mengineyo, sasa haya ambayo si ya kuambukiza yanaachiwa na kuathiri watu.

Kwa mfano, maradhi ya Kisukari, yaani hivi sasa utaona watu wengi wanakufa kwa Kisukari ni maradhi ya kawaida, lakini la hatari kwa sababu kama hukufuata miko basi huwezi kupona.

Mhe. Spika, jengine kubwa kwa maradhi ya Kisukari hivi sasa, maana yake zamani yalikuwa ni maradhi ya kitajiri, mtu ukipata fedha zako unakula vizuri ndio unapata maradhi haya, lakini hivi sasa mpaka masikini wa mwisho maradhi haya anayapata. Lakini zaidi mpaka mtoto mdogo wa miaka mitatu minne anapata maradhi haya na wala mtoto huwezi kumuwekea miko.

Kwa hivyo, ninaiomba wizara pamoja na serikali kupitia kwako Mhe. Spika kwamba kujitahidi kuona ni tatizo gani ambalo linalosababisha maradhi yasioambukiza yanaongezeka kama vile *BP*, *Cancer*. Sasa tukipata utafiti na kujua kwamba labda vyakula tunavyokula ni vibaya vimepitwa na wakati, basi tungeliweza kwanza kukinga kuliko kutibu, kwani kutibu kunachukuwa gharama kubwa zaidi. Mhe. Spika, naiomba serikali na hili ilifanyie kazi, ili tupate raia wema na waweze kuleta maendeleo katika nchi yao.

Sasa niende kwenye ukurasa wa 38 kifungu cha 76 kuhusu Kuimarisha Wazee wetu katika nchi yetu. Mhe. Spika, kwanza naipongeza serikali kwa jitihada kubwa ya kuweza kuwatunza wazee wetu ambao walitulea sisi na hivi sasa ni lazima tuwalee wao. Kwa kweli kubwa alilolifanya hapa ni kuwaongezea posho kutoka shilingi 15,000/= mpaka 40,000/= tunashukuru ni kitu kizuri.

Lakini hapa ninayo mambo mawili kwa ajili ya ushauri. Suala la mwanzo ni kwamba wazee hawako Sebleni, Welezo na Pemba tu, isipokuwa wapo wazee katika shehia na mitaa mbali mbali. Kwa kweli wazee hao tokea mimi naingia Barazani humu walikuwa wakilipwa shilingi 5,000/= lakini mpaka leo wanayo shilingi 5,000/= hiyo.

Kutokana na hali hiyo, ninaiomba serikali kwa kuwa wazee ni pacha wa Sebleni na kwenye shehia, basi na wao angalau wasogezwe kwenye shilingi 15,000/=. Kwa mfano, mzee anayekaa Mfenesini yeye anachukuwa fedha zake Mwera, hivyo inabidi apande gari mjini na aunganishe Mwera baadaye arudi tena Mjini na kwenda Mfenesini ametumia shilingi 3,000/= na kubakiwa na shilingi 2,000/=, kwa hiyo inakuwa msaada ule haukufika kule ulikokusudiwa na serikali.

Kwa hivyo, kwanza naomba misaada wapelekewe kwenye shehia, pia watoke kwenye shilingi 5,000/= ya mwaka 2000 angalau ifikie shilingi 15,000/=, ili waweze kujikimu.

Mhe. Spika, suala jengine katika mchango ukurasa wa 42 kifungu cha 84 kuhusu Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo. Kwanza niipongeze serikali kupitia wizara kwamba nayo na sisi imetukumbuka kwenye Mfuko huu wa Maendeleo ya Jimbo, kwani kuna miradi mingi ambayo imekwama, lakini hivi sasa tokea kuanza kupata fungu hili basi miradi mingi tumeweza kuikwamua. *(Makofi)*

Vile vile nashukuru kwamba awamu iliyopita tumepata shilingi milioni 10, lakini safari hii wametuongezea shilingi milioni 5 na tunashukuru zaidi. *(Makofi)*

Lakini bado kuna kilio kimoja ambacho kinakwenda sambamba na Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo, basi na hiki tukiondoe ili tuweze kwenda vizuri zaidi. Kwa mfano, wenzetu Waheshimiwa Wabunge tayari wameshajengewa ofisi na Bunge lao la Jamhuri ya Muungano. Kwa hivyo, hivi sasa ukimtaka Mhe. Mbunge unakwenda ofisini na yupo karani wake na kuweza kuzungumza shida zako.

Kwa kweli sisi bado tunazungumzia ukumbini na barazani, kwa sababu wengine wanaweza kuja na wengine wasije kwani vyama ni tofauti, na wanaopata ni chama kimoja. Kutokana na hali hiyo, wengine wanashindwa kuja majumbani kwa sababu ya itikadi ya chama chao, inaweza kuonekana kama ninampigia kampeni na anifuate mimi au vyenginevyo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tunaiomba serikali iweze kutujengea ofisi, ili mwananchi yeyote katika jimbo lile basi asiwe na hofu kwenda kwa kiongozi wake kwa shida mbali mbali.

Sasa nadhani likitatuka na hili tutakwenda vizuri na tunaipongeza serikali mpaka hivi sasa. Mhe. Spika, nafikiri kwa kuwa ni zito na wazee wapo wanasikia, isipokuwa mzee mmoja tu amepungua lakini ataelezwa basi tufanyiwe utaratibu na sisi tupate ofisi, ili tuweze kufanya kazi za jimbo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, mwisho kabisa kwa kuwa mengi yameshazungumzwa naomba nizungumzie kuhusu suala la upandishwaji wa mishahara, bajeti imesema kwamba mshahara wa kima cha chini hautopandishwa na wala si vibaya, lakini tulielezwa kila serikali itakapopata uwezo itakuwa inapandisha.

Lakini mimi bado niiombe serikali kupitia kwako Mhe. Spika kwa kiwango hiki na maisha yetu ya hivi sasa cha shilingi 125,000/= bado hali ni ngumu sana, kwa sababu ukiigawa hii itakuwa mtu unamlipa shilingi 3,600/=, ukipanga milo mitatu kwa siku moja kwa mtu mwenye familia ya watu watatu tu, basi utakuta amekunywa chai tu ya asubuhi na kulikobakia kote ababaishie mwenyewe.

Kutokana na hali hiyo, ndipo utakuta mfanyakazi ameingia kazini saa 2 na ikifika saa 4 hayupo na wala hendi kula urojo, isipokuwa anakwenda kuhangaika vipi ataendeleza familia yake nyumbani, ili ikae sawa.

Mhe. Spika, naiomba serikali kupitia kwa Mhe. Waziri kwamba bado wafanyakazi wa kima cha chini watizamwe kwa hali yoyote, kwani bado hali ni ngumu kuliko maelezo. Kwa kweli hii tukiweza kuweka vizuri wafanyakazi wetu basi utaona pale ofisini mtu haondoki tokea saa 1:30 mpaka 9:30 kwa sababu tayari ameshakinai na anachokipata. Kwa hivyo, naomba hili serikali ilifanyie jitihada, ili tuweze na sisi wafanyakazi wetu hawa watulie kwenye kazi na wajiamini na hizi familia zao zipate kunawiri.

Mhe. Spika, baada ya mchango wangu huo mdogo ambao na mimi niliona nitoe kwenye Bajeti hii ya Serikali. Kwa hivyo, mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Mfenesini, naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja. Nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Spika, kabla ya yote kwanza nimchukue nafasi hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, ambaye ametuwezesha kuwa katika hali ya uzima na hasa kuzungumzia uhai wa nchi yetu.

Mhe. Spika, pia nichukue fursa hii kukupongeza wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii, ili na mimi kuweza kutoa mawili matatu katika bajeti yetu hii.

Mhe. Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa sababu hivi sasa tunaingia kwenye kipindi chetu cha pili cha bajeti, ambapo ninakusudia mwaka wa pili huu wa bajeti. Kwa hivyo, nimpongeze katika miaka miwili hii ambayo kwa kweli kuna baadhi ya mambo ameyatekeleza ipasavyo. Ni wajibu wetu sisi kumsaidia, sisi ndio tunayoisukuma serikali.

Mhe. Spika, nimpongeze Mhe. Rais kwa Bango Kitita. Japo Bango Kitita halipendwi lakini mimi nasema kwa kweli nimpongeze sana kuhusu Bango Kitita. Bango Kitita limesaidia sana utekelezaji wa Wizara. Ingawa fedha zenyewe hazikutimia kwa mipango yao, lakini kwa kweli limesaidia sana Bango Kitita katika wizara mbali mbali kutekeleza wajibu wao.

Lakini pia nimpongeze sana Mhe. Rais kwa kuwaona akina mama wajawazito. Ni suala ambalo lilikuwa si mwanamme si mwanamke ambalo suala hili lilikuwa limetukaa na roho, kila ikifika Wizara ya Afya basi tulikuwa tunalizungumzia. Walikuwa wana shida kubwa sana akina mama kwa ajili ya uzazi na mpangilio salama. Hili nimpongeze sana Mhe. Rais, ameona umuhimu na hasa ilivyokuwa na yeye kapitia mambo ya udaktari.

Mhe. Spika, nimpongeze Mhe. Rais kwa sababu ndio tunasema kwamba Waziri wa Fedha ndio mwenyewe. Nimpongeze kwa muda wa miaka mingi kutokana na mishahara ya wafanyakazi pamoja na kwamba hali yetu, lakini kwa kweli amethubutu kuhakikisha kile kilichopo na wafanyakazi na wao wanafaidika nacho. Katika Nyanja hizo sina budi kumpongeza na namuomba kila mwaka panapohitajika kama fedha itaruhusu basi wafanyakazi waongezwe mishahara. Kwa sababu ni miaka mingi wamesota, nawaombea kwa kweli Mhe. Spika.

Mhe. Spika, nije katika Wizara ya Afya, nayo niipongeze kwa upande mmoja kwa kufanya baadhi ya mabadiliko ya mambo ya maslahi ya madaktari. Lakini bado tumewasahau wale watu wa chini. Sisi tunapokwenda hospitali tunapata yale baadhi ya malalamiko. Naiomba Wizara, namuomba Mhe. Waziri na naiomba Wizara ya Afya ikae ifanye utafiti, hasa wauguzi kwa sababu wao ndio wanaofanya kazi ngumu tena ngumu, hawana wakati. Mtu utamuona toka asubuhi yupo kazini mpaka usiku, hayo nimeyashuhudia kwa macho yangu hivi karibuni. Na wao waangaliwe katika maslahi yao ili kama ni posho kama ni lolote lakini na wao wapewe kipaumbele kwa kazi wanayoifanya ngumu.

Mhe. Spika, nije kwenye kilimo. Kwa kweli na mimi nathubutu kusema kwamba hakijapewa kipaumbele. Tunasema kwamba kilimo ni uti wa mgongo. Bado serikali itafakari na ikae chini ihakikishe kilimo tunakipa

kipaumbele kipi kwanza, ili wakulima wetu wasivunjike moyo. Kwa sababu Mhe. Rais alikuwa na nia safi kabisa, lakini matokeo yake mbegu hazikuwafikia walengwa, mbolea ilitolewa kwa kusaidia wakulima wetu. Lakini mbolea nyingi ilichukuliwa na hivi nyengine ipo madukani inauzwa hiyo mbolea, mie sielewi. Serikali ina jitihada maalum za kuwasaidia wananchi wake lakini kuna wachache wabadhirifu na waroho wa kutaka kuiyumbisha serikali wanafanya mambo ambayo siyo ya kutegemewa. Kwa hivyo naomba Wizara ya Kilimo iwe makini katika suala hili hasa kipaumbele cha mbegu na mbolea.

Mhe. Naibu Spika, alizungumza hapa Mhe. Ali Abdalla nimuunge mkono, hawa mabwana shamba wako wapi, watu wanalima vilimo wanajitahidi lakini hawapati miongozo ya kuweza kuleta tija kile kilimo ambacho wanakilima. Tunaomba sana sasa hivi Wizara ya Kilimo ifunge mkaja ili kuhakikisha kwamba wananchi wao wanapata huduma bora.

Mhe. Spika, wenzangu wamezungumza kuhusu habari ya ukuaji wa uchumi. Na mimi huwa najiuliza ukuaji wa uchumi, lakini nimpongeze Mhe. Waziri na watendaji wake. Kwa sababu bajeti iliyopita kidogo uchumi uliyumbayumba. Bajeti hii kidogo umeongezeka. Lakini mimi nataka nijue aje anieleze Mhe. Waziri na hasa kwa manufaa ya wananchi. Tulipata pataje uchumi wetu ukakuwa kama alivyoeleza kwenye Bajeti yake lakini hasa ni msimamo upi wa serikali ambao unahakikisha kwamba huu uchumi unapokuwa basi na mwananchi na yeye apate kipato, tusizungumze tu. Mhe. Waziri aje atuelimishe umekuwa vipi na tumeongeza vipi. Pamoja na kwamba ameeleza humu lakini bado haijaeleweka. Sisi ndio tunaotunga sheria, sisi ndio tunaelimisha. Lakini na yeye mwenyewe Waziri wa Fedha akitoa ufafanuzi mzuri basi na wananchi watanufaika.

Pia katika ukurasa wa 35 katika ukuaji wa uchumi ameeleza lakini mimi bado sijaelewa. Kwa sababu Wizara ya Uvuvi ilikuwepo zamani lakini mchanganyiko, lakini sasa hivi Wizara ya Uvuvi imetengwa. Katika bajeti yake ameeleza kwamba ukuaji wa uchumi kwenye uvuvi. Mimi nasema bado serikali ikae iipe kipaumbele Wizara hii ya Uvuvi ili tulingane na karafuu, tulingane na utalii, iwe wizara hizi tatu zinashindana kiuchumi. Kwa sababu bahari tunayo, niiombe serikali ikae kwa makini, Mhe. Waziri akae na watu ambao wanaohusika kutafuta mbinu za kuhakikisha tunatokana na umasikini ambao hatuutarajii kwa kisiwa hichi, kisiwa kwa kweli kina manufaa yake.

Mhe. Spika, nije kwenye ajira, sasa sijui nimwambie Mhe. Waziri kwamba hapa amekosea ukurasa wa 38 au sijui ilikuwa kuwaje, kusema kwamba katika vijana 24 lakini mmoja wao hana ajira. Hapa sijaelewa, maana yake kelele tunazozipiga ni kwamba vijana wetu kwa kweli hawana ajira, sasa hapa mimi sijaelewa. Mhe. Waziri uje utufafanulie vizuri. Maana siku ile uliyosoma bajeti yako tulikupigia makofi mwenyewe sijui kama ulifahamu au hukufahamu. Lakini tulikupigia makofi yale si kwa sababu kwamba ni mazuri, makofi yale ni ya kukutanabahisha kwamba hapa labda kuna matatizo, vijana bado hatujafika asilimia kwamba mmoja kati ya 24 kwamba kijana mmoja tu ndiyo hana kazi. Uje utufafanulie vizuri.

Mhe. Spika, jengine mimi naomba Mhe. Waziri kuhusu habari ya petroli, dizeli na mafuta ya taa, kwa nini serikali haifanyi uwezo ikaagiza yenyewe. Nina imani kwamba serikali inaweza kufanya hivyo, ili kuwapunguzia mzigo wananchi wa kisiwa hichi. Petroli inapoagizwa na wengine ikapitia moja kwa moja ikaja huku kwa kweli tunawapa mzigo wananchi. Katika ongezeko moja tumeongezea katika petroli. Naomba ifanye mipango yako ambayo itahakikisha kwamba sasa na sisi petroli inatoka moja kwa moja inafikia Zanzibar, ili kuhakikisha na wananchi wetu na wao na wafanyabiashara ambao unapopandisha petro basi na chakula kipo juu.
Mhe. Spika, bajeti hii huko vyakula vimeshapandishwa, bidhaa mbali mbali zimeshapandishwa. Mimi nitakuomba Mhe. Waziri uje unifafanulie kuhusu uagiziaji wa petroli kwa upande wa Zanzibar ili kuhakikisha kuwapa matumaini wananchi wetu.

Mhe. Spika, nije katika mikataba ya wizara mbali mbali. Naiomba sana serikali kupitia kwa Mhe. Waziri wa Fedha si hivyo tutaomba chombo hiki kila mwenye Kamati yake anaona wizara mbili, tatu, mikataba ipitie kwenye kamati. Kwa sababu tumeona ubadhirifu wa hali ya juu katika mikataba inayofungwa na wizara serikalini. Siingilii mikataba mikubwa nasema mikataba Wizara fulani inataka kufunga mkataba na mtu ambaye tuseme anataka kujenga nyumba, anataka kujenga kituo, anataka kujenga nini. Kwa kweli ina ubadhirifu wa hali ya juu na haifuati taratibu Mhe. Spika. Naomba sana Wizara ya Fedha na wizara nyengine naziomba sana. Wanapofunga mikataba basi wahakikishe mikataba ile inafuata taratibu kusiwe tena na asilimia 10, asilimia 20, asilimia ngapi, hili lote ni tatizo la asilimia ya mtu.

Mhe. Spika, nine katika nyumba za serikali, nitaiomba sana serikali na kwa kila Wizara Mhe. Waziri wa Fedha, huko nyuma tunajua ina nyumba kila wizara imepewa nyumba na serikali. Tutaomba kila wizara utwambie ina nyumba ngapi, wapi na wapi, na nani na nani waliokodishwa au walioazimwa au walionunua. Kwa sababu

tumekuwa na upungufu mkubwa sana wa baadhi ya nyumba ambayo kwa kweli mtu. Mie nitasema kweli bora niseme hasa uwazi nisifiche. Tuseme mfano kama mie Asha Bakari bora nijitolee mfano mwenyewe.

Kama mimi Asha Bakari nina nyumba yangu halafu siwezi nikahodhi nyumba na wala sikai mie naweza nikamuweka mtu yeyote kama jamaa yangu. Kwa kweli tunafanya mambo si mazuri halafu tunalipana kama ni mkurugenzi au nani wakati wizara yake ina nyumba, lakini tunamlipa posho la nyumba, kwa kweli hili sitokuwa pamoja. Nitaomba na nitachangia sana kwa kila wizara ambayo nitapata nafasi ya kuchangia.

Jengine Mhe. Waziri amezungumza habari ya walemavu. Nakuomba sana Mhe. Waziri walemavu hukuwapa kipaumbele cha kutosheleza. Lazima walemavu tuwape kipaumbele kwa sababu na wao ni katika jamii ambayo ina haki sawa na aliyekuwa mtu si mlemavu. Kwa sababu na hawa na wao wanasomeshwa, wanasoma kuna wenye digirii, kuna wenye diploma, kuna wenye PhD, tusiwabague walemavu tuwape haki zao. Nitaomba ombi na sio ombi la leo hilo kwamba ule utaratibu wa mtu ambaye tunaye humu basi ufanikishwe ili aweze kufika juu. Pia tuwe na mkalimani kama sasa hivi kipindi hichi kipo hewani, walemavu na wao wale waliokuwa hawasikii, hawaoni wapate haki na wao wanasikiliza serikali inahitaji nini na inawafanyia nini na nini.

Mhe. Spika, wenzangu waligusia suala la Muungano nitapata dhambi kama sikugusia suala la Muungano. Kwanza lazima tukubali Muungano huko tulipotoka umetulea, kama umetulea basi na sisi tuulee. Kwa maana gani? Lazima tukubali kwamba katika muungano wetu uliodumu kwa muda mrefu una baadhi ya mambo ambayo lazima yarekebishwe. Na kwa sababu kesho kutwa kunakuja Katiba, mimi ningewaomba sana Wazanzibari tungoje tume ya Katiba, tuzungumze yale yetu tuliyokuwa nayo. Kwa sababu tumeweka taratibu na sheria, tufuate zile sheria na taratibu ili ikija tume tuseme tunayoyataka. Si vyema kwa sasa hivi kwa kweli tukaubeza muungano

Mimi sipo pamoja na wale wanaosema kwamba Muungano haukufanya chochote. Si kweli Muungano umefanya chochote. Muungano Mhe. Spika, umetuletea amani na utulivu katika nchi hii. Muungano Mhe. Spika, tokea huko nyuma enzi kabla hakujakuwa na muungano tumefunga udugu, Mmanyema kamuoa Mpemba, Mngazija kaolewa na Mnyamwezi. Tusikatae ukweli ambao upo hai, kama kuna dosari, hatukatai dosari zipo Mhe. Spika.
Mimi nasema kwamba hakuna kitu kama amani. Amani hainunuliwi dukani, hata ukisafiri ukenda wapi huwezi ukaipata. Mie natoa wito kuna mambo ambayo yametokea kati kati hapa. Mie huwa ni muwazi, sasa mtu atakayenitafsiri potelea mbali.

Mhe. Spika, hebu hawa waliotupa madaraka watuamini sisi viongozi wao. Watuamini tumo humu kwa ajili yao. Nawaomba sana kama mtu hana mwakilishi basi atafute pa kwenda, lakini wasituvurugie nchi kwa kisingizio cha muungano. Mimi la ukweli nitalizungumza na la uovu namuachia mwenyewe. Mimi nasema kuna tume imeundwa, tume ambayo itapitia kisiwa cha Zanzibar, Pemba na Unguja, wajikusanye wote waliokuwa hawataki Muungano wazungumze kwa utaratibu na sheria. Hatutaki Muungano kutokana na 1, 2,3,4,5, lakini mtu azuke tu hajui historia ya nchi hii. Tuna wajukuu sisi watuharibie nchi, hakuna kitu kama Amani na Utulivu katika nchi. (*Makofi*)

Mhe. Spika, mimi kwenye suala hili sipo pamoja na mtu yeyote. Kwa sababu inapovurugika amani ndizi yako mwenyewe chini ya mlango huwezi ukaivuna. Lakini tusisahau tunapotoka, tulitoka katika mfarakano mkubwa sana wa nchi na tukajisahau hatukuleta maendeleo ipasavyo na sisi tulipewa madaraka na wananchi. Nawaomba sana Wananchi wa Zanzibar hakuna kitu kama amani. Nawaomba sana wangoje taratibu zilizowekwa na kwa mujibu wa sheria na watutumilie sisi wawakilishi wao, kama wana lolote sisi tunawazungumzia hapa. Ndio kama hivi tunazungumza. Sitaki nitoe history *Wallahi* naapa na *ismu* ya Mwenyezi Mungu tukifanya mchezo hapa rafiki yangu, patakuwa na hatari. Dola sio ya kuchezewa jamani, Dola haichezewi. Mimi jana nilionana na vijana wangu walinisomba tu, nikawaeleza maneno mazuri. Nikawambia kama mtanitepu nitepuni na nasema hayo walikuwa wananisikiliza. Maana niliwambia nitazungumza, nitepuni, nipigeni picha tumekaa pamoja, *I don't care*.

Mhe. Spika, nchi hii imetoka katika mtafaruku mkubwa, tusirudishe tena. Mapinduzi yalikuwa siku hii moja tu. Hayatotokezea tena Mapinduzi hapa. Kwa hivyo naomba sana wananchi wa Zanzibar, tutizame tunakotoka, tutizame tulipo na tutizame tunapokwenda. Siku chache tu tunaleta maendeleo mengi sana, baada ya kukaa pamoja tu Serikali ya Umoja wa Kitaifa, tumeshikana kitu kimoja humjui CUF humjui CCM kwa kuleta maendeleo ya nchi hii. Wasitokee watu wakatumia mwanya wa vyama wakatuvuruga, hatuwaachii.

Mimi nasema Mhe. Spika sitokuwa tayari mimi nikifa leo hata habari sina maana nishakula chumvi Ahamdulillah. Lakini kuna wajukuu wetu ambao kama tukiwa hai wakiwa wameshakuwa wakubwa watakuja

kutusuta. Wewe ulikuwa muheshimiwa katika serikali hii ndiyo ulivyotufanyia hivi. Mimi sitokuwa tayari Mhe. Spika.

Mhe. Spika, nilisema hili niliweke mwisho kwa ajili ya kuleta mustakbali mzuri kwa utawala ambao sasa hivi ni Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Wasituyumbishe tena na nawaomba Waheshimiwa wenzangu Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuwe makini, tusitumiwe na watu ambao hawaitakii mema Serikali ya Zanzibar. (*Makofi*)

Mhe. Spika, tumetoka mbali, tumechinjana bure, tumeuwana bure, hakuna sababu mtoto wa shangazi na mjomba wanahasimiana, sasa tunataka kurudishwa tena kule kule, *no way*. Mimi nimesema hili Mhe. Spika, nilizungumze na nawaomba tena Wazanzibari, watuamini kwamba sisi ni waheshimiwa wao, tunawawakilisha wao sio kwa mambo ya maendeleo tu hata kwa mambo ya usalama wao.

Nitamuomba Mhe. Waziri tujitahidi tusiwe na bajeti tegemezi kila siku. Uwezo tunao wa kuhakikisha bajeti yetu haitegemei muhisani. Tujifunge mkaja pesa tulizozikalia tunyanyuke tuhesabu pesa tulizozikalia, tuna fedha nyingi sana Mhe. Spika, tumezikalia. Kamati teule iliyopita imeonesha njia, hebu tuifanyie kazi ile Kamati teule. Kukua huku hizi pointi ngapi zitakuwa mara tatu zaidi. Kitu muhimu ni uaminifu na uadilifu.

Mhe. Waziri wa Fedha naomba sana baada ya kusema hayo Mhe. Spika, niombe tena wananchi wa Kisiwa hichi cha Zanzibar wasinielewe vibaya. Yote haya nayazungumza kwa nia safi kabisa, kwa sababu sisi ndio tuliyokuwemo kwenye chombo hichi. Sisi ndio wana siasa, tunajua jema tunajua baya. Sisi ndio tulikuwa tunakumbana na Vitakuru vingi tu katika siasa zetu. Kwa hivyo nawaomba tena wananchi, nitarudia tena. Nawaomba tena wananchi inapokuja tume ya Katiba washiriki kikamilifu, watoe maoni yao wananchi waamue. Sio kikundi fulani, wala sio mtu fulani. Baada ya kusema hayo naunga mkono hoja *mia fil mia*. Pale ambapo yale niliyosema nipatiwe ufafanuzi niweze kupatiwa ufafanuzi. Ahsante sana.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Ninakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii, awali ya yote ninamshukuru Mola wangu kwa kuniwezesha kusimama hapa. Mhe. Spika, vile vile nimpongeze Mhe. Waziri kwa bajeti yake ambayo imegusa maeneo mengi.

Mhe. Spika, mimi nitaanzia katika maeneo ya kipau mbele, katika maeneo ya kipau mbele ninaipongeza sana Serikali kwa kuona umuhimu wa afya na kukusudia kuimarisha upatikanaji wa dawa pamoja na vifaa. Mhe. Spika, bila ya afya kwa wananchi maendeleo hayatopatikana. Mhe. Spika, vile vile katika bajeti ya mwaka 2011 na 2012 katika maeneo yaliyopewa kipau mbele ni kuimarisha kilimo kwa kutayarisha miundombinu ya umwagiliaji pamoja na kuweka mitaro.

Mhe. Spika, katika suala la uimarishaji wa kilimo naomba nimuulize Mhe. Waziri katika kipau mbele hiki tumefikia malengo yaliyokusudia, na kama hatukufikia ni kwa sababu gani mwaka huu kilimo hakikupewa kipau mbele wakati ndio tegemeo kwa wananchi. Mhe. Spika, vile vile tukija katika uongezaji wa kodi. Mhe. Spika, wananchi walio wengi walitegemea katika bajeti hii kutakuwa na mpango madhubuti wa utafutaji wa meli ya uhakika na vyombo vya uokozi kati ya Pemba na Unguja. La kusikitisha Mhe. Spika, katika bajeti hii imeonesha kuongeza kodi kwa Unguja na P emba kwa vyombo vile vile visivyokuwa vya uhakika.

Mhe. Spika, katika kuimarisha ajira Mhe. Waziri ametupa takwimu zinazoonesha kuwa kati ya vijana watano mmoja hana ajira. Mhe. Spika, ninamuomba Mhe. Waziri atufahamishe takwimu hizi amezipata wapi. Mhe. Spika, ushauri wangu kwa hili Serikali iwe na kitengo maalum cha kusajili vijana waliokuwa hawana ajira ili pale itakapotatikana vijana kuajiriwa wawe ni rahisi kupatikana na wajulikane uwezo wao. Pia hii itasaidia kutolewa takwimu za uhakika kwa vijana hao.

Mhe. Spika, kwa kumalizia tukitaka kulijengea heshima Baraza letu kwa wananchi na kurejesha imani wananchi hao kwa Baraza hili pamoja na Serikali yetu, ni muhimu sana utekelezaji wa kamati teule uonekane.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naunga mkono hoja. Ahsante.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi angalau kuzungumza machache sana ndani ya bajeti kuu ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa mwaka 2012/2013. Mhe. Spika, kwanza niwapongeze wote wale walianza kuichangia bajeti hii na kwa ujumla yametajwa mazuri na yametajwa pia mapungufu. Napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza sana ndugu yangu Mhe. Raza, lakini nimpongeze zaidi Mhe. Jussa kwa kazi nzuri ile ya kitaalam aliyotanabaisha wenzetu wanapoweka tarakimu zao kwenye vitabu hivi. Kwa sababu kazi hii inaonesha ilimalizika jana leo tutie mkazo

mule mwenye mapungufu, lakini mkazo huu nia ni ile ile ya kuwataka wenzetu waondokane na kasoro zinazojitokeza kila siku.

Mhe. Spika, nianze kwa kuwaomba wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba, chombo hiki ni miongoni mwa mihimili mitatu mikuu ya dola. Chombo hiki ndio chombo kinachowakilisha wananchi wa Zanzibar, hivyo dhamana tuliyonayo tuitambue ni kubwa kwa wenzetu, madaraka waliotupa wametuamini tutakapoyatumia vibaya au kutotia tija kwao hiyo ni dhima itakuwa tumeibeba. Mhe. Spika, kusema hivyo Baraza lako tukufu lilitume kamati teule, kamati teule imerudi na ripoti imesomwa hapa na imechangiwa, wananchi wameyasikia yaliyomo kwenye ripoti. Serikali haijatoa jibu lini itatoa jibu hata kusemwa haikusemwa, matokeo yake wanaleta sasa bajeti yao kulitaka Baraza hili tukufu lipitishe matumizi liidhinishe na makusanyo na mapato hayo watu wakatumie fedha, kama wajumbe wa Baraza lako watakubali hiyo basi wayakubali pia na ya wananchi yatakayokuja dhidi yao. Wananchi wanafatilia na wanatusikia. Serikali haitaki kujibu kuna sababu gani na sisi tuwaidhinishie matumizi yake.

Kwanza, Mhe. Spika, siku zote duniani nchi zote mipango endelevu inayopimika, inayowea kufanyiwa tathmini, inayo Wizara majibu ya mafanikio au kufeli kwao na kwa sababu kwa nini tumefeli ama tumefanikiwa. Hizi ndio bajeti zinazolenga mahitaji ya watu wake. Mhe. Spika, katika masuala yetu ya kupanga kiuchumi tulijipangia *cluster* zilikuwa ni tatu, moja ilikuwa ni ya kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa kipato, humu ndani mkawa na sekta maalum. Ya pili kukawa na huduma na ustawi wa jamii, maji elimu na kadhalika. Tatu utawala bora na umoja wa kitaifa. Tulitarajia bajeti hii ijibu haya kwanza, tumefika wapi katika suala la umaskini, tumefika wapi katika huduma, tumefika wapi katika utawala bora. Swahiba yangu Mhe. Haji Omar Kheri, cluster ya tatu ni yako. Na tokea atawazwe Mhe. Sheni kuwa Rais wa Zanzibar hii hapa mambo yamechafuka. Kuna maeneo dada yangu nitakuwa pamoja nae na kuna maeneo nitahitilifiana nae suala la utawala bora ndani ya awamu ya saba mambo yamechafuka. Waziri mwenye dhamana ninakuomba sana ukakae kitako kupanga safu.

Mhe. Spika, tutasema tukisema uchumi wa Zanzibar kamwe hautanyanyuka hata kiama. Kile kiama kikitufika uchumi bado, kwa sababu ninasema hivi chumi zote duniani zinakuwa na chombo kinachosimamia chumi za nchi hizo, zinazo-*regulated* chumi husika, Zanzibar chombo hicho hatuna wataalam wanalijua hilo, wataalam wetu hilo wanalijua tunalokalia hapa ni lugha tu za kisiasa siasa tunajaza kwenye vitabu ukweli unabaki pale pale. Mhe. Spika, mimi nilikuwa mjumbe kipindi kilichopita kamati ya Fedha na Uchumi. BOT Benki Kuu inasemwa ya Tanzania Benki Kuu wao wanasema hawawezi kusimamia Tume mbili ndani ya nchi moja. Benki Kuu wanasimamia uchumi mmoja, uchumi mmoja ni upi nitasema kwa hili jina linalofurahisha Tanzania Bara. Lakini Tanganyika kwa maana ile benki ya Tanganyika haina sababu ya kutusaidia sisi katika suala la uchumi ndio lugha yao. Tukikubali, tukikataa majibu yapo hata kwa ile sura ya mule ndani. Ile *bank non touch for us*.

Mhe. Spika, nimeichukua hii katiba ya Jamhuri ya Muungano mimi nilikula kiapo hapa kwa kuikubali, nayasema haya si bwabwaja sura 102 (1) ya Katiba ya Muungano inasema kutakuwa na Katiba ya Zanzibar itakayojulikana kama Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo itakuwa na mamlaka katika Zanzibar juu ya mambo yote yasiyokuwa ya Muungano kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii. Kutakuwa na Serikali maana kama kwamba kulitangulia muungano ukishakaa sasa hapo patazaliwa Serikali ya Zanzibar hivi ndivyo lugha. Sasa aliyezaliwa, aliyezaa ndie mwenye mamlaka kwa tafsiri yangu nyembamba. Uliyezaliwa huwezi kuwa na mamlaka aliyekuzaa. (2) bila ya kuathiri masharti yaliyomo katika ibara hii na katika ibara zifuatazo katika sura hii ya katiba hii Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaundwa itatekeleza madaraka yake kwa mujibu wa katiba hii na katiba ya Serikali ya Zanzibar 1984 hii hapa ndipo tulipo.

Sasa Mhe. Spika, wajumbe wenzangu ninalokuombeni hiki kilicho ndani ya madaraka yetu yaliyobaki yote tusijidanganye na ndio maana hizi kelele zote mafuta, nishati, gesi wenzetu wamekamata mpini na sisi tumeshika makali. Kwenye lugha ya kisheria tuliingizwa tukaingia, palipobaki sasa ni kurudisha heshima ya Zanzibar ni sisi wenyewe kushikamana tukawa pamoja tukakubaliana, tukaelewana hayo yanawezekana sio kufarikiana tena. Tunapofanya vyenginevyo hata hiki kilichopo mambo ni haya fedha ipo Mhe. Spika, Zanzibar ya kutuwezesha kuendesha shughuli hizi tulizoambiwa ni zetu lakini sasa kumezuka wimbi jipya wizi uliokithiri, wizi hauna mipaka, kusimamia mambo haya yasiendelee tukasema utawala bora hapa umechachuka. Nidhamu ya matumizi Mhe. Spika, haipo watu wamejijengea tabaka wanaokula nchi na wengine kazi yao kujenga nchi hali hii ni ngumu mno, wanakula bila kujua kwamba kuna wenzao.

Mhe. Spika, nitazungumza eneo moja, Mhe. Spika, suala la umeme si anasa umeme ni maendeleo ya mtu yoyote yule na ni tegemeo kubwa. Umeme leo mpaka kufika ndani ya nyumba, kwanza maskini ya Mungu hawezi kuunga umeme umewekwa masharti, vidokezo mpaka ushatushinda. Waheshimiwa wako hivi sasa wamo humo

ndio wameweza kulipa umeme. Subiri baada ya 2015 mwenye nyumba mbili atawasha moja koroboi pengine siku ya zamu ndio atawasha umeme ndio ukweli wenyewe huo.

Mhe. Spika, neno linaitwa *service charge* unainunua nguzo, unanunua waya, vikombe vyake, visahani, unalipa tena kuja kuungiwa service charges ipi hapa ya weye ulipishwe mwezi hadi mwezi inatokea wapi? Wao kufanya kazi zao ndio *service charge* ulipe weye mteja. Nimesema mwanzo kuna wananchi na wanaojenga nchi. Serikali ya Mapinduzi Zanzibar chini ya uongozi wa Mhe. Ali Mohammed Shein nakuombeni sana Mawaziri msaidieni Serikali sasa wananchi wanailalamikia wanaichukia hakuna usimamizi. Huyu anakatiwa umeme Mhe. Spika, kwa sababu miezi miwili hajaulipa maskini ya Mungu Kidoti, kuna bosi tajiri yeye anadaiwa shilingi milioni ishirini moja umeme haukatwi. Barua inatolewa ndani ya taasisi ya Serikali kuwa wacha huyo, sasa hatuwezi kuwa namna hiyo, hoteli miaka 15 hailipi umeme hata gamba kwamba yeye ni mteja wa ZECO halipo, faili halipo tunamuonea huyu wenzetu yanayofanywa ni mabaya mno, tutakuwa wapi na uchumi imara katika sura hii.

Mhe. Spika, ninatonoa tonoa tu kuna balaa, ninakuombeni sana waheshimiwa wajumbe chombo hiki kina dhamana ya watu, tumepiga kelele hapa Baraza lililopita, tume teule tumepiga makelele viwanja vinauzwa ovyo, basi mkishauza hii pesa ileteni isaidie, hapakuletwa fedha yamekwenda kuuzwa na ma-*godown* sasa wanatwambia na hapa tunauza. Lakini Serikali ipo, vyombo husika vipo, wawakilishi wa wananchi wapo jamani hii tena tuogopeni gharka ya Mwenyezi Mungu itakuja kuwa balaa hapa. Mungu kwenye dhulma hakubali hilo tulijuweni. Na hivyo Mhe. Spika wetu kipenzi tunayekupenda, kikija kimbunga ni cha wote Mungu atakwenda kupangua huko mbele ya safari. Kwa hivyo ninakuombeni sana waheshimiwa wajumbe wa Baraza hili tusikubali kuipa nafasi Serikali, kama haitaki kuchukua hatua kwa walionekana hawa ndio Baraza likatae, kwanza tuikatae bajeti. Si kama tunamgomea Waziri hata kidogo. Tunaitaka Serikali ione hili jasho la wananchi wake huku kwani kuna nini watu wako wengi na hapa Mhe. Spika, ni pale tunaposema mara nyingi si kila uwanja mumwachie Rais kuteua matokeo yake haya maovu haya nusu na robo ni wale wanaoteuliwa na Rais. Lakini ingekuwa nafasi hizi zinatangazwa watu wanaomba kazi ingekuwa nyembamba mno kaa upande hufai, wateule wa Rais ni mwenyewe Rais lakini leo tunamwambia Mhe. Rais kwa heshima na taadhima sisi si wasemaji wa Rais lakini nyumba mwananchi hoi bin taaban Zanzibar watu taaban.

Sasa Mhe. Spika, tunapoyaacha haya tukenda kuwabebesha mzigo wananchi tunaongeza kodi ya mafuta, Serikali yenyewe inalia kelele kwamba mafuta yakiongezeka duniani ni kizaizai. Sisi tunawaongezea wananchi hapa kodi gari, maleseni mpaka sasa kupita bandarini tunaongeza tena ada sahiba yangu mpenzi Waziri wa Fedha wenzio ungewaambia basi kwenye visiwa bandari *is a political road.* Ndio maana wakoloni walipanga na usafiri wa meli japo kama mna watu watatu meli iende Pemba na kama mna watu wawili meli ije Unguja haibadilishi ratiba. Maisha ya watu wa visiwa ni baharini. Unapowaongezea kodi maana yake unawakomoa wapite wapi na nundu zao, masheli sheli, kuku, maembe balaa zote sokoni Darajani Unguja ndio twende. Yamesemwa karafuu zote na mapesa yote sasa hivi kukavu hakuna kitu kwa nini? Maana yake pesa zote za wapemba, karafuu zishaletwa kwa wasambaa kununua maharage haziko tunapeleka pesa tu sisi hatuchukui pesa kutoka kwao. Ndio mfumo uliojengwa wa uchumi ndio nikasema haukui hata kiama mpaka mfumo ubadilike, huu ndio ukweli. Wataalam kule juu na wale wa muungano wanalijua hilo.

Mhe. Spika, ajira sahiba amesema jamani wamesahau wenzetu ama ni kibinaadam ajira iko wapi? Mhe. Spika, tulisema GSO haifanyi kazi iliyotajwa na kama inafanya kazi iliyotajwa yasingekutwa madudu unamkuta mtu kaajiriwa ana mavyeti nimesema hapo andika nimeondoka saa kumi na mbili na nusu nimefika kazini lakini nimeondoka nimekwenda kunywa chai, hajui analia lakini yuko katika ofisi na meza ya Serikali. Ni ujomba, ushangazi na mengine mengine na rushwa tele utawala bora bado na ndio nikasema *cluster* zile tatu hazijafanyiwa *evaluation* tukajua *suspection failure and positive agence* hakuna kitu.

Mhe. Spika, tunataka serikali kwa heshima zote na mapenzi makubwa chini ya kiongozi mkuu Rais Ali Mohammed Shein na wasaidizi wake wakuu watujibu hoja za kamati teule kwanza. Lakini kitabu cha bajeti Mhe. Spika, kina maneno jazba tumelia, tumenyamaza sasa tunaongeza ada, si mshanyamaza kulia sasa mtalipa ada zaidi mupite hapa au msipite ndio tafsiri ijavyo. Tokea juzi baada kusikia bajeti, Mhe. Spika, kweli Serikali hata sentensi moja kwa mpango gani angalau wananchi matumaini wa usafiri imara wa uhakika, hawa watu wa visiwa maisha yamo ndani ya mwambao wa bahari hii hawana pengine. Haiwezekani hivi jamani ni wajibu si ombi, kama kujuta yaliyotokea ijute badala yake tunapandishwa mule mule kwenye madude mabovu *commit* ya meli zile inatolewa na Serikali hii hii. Jamani wataelewa nini watu mshawachoka haiwezekani maana tutauliza mengi, basi tena linalovusha si dau Mhe. Spika, Serikali ina kila dhima na dunia inatushangaa watu wale jamani tumepiga kelele kwenye bajeti iliyopita hapa, miezi miwili mbele linatokea lilitokea.

Mhe. Spika, hadi hii leo wanaendelea kufa kwa kisa kile. Kijana ambaye mke wake alikuwemo kwenye ile meli anakwenda kwao Pemba kujifungua, kupewa taarifa ile alipoteza akili, juzi kajitundika hapa leo ya tano. Sasa suala tumelia tumenyamaza hatujanyamaza wala hatunyamazi. Tutashukuru kwa sababu Mungu mwenyewe sasa mnatwambia na mkono wa mtu mbona hamtusikilizi. Hivi jamani ni kweli juu ya yote hii sisi tunashindwa kwenda kuwaambia hao wahisani wachangiaji wa maendeleo kadhia yetu ni hii hilo hatuliwezi. Mhe. Spika, na mimi nitakuwa mgumu mimi Asaa Mwakilishi wa Wete bajeti hii ikifika kupitishwa nitakuomba unipe ruhusa nitoke nje kama hakujatokea mawili. Serikali itaje mpango gani wa uhakika tutakuwa na chombo cha kusafiria moja la pili ripoti ….

Mhe. Spika: Waheshimiwa wajumbe, kimsingi muda umekwisha na uliobaki pia haumtoshi huyo mwengine, sasa basi amalize maneno mawili matatu.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Ninakushukuru nina mapenzi makubwa na Serikali yangu, nina mapenzi makubwa na uongozi wa dokta Shein lakini pia namuonea huruma sana Mhe. Rais, dhima yake ni nzito leo na kesho. Kuna wenzie hawana nia njema hawamsaidii kama kwa makusudi ama wana yao, wanapokaa nae na mabango kitita sijui yanaitwaje mambo mazuri, utekelezaji wa hapo ni kinyume nyume, ya mdomoni machache kuliko yaliyo kifuani mwao. Lakini mambo ni magumu kwa nini hali ya maisha ya watu wetu haimithiliki sasa ni mbaya kuliko maelezo kila mtu alipo hataki kuwajibika ipasavyo. Rais yupo pale ni mmoja waliobaki wasaidie, lakini Mhe. Spika, niseme nina mawili ya mwisho. Jamani kila mmoja atabeba mzigo wake wala isije kichwani kwamba wanamlani Rais unajilani mwenyewe, wala huwakomoi wazanzibari unajikomoa mwenyewe. Lakini kila mmoja afahamu kwamba ana wajibu wa kuwatumikia wenzake kwanza halafu yafuata mengine.

Mhe. Spika, nistahamilie la mwisho. Mhe. Spika, kwa nafasi hii naomba niitumie kwa kuwaambiawazanzibari wanaonisikia kwamba katika mazingira tuliyonayo, nawaomba Tume ya Kusikiliza Maoni iliyokwisha undwa na Mhe. Rais Dokta Jakaya Mrisho Kikwete iko karibu kufika Zanzibar nawaomba wazanzibari nafasi hii ni muhimu sana kupita yote. *Opportunity never comes twice*. Tukisimama kwa umoja wetu na kwa uzanzibari wetu lazima tulitakalo liwe sisemi tunataka nini tutakaloiambia hiyo Tume mimi sijui. Lakini tukigawika ni mtihani wala tusije kumlaumu mtu, tuitumie nafasi iliyopo ni uhuru, uwazi tulizana uje uzungumze na Tume. Matokeo ya Tume chombo hiki cha Baraza ulilotuweka sisi mheshimiwa mwananchi ndio tutalinda hicho ulichokizungumza, ahadi tunaibeba wengine tutakufa na maelezo yenu mtakayoyaeleza tuhakikishe kwamba yaliyotakiwa na wazanzibari kwa faida yao na hatma ya maisha yao ni haya ni lazima tutayasimamia kwa nguvu zetu zote.

Mhe. Spika, mengine yote hayatotusaidia yataharibu mustakbali wa Taifa hili la Zanzibar. Hayo tunayoyatarajia hayaji kwa pupa wala vishindo kama kuna makosa yaliyotendeka yameshatendeka, lilobaki ni kutengeneza. Watengenezaji ni wazanzibari waliopo sasa lakini lazima kwa heshima zote tuwe wapole, wataratibu lakini wenye kuelewa tunalolifanya.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, mimi nakushukuru kwanza kwa kunivumilia, lakini nikuombe sana kwa salamu nilizopewa nitasikitika kama majibu mawili ya maeneo niliyoyataja makubwa, ikiwa Serikali hawakutaka kuyataja kama wananchi wanavyoyataka. Mhe. Spika, nikuombe tena uniruhusu nitoke nje bajeti ipite ili wananchi walionichagua niwape heshima waliyonipa.

Mhe. Spika: Mheshimiwa tunakushukuru kwa mchango wako huo. Waheshimiwa wajumbe kabla sijaahirisha kikao kuna tangazo moja dogo tu ambalo tuliwahi kuambizana kwenye *briefing* zetu na ambalo linaonekana bado halijatekelezeka vizuri. Shirika la Umeme walituomba tuwapelekee *account* zetu za kulipia umeme ambazo waheshimiwa tutakuwa tunazijua kwa nyumba zetu zote. Kwa hivyo tunahimizwa kwamba tufanye hivyo ili waweze kuchukua hatua za kusaidia masuala yetu.

Baada ya hayo waheshimiwa wajumbe wachangiaji kwa jioni ambao watatangulia ni pamoja na Mhe. Saleh Nassor Juma, Mhe. Subeit Khamis Faki, Mhe. Ashura Shariff Ali, Mhe. Farida, Mhe. Bikame na wengine wengi. Kwa hivyo niwaombe wafike mapema ili mjadala wende kwa mtiririko unaostahili.

Baada ya hayo waheshimiwa wajumbe naahirisha kikao hadi saa kumi na moja jioni.

(Saa 7.00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11:00 Jioni Baraza Lilirudia)

(Majadiliano Yanaendelea)

Mhe. Ashura Sharif Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, awali ya yote sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu (SW) aliyetujaalia uhai, uzima tukawepo hapa kutekeleza majukumu yetu kwa maslahi ya taifa letu. Pia nikushukuru na wewe kwa kunipatia na mimi nafasi hii ya kutoa mchango wangu.

Mhe. Naibu Spika, nianze na kumpongeza Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri wa hotuba hii. Aliitoa kwa ufasaha sana na kwa kweli alikwenda kwa kasi sana na kuondoka kwa muda ambao ulikuwa mzuri.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli wananchi wakati wakisikia kipindi cha bajeti hujenga matumaini makubwa. Wazanzibari wote tarehe 13/06/2012 walikuwa kwenye vyombo vya habari kutega ili kuweza kusikia ni kitu gani kitakachozungumzwa kuhusu mustakbala wa mwaka wa fedha wa 2012/2013.
Mhe. Naibu Spika, baada ya hilo wananchi walitarajia kuona kwamba kuna mambo yatawagusa katika njia moja au nyengine. Hayo ndiyo yaliyokuwa matumaini makubwa ya wananchi wengi wanaotusikiliza.

Mhe. Naibu Spika, naomba baada ya utangulizi wangu huo niende sasa katika mchango wangu. Katika ukurasa wa 7 kifungu nam. 16 kinachosema uchumi wa Zanzibar. Hapa Waziri alitueleza ya kwamba uchumi wa Zanzibar umekuwa kwa asilimia 6.8. Matumaini makubwa yalijengeka mno, 6.8 ya ukuaji wa uchumi ni hatua kubwa inayopendeza mno ndani ya masikio ya wananchi. Baada ya kuangalia nikawa nina maswali ya kujiuliza. Katika kuendelea kusoma bajeti hiyo niliona kipengele chengine kinachosema pamoja na yote hayo lakini pato la mwananchi halikuwa lenye kuongezeka au haukuondoka umasikini wa kipato. Hapo nikapigwa na butwaa tena. Je, yale matumaini ya Wazanzibari yanaelekea wapi, nikakwazwa sana.

Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja katika majumuisho nami anielimishe jamii ya Wazanzibari wananchi wanaotutegemea miongoni mwa vijana wanawake watafaidika vipi na uchumi huu katika kukua kwake.
Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri alieleza katika bajeti yake hiyo ya kwamba kuna mambo ambayo yalichangia kukua kwa uchumi, moja wapo ni usafirishaji wa zao la karafuu. Akaendelea kusema Hoteli na uchimbaji wa mawe na mchanga. Hapo mimi nilikwazwa mno nikikubali ya kwamba hivi sasa zao la karafuu ni kweli kabisa limetupatia fedha nyingi za kutosha na wananchi wetu walizipata hizo. Lakini serikali haioni kwamba umefika wakati sasa usiwe wa kutegemea kwamba tunazalisha zao hili la karafuu na kuliuza kama lilivyo, badala yake ni kuamua kuingia katika mambo ya viwanda na kulisarifu ili na sisi tukaongeza tija na pia kuongeza ajira kwa wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, kagusa tena katika utalii nami nikiwa najiuliza Sekta hii ya Utalii ambayo bajeti iliyopita tuliambiwa inaingiza pato la taifa kwa asilimia 80. Napenda Mhe. Waziri atakapofika hapa anielimishe na mimi nielewe huu utalii unamnufaisha vipi mwananchi wa kawaida. Imani yangu kwamba katika utalii wanaonufaika ni wachache ni wageni. Nayasema hayo nikiwa na ushahidi wa kutosha kwamba nafasi chache za ajira zinazopatikana tena kwa tabu mno, kwa kweli hazijafikiwa kiwango cha kusema ya kwamba Wazanzibari wananufaika au wananchi wananufaika na utalii huo.

Utalii unaingia katika nyanja na mambo tofauti hivi niulize Mhe. Waziri wa Uchumi, Mipango atuambie ni Wazanzibari wangapi tumejielekeza nini na utalii wa kuona kwamba tunajifunza kuzalisha na kuweza kuwapatia yale mahitaji wanayohitaji wale wawekezaji wetu katika hoteli zao na wakafaidika Wazanzibari. Tujiulize kuna mpango gani madhubuti unaofanya wakulima wa Zanzibari waweze kulima mboga mboga na kuzifikisha katika sehemu za utalii na kufaidika na utalii huo. Ni wangapi wanaoweza kuvua katika uvuvi wetu. Tukijitizama sisi ni visiwa wanaweza kuvua na vitoweo hivyo vikaweza kufikishwa katika hoteli za utalii na mwananchi ukamgusa utalii huo. Hapa napata mashaka ya kwamba ni kweli kabisa hili ni pato la taifa lakini haliwanufaishi Wazanzibari ambao ndio wazalendo wa nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea tena anasema Mhe. Waziri ya kwamba uchimbaji wa mawe na mchanga nao umekuwa pato la taifa. Hii ni ajabu, hivi wachumi kwa fikira zao na mipango yao wanasema kwamba uchimbaji wa nishati ya mchanga na mawe ni pato la taifa. Tumejiuliza ya kwamba kijiografia ya kwamba nchi yetu ni kisiwa. Nashangaa na napigwa na butwaa mno. Nchi ndogo ya kisiwa kama hii kuweza kuona kwamba mchanga, mawe, inasema ni nishati inayoingiza pato la taifa, jamani tunakwenda wapi? Wachumi wanasemaje, wachumi wetu hawa.

Mhe. Waziri haya ni mambo ya hatari sana katika kuhifadhi mazingira nimeona katika kitabu chako umeeleza humu, uhifadhi wa mazingira. Ni mazingira gani yatakayohifadhika Mhe. Waziri wakati uchumi wako

unatokana na uchimbaji wa mahandaki ya mchanga pamoja na mawe. Inaelekea ya kwamba wachumi wetu sasa hawajaona na wala hawajaelekeza nguvu zao katika mambo muhimu ya msingi ambayo Wazanzibari na taifa litawapatia pato, serikali yetu na kuweza kuendeleza taifa letu au kwa maslahi ya wananchi wa nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, uchimbaji wa mchanga ni uchafuzi wa mazingira. Ni hatari sisi ni watu wa kisiwa jamani hili nasema kwamba kuitwa pato la taifa ni aibu kwa watu kama sisi tuliokuwepo katika kisiwa. Wenzetu walioendelea wanaohitaji kujenga basi chumi zao zilizokuwa zimeendelea huko zimeinuka wanatafuta *resource* hizi katika nchi nyengine na kuleta katika nchi yao kwa ajili ya kufanikisha mazoezi ya makaazi. Sisi tuna nini watu wa kisiwa tunachimba ardhi zetu na kusema ni pato la taifa.

Mhe. Naibu Spika, ninaendelea katika ukurasa wa 8 kuimarika kwa sekta ya kiwanda nayo pia ilitajwa. Mimi nataka kumwambia Mhe. Waziri nataka nivielewe viwanda hivyo ni vipi. Maana kwa ufahamu wangu kwa kihistoria kabisa nilikuwa nafahamu viwanda vikubwa ambavyo sasa havionekani tena na kiwanda ambacho kilikuwa kimebaki ni kiwanda cha sukari pekee ambacho amepewa muwekezaji na hatima yake hatuielewi.
Mhe. Naibu Spika, naomba atakapokuja hapa Mhe. Waziri na hili nalo anielekeze na anifahamishe, hii hatima ya kiwanda cha sukari ambacho tulitarajia tumempa muwekezaji na tukatarajia ili vijana wetu, ndugu zetu, Wazanzibari ambao wana shida ya ajira walitarajia sana watu wa Kaskazini wangeliajiriwa katika kiwanda hichi cha sukari. Kulikoni nacho kimeingia mitini?

Mhe. Waziri si hilo tu, mabonde ambayo mmempa muwekezaji kwa ajili ya kiwanda hicho cha sukari yameleta utata mkubwa mno, wananchi wanashindwa kuyatumia kwa kuweza kuzalisha chakula ambapo kilimo ndio uti wa mgongo wa taifa hili. Hebu Mhe. Waziri niambie wananchi wambao walikuwa wanatumia mahekta kwa mahekta ambazo amepewa muwekezaji hazina kazi na zimesababisha ugomvi mkubwa na hatimaye kesi nyengine zipo Mahakamani. Hetu tuambie Mhe. Waziri kulikoni kuhusu hili?

Wananchi walitarajia katika hotuba yako ya bajeti 2012/2013 ya kwamba utalizungumzia hili na kuonesha hasa dhamira ya serikali nini itawafanyia Wazanzibari wananchi wazalendo ambao hali zao ni duni mno kimaisha.
Mhe. Naibu Spika, niende katika ukurasa wa 11, kifungu nam. 22 maendeleo ya kiuchumi. Naigusia katika namba (VI) inasema kwamba “imeimarika sekta ya elimu katika uwiano wa elimu na wanafunzi kwa sasa imefikia mwalimu mmoja kwa wanafunzi 27”. Huku ni kutudanganya ni nani asiyeelewa ya kwamba watoto wamelundikana mno katika madarasa, na siku zote tunapiga kelele ya kwamba madarasa yana watoto wengi kiasi ya kwamba walimu wanashindwa kuwasomesha watoto vizuri.

Mhe. Waziri, hebu aniambie atakapokuja hapa, hili limebuniwa, hili amelichukua katika msingi gani. Mimi nimeshangazwa mno kuona hili tena amelilinganisha. Amesema kwamba mwaka 2010 ilikuwa ni watoto 28 kwa mwalimu mmoja. Jamani Mhe. Naibu Spika hii ni ajabu ya kimataifa, hakuna Mzanzibari yeyote asiyeelewa shida iliyotukwaza katika shughuli za kielimu, kimadarasa pamoja na walimu wenyewe ni nani asiyejua unaeweza kumdanganya kuhusu hili.

Nimesema nimeipitia vya kutosha hotuba hii, nimeiangalia kwa kina lakini pia mimi ni mjumbe wa kamati ya maendeleo na ustawi, nipo na watu wa Wizara ya Elimu ambao nipo nao katika bajeti. Kwa hivyo hili sidanganyi na nasema ndivyo ilivyo. Ni kipofu gani utakayemdanganya na nikiziwi gani asiyesikie, asiyejua habari za elimu zilivyotukwaza hapa kwetu Zanzibar. Mhe. Waziri kama ni watendaji wamekupotosha, ukweli wa mambo naomba unieleze na niweze kufahamu na Wazanzibari wajenge matumaini juu ya hili.

Mhe. Naibu Spika, katika ukurasa wa 21 katika kifungu cha 46 hapa kuna tathmini ya hali ya mahitaji ya wataalamu. Nashangazwa mno katika taifa letu ambalo linakwazwa na wataalamu kwa kila fani. Linashindwa kabisa kusimamia au kujibajeti kwa ajili ya kuekeza elimu kwa ajili ya kupata wataalamu wa baadae. Nini lengo hasa la serikali la kukwamua tatizo hili. Mimi nina taarifa inayosema kwamba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar inahitaji kuagizia walimu wa sayansi kutoka Nigeria. Hivi kuna nini tusijipange wenyewe tukaonesha katika bajeti kwamba tuna malengo. Nashangazwa vya kutoshwa, hapa tuna Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, mimi nina idadi ya watu 1600 ambao walihitaji kwenda kuchukua mafunzo ya elimu ya juu. Vijana hawa waliopata mikopo ni 300 tu.

Mhe. Waziri hebu niambie kwa sababu tuna matatizo ya wataalamu wengi katika sekta tofauti. Vipi umejipanga kwa ajili ya kuonesha katika bajeti yako kwamba sasa tunaekeza katika elimu tuondokane na kuagizia wataalamu kuondokana kabisa katika mambo ambayo hayakupaswa kufanywa na watu wageni, Wazanzibari wanao uwezo mzuri wa kusoma. Huko duniani katika nchi tofauti Wazanzibari walipo ni wataalamu wa sekta tofauti na sifa nyingi zinakuja Zanzibar kwamba vijana hao wanao uwezo mzuri.

Mhe. Waziri nakuomba sana muda umefika, muda ukitimia ni lazima kutekeleza azma ambayo itaondosha kero kwa ajili ya maslahi ya taifa hili bila ya wataalamu tusijidanganye tunawahitaji wataalamu. Wataalamu hawatozaliwa kama yai la kuku, hilo yai la kuku ni lazima mama naye awe atayarishe apatiwe na jogoo, hatimaye ndio lipatikane yai. Hivi sisi bila ya maandalizi haya wakati huu wa mapema wa kuonesha bajeti jinsi ilivyoonesha, tunakwenda wapi.

Mhe. Naibu Spika, katika ukurasa wa 37 katika maeneo ya Kipaumbele ya Bajeti katika mwaka uliokwisha. Huko tulikotoka bajeti ya 2011/2012 Mhe. Waziri uliisoma bajeti ile sote tulipiga makofi, na wananchi walijenga matumaini kusema kwamba sasa vipaumbele ni kwenye mapinduzi ya kilimo. Mhe. Waziri kwa masikitiko makubwa umewakata matumaini wakulima wa Zanzibar ya kutokujua wapi pa kuelekea wakiangalia ya kwamba, hatukujua kwamba hili zoezi la Mapinduzi ya Kilimo lilifikia hatua gani? Hii NERICA ilipatikana kiasi gani, tunaona tu kwamba imezalishwa na fedha nyingi zilitumika kwa ajili ya kuzizalisha mbegu hizo. Hebu twambie Mhe. Waziri tulifanikiwa kwa kiasi gani katika kilimo hichi cha mbegu hizi za NERICA na wananchi wamefaidika nini na unatarajia nini? Kama unatarajia mbona sikuona kuliingiza tena katika bajeti yako kulipa kipaumbele au wananchi sasa tayari wameshaingia katika chakula na lishe.

Mhe. Waziri, tunapojipangia mipango yetu kwa ajili ya maendeleo ya taifa hili tusiwe tunafanya mambo kwa kubahatisha, tufanye mambo yanayotustahiki kabisa. Wachumi wawe wanafikiria njia mbadala za kuweza kuondokana na umasikini wa kweli kwa Wazanzibari. Isiwe njia ya kuandikiana manambari na kuja kusomeana. Jamani Wazanzibari walio wengi nje kwa sasa ni wasomi, hawadanganyiki tena. Zamani ukisimama ukisema basi anaamini hilo limekwisha. Leo tumewasomesha vijana na wanao uwezo huo.

Mhe. Waziri, nirudie tena katika kipaumbele chako ambacho 2011/2012 ulikiweka, ulisema uimarishaji wa bahari kuu. Mheshimiwa sisi ni watu wa visiwa, bahari ndio rasilimali aliyotupa Mungu nayo. Tuambie mwaka jana ulisema mwaka huu una nini mbona sikuona matokeo yake. Zile meli na kampuni tena zimekwisha. Hivi tunawapa matarajio gani wavuvi wa Zanzibar. Tunawambia nini Wazanzibari wetu wa visiwa ambao wamezoea kula samaki, wamezoea kuzalisha samaki. Wana uwezo mzuri wa uvuvi. Mhe. Waziri kuacha vipaumbele hivi viwili vya kilimo na uvuvi kwa kweli Wazanzibari kumewavunja moyo, nawambia wachumi.

Mhe. Naibu Spika, sheria ilikuja na nadhani mnakumbuka nyote ya Uhakika wa Chakula na Lishe. Bila ya bahari tukapata hiyo *resource* iliyokuwepo hupo na bila ya kilimo sidhani kwamba taifa hili litakuwa limefikiwa katika malengo. Je, ile dhana ya chakula na lishe imeshapitwa na wakati, Wazanzibari wanashiba. Yale maghala ambayo tulisema tunajiwekea sasa basi yameshajaa hivyo vyakula.

Mhe. Naibu Spika, ukurasa wa 49 kifungu namba 99 Mapendekezo na Hatua za Kuimarisha Mapato. Mhe. Spika, hapa Waziri amenimaliza nguvu, maana aliitanguliza hoja yake kwa kusema hatoongeza kodi na baadae mwisho wa sentensi akaifungia. Lakini huku kuna nakisi ya bajeti itabidi itoke katika ongezeko tena lile lile la kodi. Nikawa najiuliza sasa haya maneno labda yalichezana au ikawa haikufahamika. Nikawa napata tabu kidogo sikujielewa.
Mhe. Waziri ukisema kwamba huongezi kodi na baadae ukapenya upande mwengine kuongeza nakisi ya bajeti ni lugha tofauti au ni vitendo tofauti. Naomba Mhe. Waziri utakapokuja na hili nalo unipatie jibu lake. Kwa masikitiko makubwa na huzuni nzito nimeona umeongeza ongezeko la ada huko bandarini, pahala ambapo hukuweza kupatunza huwezi kutoa mapato. Hivi kuna lipi kubwa lililoongezeka bandarini mpaka wananchi wanatozwa kodi tena. Imarisha kwanza ili uweze kufanya hilo. Kwa nini nasema hilo?

Kwa sababu sote ni mashahidi na ni waathirika wa tatizo ambalo lilijitokeza usiku wa tarehe 9 kuamkia tarehe 10 mwezi wa 9 kipindi kilichopita, kwa kuzama kwa Meli ya MV SPICE. Wazanzibari tuliingia katika kiza cha huzuni na Watanzani na Dunia nayo pia ilitupa mikono ya pole kwa tokeo kubwa kama lile. Nilitarajia bajeti hii serikali kwa kuthamini wananchi wake, kwa kuthamini pale pahala ambapo kodi inapatikana itaweza kuweka usafiri wa uhakika unaotoka Unguja kwenda Pemba. Kilichonishangaza zaidi ni kuona hapo pameongezwa ada ya mapato.

Mhe. Waziri ningeomba nione ya kwamba angalau serikali iliweka azma ya kusema tutanunua meli au tutafanya mikopo au tutafanya mazungumzo na matajiri fulani. Ili usafiri wa uhakika wa Wazanzibari hawa, kwa kukumbuka kile kidonda kikubwa tulichokuwa nacho. Lakini nilichokiona katika Bajeti hii hata uzalendo umepotea. Kwa sababu tumeliona hilo tungejenga imani ya kwamba hapa anapoongeza kodi basi angalau pawe pameimarishwa kuna usafiri wa uhakika.

Mhe. Naibu Spika, nimalize kwa kusema ya kwamba kuongezeka kwa kodi ya aina yoyote sitounga mkono bajeti hii, kwa sababu inamgusa mwananchi wa Zanzibari kwa asilimia 100. Hakuna mfanyabiashara

atakaeumia, hakuna tajiri atakaeumia, badala yake ni Wazanzibari wanaotarajia kujinasua na umasikini uliokithiri hata wa chakula. Sitounga mkono bajeti hii narudia tena mpaka pale Waziri atakaposema kaondosha kodi hii kwa ajili ya wananchi.
Baada ya kuyasema hayo Mhe. Naibu Spika, naomba kwa heshima na taadhima sasa nikae kitako.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipatia fursa ya kutoa mchango wangu kuhusu hoja iliopo mbele yetu. Awali ya yote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehma kuweza kutujaalia kuwa hai na hatimae kutupa uwezo wa kutoka majumbani mwetu mpaka katika jengo hili. Kuja kuzungumzia juu ya maendeleo ya nchi hii. Hizi si nguvu zetu bali ni uwezo wa Allah, kwa vyovyote vile hatuna budi kumshukuru.
Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu nadhani Mhe. Naibu Spika, nitakuwa mchache wa shukurani kama sikuweza kuitumia fursa hii kukushukuru wewe ambae umenipa nafasi hii, na mimi angalau kutia nyalio kuhusu bajeti ya mwaka huu. Kwa hili kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Wawi nasema ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, nadhani vile vile niungane na wenzangu kumpongeza Mhe. Mwakilishi Marina Joel kwa kuteuliwa na Mhe. Rais kuwa Mwakilishi. Kwa kweli Mhe. Rais chaguo lake limesibu sawa sawa kwa sisi wataalamu katika fani za viumbe kama binaadamu, tukimuangalia huyu mama tunamuona kwamba Mwenyezi Mungu kamjaalia vipaji vitatu vikubwa. Huyu mama anaonekana kwamba ana ubongo wa hekima, kipaji chake cha pili ana ulimi wa fasaha na cha tatu ana moyo wa unaoweza kuhifadhi siri za nchi hii likiwemo Baraza letu la Wawakilishi. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, ninamini huyu mama Mariana atawatetea Wazanzibari utumishi ulio makini, mahiri na karibu sana katika Baraza letu.

Mhe. Naibu Spika, kabla sijaenda katika ndani ya hiki kitabu, hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Mipango ya Maendeleo Mhe. Omar Yussuf Mzee kuhusu mpango wa maendeleo na makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka 2012/13.

Mhe. Naibu Spika, ili tuendelee sisi tuliokuwa katika Afro Shirazi au CCM mpaka sasa hivi tunaamini kwamba ili tuendelee tunahitaji mambo manne, watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora.

Mhe. Naibu Spika, katika nchi hii hakuna tatizo la siasa safi kwa sababu *GNU spirit* inatosha kuelekeza katika maendeleo makubwa. Kwa hivyo vile vile hakuna tatizo la ardhi kwa sababu ardhi imeshauzwa sana kwa wageni. Hivyo hata tukisema vipi ardhi hatuna.

Sasa nizungumzie watu. Kuhusu watu tunao Mhe. Naibu Spika, kama nchi inataka maendeleo lazima ijali raslimali watu. Wenzetu wa China wamefika walipofika kwa sababu ya kujali raslimali watu. La kusikitisha katika nchi hii kama kuna kitu serikali iliopo hii haijapa umuhimu wa mwanzo basi ni raslimali watu.

Mhe. Naibu Spika, hiki ni kisiwa. Kwa hivyo katika kisiwa tena kwa bahati kisiwa chenyewe Zanzibar ni yenye visiwa viwili vikubwa Unguja na Pemba. Zanzibar kutakuwa na haja ya maingiliano ya wenyewe baina ya Wazanzibari tena ya kila siku, saa kupitia usafiri.

Sasa wewe unakuna hapa na mpango wa maendeleo wa mwaka 2012/13 bila ya kujali maingiliano ya wananchi wa Ungunja na Pemba, tukuelewe vipi? Hawana usafiri siku zote watu hawa wanazama katika maboti, mara boti livutwe au lisikumwe, hawana usafiri wa uhakika. Leo umekuja hapa kwamba tukupe pesa shilingi bilioni mia sita na arobaini na nane, mia tisa na arobaini na nne. Huku walipo kodi wa nchi hii wakiendelea kuzama katika bahari. Hatumfahamu Mhe. Waziri hapa, humu hamna meli wasafirie nini hawa? Tutakuwa tunamtegemea Bakheressa mpaka lini? Waswahili wanasema “shike shike na mwenyewe upo nyuma”.

Mbona sisi katika Afro Shirazi tulikuwa na meli zaidi ya tatu? Hakuna meli hata moja ya serikali, ma-graduate nyote muliopo wakati sisi hatukusoma katika Afro Shirazi, kwa nini munashindwa kununua meli mpaka leo hii. Ni aibu na maendeleo hayawezi kupatikana wakati wa walipa kodi wa nchi hii wanaedelea kuzama kila siku baharini.

Juzi walizama zaidi ya watu elfu mbili, hebu ukifanya kwa mwaka utapata watu wangapi wanaozama. Ninadhani sisi hatujakufahamu Mhe. Waziri katika hili. Maana Mhe. Rais Aboud Jumbe Mwinyi na serikali yake pamoja na Waziri wa Fedha yule alikuwa Mpemba yule walimudu kununua *jet.* Sisi tunaona haya kwamba Rais anataka kusafiri anasubiri ndege hapa. Sisi tulikuwa na ndege iliharibika kwa bahati mbaya tu ile. Munatutia aibu watu wa serikali muna madaktari humu, maprofesa, munashindwa hata kumnunulia ndege Rais

wetu. Hatuwafahamu katika hili na ninachowaambia kwamba Mhe. Waziri hebu uje utupe maelezo, kwa nini katika bajeti yako hamna meli. Hilo ni moja.

Mhe. Naibu Spika, ninataka kuuliza swali moja na sijui nani atakayeweza kunijibu humu ndani ya Baraza. Hizi CCM hasa ni ngapi? Ninauliza hivi kwa sababu sheria Na. 5 ya mwaka 1995 imeweka mtandao wa vyama vya siasa, kuanzia tangu kule Mnarani Pemba mpaka Kigoma. Yaani chama kiwe cha kitaifa.

Wenzetu Tanganyika kulitokea ubadhirifu wa fedha za walipa kodi, ikasema ripoti ya CAG, Mhe. Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano akataka ridhaa kwa Chama chake cha Mapinduzi. Ni kesi ile ile tumeteuwa kamati teule ikaleta taarifa hapa kwa fedha za walipa kodi, Rais anatoka vile vile katika Chama cha Mapinduzi lakini haikuchukuliwa hatua yoyote.

Mpeni ruhusa Rais wetu Mhe. Shein na yeye atekeleze hayo maamuzi kama yaliyochukuliwa na Rais Kikwete kule. Mhe. Naibu Spika, ikiwa CCM si mbili kama alivyofanya Rais Tanzania Bara kule na kama CCM ni mbili, basi tunamuomba Rais wetu apate ridhaa kwa chama chake cha Mapinduzi ili achukua hatua kwa hawa wote wabadhirifu waliohusika kwa fedha za walipa kodi nao wachukuliwe hatua mmoja baada ya mwengine.

Sasa niende ndani Mhe. Naibu Spika, maana nilikuwa hapa nje tu; Mhe. Naibu Spika, katika ukurasa wa 17 ibara ya 16, 17 na 18 kwamba uchumi umekua kwa asilimia 6.8. Ukuaji huu wa uchumi ni aibu kusema kwa sababu haumnufaishi Mzanzibari katika kila hali.

Tuangalie pato la mtu kwa mwaka ni shilingi laki tisa na elfu sitini, kwa mwezi ni shilingi elfu thamanini, kwa siku pato la mtu ni shilingi mbili mia sita na sitini na sita. Mhe. Naibu Spika, mimi nina tatizo sana na hii bajeti na tatizo lenyewe linatokana na nini. Tunajitakia wenyewe huu umaskini.

Taasisi za uzalishaji kwa mfano mabenki, mahoteli, makampuni serikali haina utaratibu wa kuwa-asses hawa wawekezaji. Sisi tunachukua Wataliana, Wakenya tukiwapa hivi. Hivi sasa tukenda kote mahoteli wameliki ni Wataliana, wafanyakazi ni Wakenya na Wamasai. ‘Sasa zinazopatikana zinatumika Utaliana, Loliondo hazitumiki Zanzibar.

Mimi ninadhani Mhe. Naibu Spika, katika hili kuwe na sera maalum sasa ili fedha tupate kuzidhibiti. Leo unachukua mahoteli yote unawapa wageni na ajira zote unawapa nani kule.

Wenzetu wa China wanahamasisha local investors, matokeo yake makampuni makubwa ya China yanamilikiwa na Wachina wenyewe. Leo hapa munatwambia kwamba katika vijana watano ni mmoja tu aliyekuwa hana ajira, si kweli. Rais wetu ni lazima achukue hatua.

Hivi sasa Mhe. Naibu Spika, mimi nimeperuperuzi na kwenda kuangalia pale uwanja wa ndege ZAT wale ni wazalendo, wanalipa kodi na mwenyekiti wao ni Bwana Mohamedraza Hassanali. Wanataka kuwaondosha waweke hawa wageni. Kwa hili hatutokubali hata siku moja. Wale ZAT wameajiri vijana wetu wazawa 160 wa hapa hapa nchini.

Hawa TRA wamelipwa shilingi bilioni moja milioni mbili sitini na mbili. Hawana deni ZRB, ZSFF. Tatizo la bajeti hii haiku-exhaust vyanzo vya mapato. Tatizo kubwa ni kwamba uchumi wa nchi hii unatumia siasa badala ya siasa kutumia uchumi. Siku zote inatakiwa siasa itumikie uchumi, sio uchumi kutumia siasa.

Unapopeleka siasa katika uchumi ni tatizo na kuleta umaskini katika nchi. Hapa tumeshaamua katika Baraza lililopita kwamba mafuta ni ya Wazanzibari, laiti yale mafuta ingelikuwa ni kama vile maji unachimba kisima haki ya Mungu tungekuwa tushayachimba. Baraza limeamua na mimi ninaungana na hoja ya Mhe. Omar Shehe na alete hoja yake hapa ya kuanzisha chombo cha uchimbaji wa mafuta.

Mhe. Naibu Spika, laiti uchumi usingekuwa unatumikia siasa tusingekuwa tumo kwenye OIC ili uchumi wa nchi hii ukawa unatononoka, ruzuku na misaada kwa ndugu zetu wa Msumbiji wanapata sana lakini sisi tunaogopa, ukiogopa mwana kulia utalia wewe. Sisi tunawaogopa Watanganyika.

Mhe. Naibu Spika, katika ukurasa wa 11 na 12 paragraph ya 22, ningependa kuipongeza serikali katika hili pale Waziri alipozungumzia juu ya afya ya mama na mtoto. Mimi ni mdau wa akinamama na msemaji sana wa hawa akinamama na nitaendelea kusema sana katika hili.

Mimi nipo katika Kamati ile ya Ustawi wa Jamii Wanawake na Watoto. Sasa niipongeze serikali pamoja na mikakati yoyote imeeleza kufanya utafiti wa akinamama na mtoto. Lakini juzi nimealikwa katika Bunge la Afrika ya Mashariki hapo Arusha. Hawa EAC wanataka ku-harmonize mother, new born and child motality. Yaani wanataka kuweka strategic zile za kunusuru vifo vya mama, mchanga na watoto.

Sasa ili tusiwe nyuma katika hili kwa sababu wenzetu wamezim-improve katika kuona kwamba hili wana-minimize mortality kwa ku-improve bajeti zao. Sasa Mhe. Waziri hapa ataniambia vipi ili Wakenya, Waburundi wasije wakatuacha nyuma. Hili itabidi Mhe. Waziri aje anieleze.

Mhe. Naibu Spika, katika hili ni lazima tukubali kwamba hali ya afya ya mama na mtoto ni mbaya sana, lazima tujikaze kwa sababu kwa mujibu wa health data ya mwaka 2011, akinamama wanaojifungua katika vituo vya afya ni asilimia 70.8, ina maana wengine wanajifungulia vichochoroni huko. Kwa hivyo hii idadi ya watoto kufa ni kubwa sana.

Jengine ni kiwango kidogo cha wale ambao wamejisali katika uzazi wa mpango ni asilimia 12.4 tu kuanzia katika mwaka 2010. Sasa tatizo hili ili tupate afya ya mama awe anazaa vizuri na uwitikiaji wa mama na baba katika uzazi mpango ni mdogo sana katika bajeti hii ya mwaka huu. Imelionaje hili ili kuona kwamba akinamama na akinababa wanajipeleka wenyewe kule angalau ku-improve hii bajeti yetu ikoje katika hili.

Kliniki zilizopo ni karibu asilimia 99 akinababa wanapata hata zile sehemu ambazo out service ni nyingi, kuna zile *mobile clinics* zinakwenda huko katika sehemu za remote area. Lakini akinamama wanaopata wajawazito mpaka kujifungua katika kliniki hizo ni asilimia 49 tu, 51 wapo nyumbani na vitumbo vyao tu.

Sasa Mhe. Waziri katika hili Mhe. Spika, ili tusiachwe nyuma na wenzetu wa Kenya, Uganda kwa sababu wana-harmonize haya mambo itakuwaje angalau hii asilimia 51 nayo iweze kwenda kupima uja uzito.

Mhe. Naibu Spika, sasa niende katika usafiri wa barabarani kwenye ukurasa wa 16 ibara 55, marekebisho ya viwango vya leseni. Katika hili kuna kutozwa shilingi elfu kumi na tano na vile vile kuna kodi ya mafuta imepandishwa shilingi hamsini. Ninaanza kupata tatizo kidogo. Hizi gari zinazotoa huduma kwa wananchi yaani daladala, wataanza kupandisha na wao na kuwatoza wananchi nauli kubwa.

Mimi ninadhani hili tungelifanya kwa zile gari za mizigo na za starehe, lakini hizi gari za daladala halafu huku wana TRA, ukipiga mahesabu kwa mwaka wanalipa karibu shilingi laki mbili ushuru pamoja na leseni. Kwa mfano kama kule kwetu katika siku 30 wanatoka siku 15 za kazi, halafu kodi kubwa namna hii. Wao wataendelea kutukomoa sisi kwa nauli. Mimi ninasema hii sikatai mpango huu lakini zingelifanywa kwa gari zile za mizigo pamoja na za starehe. Hawa watu wa daladala watatuuwa.

Mhe. Naibu Spika, halafu tumeambiwa kuna pesa ambazo za shilingi kumi na tano katika kodi hii zitatumika kwa ajili ya kununua madawa. Mhe. Spika, ninataka hawa wataalamu, wana-*create* mind lakini vile vile wawe na *dynamic decision*. Kwa sababu hawa wataalamu wameleta shilingi kumi na tano kwa kila itoe na kwa sababu magari yamekuwa ni mengi, yanamwaga moshi kwa mujibu wa hotuba ya Mhe. Waziri kwa hivyo yanasababisha mambo haya ya mazingira.

Magari kumwaga moshi ina hewa inakuwa polluted na *carbon dioxide* pamoja na *carbon monoxide*. Sasa ukiniambia unakwenda kununua dawa mimi siwafahamu hawa watalaamu. Hewa hizi zinazopokuwa nyingi na kwa sababu magari yameshakuwa mengi na kisiwa ni kidogo, tutarejea kuwa hewa ikiwa *polluted* watu watavuta hewa, wakivuta hewa hii *carbon dioxide* inachanganyika na rangi nyekundu kwenye damu ambayo inayoitwa *hemoglobin* ambayo ni sumu. Hii ikiingia katika *cells* zinaziuwa, hivyo uwezekano wa kupata kensa hapo mbele Wazanzibari ni mkubwa, hii ni kutokana na kisayansi ongezeko kutokana na ongezeko la hizi gari na mabadiliko ya tabia ya nchi basi uwezekano wa Wazanzibari ni mkubwa sana.
Leo mimi nilifikiri hizi shilingi elfu kumi na tano wanazotozwa magari, wangefikiria kuweka pale Hospitali ya Mnazi Mmoja …

Mhe. Naibu Spika: Bado dakika 5

Mhe. Saleh Nassor Juma: Kumbe wanakwenda kununua dawa za kutibu homa, wakati magari yanatusababishia kensa, sisi twende Hospitali ya Ocean Road mpaka lini. Ni tatizo hilo wataalamu lazima pesa hizi muhakikishe kwamba zinatumika kwa lile lengo. Hizi zimetolewa kwa sababu ya kutoa magesi.

Mhe.Naibu Spika, katika suala zima la kuhifadhi mazingira na hii ya tabia ya nchi ni kwamba serikali haipo serious haipo na suala hili. Laiti wangelikuwa serious hawa tungemuona profesa Rai aanzishe *department of environment* pale SUZA, kusudi apale wataalamu wa kusaidia nchi kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi.

Kashindwa kuingiziwa fedha kuanzisha hiyo. Mimi nina ushahidi sio ninasema tu kwa sababu mimi ni mjumbe wa kamati tunakwenda pale kila siku Rai anatueeleza kwamba anataka kuanzisha *department ya environment*, anashindwa na kitabu hiki hakikuelezwa chochote zaidi ya kusema kuwa atakusanya kumi na tano atanunulia dawa na kupandia miti, huku wataalamu wa kupambana na mazingira hakuna.

Sasa mimi nilikuwa ninafikiria jambo moja Mhe. Mwenyekiti, bajeti yetu hii iwe *creative*, ipeleke pesa hizi katika kuona mazingira tunayadhibiti vipi na kupambana vipi na mabadiliko ya tabia ya nchi kwa kuanzisha *department of environme*nt katika Chuo Kikuu cha SUZA.

Mhe. Naibu Spika: La mwisho hilo liwe.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Spika, muungano ni jinamizi sana kwa uchumi na siasa za nchi. Ninawaomba wananchi wa Zanzibar wajitokeze kwa wingi itakapokuja Tume hii ya kukusanya maoni kusudi wakatoa maoni yao kwa tume kuhusiana na Katiba. Hii ni haki yao, wahakikishe kwamba sisi kama ni wawakilishi wa nchi hii tutayathamini mawazo yao.

Wao kama wanataka kwennda Pemba basi hawezi kwenda kwa miguu. Ninawaambia Wazanzibari wenzangu kama unataka kwenda Pemba basi upande meli, boti, ngalawa au ndege. Lakini kwa kusema unakwenda kwa miguu hufiki. Chombo pekee cha kufikia huko wanakokutaka Wazanzibari ni hii Tume inayoongozwa na Jaji Warioba ya Kuratibu Maoni.

Na mimi nina amini kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu itawafikisha wanakokutaka. Waende kwa wingi kutoa maoni, watoe maoni yao, waseme wanalolitaka na maamuzi wanayoyataka wananchi basi tutahakikisha tunakuwa nao bega kwa bega kama wawakilishi wao. Tunawaahidi wananchi hilo, watulie, waitunze amani iliopo na wajitokeze kwa wingi katika kutoa maoni yao na sisi tupo pamoja na musiwe na wasi wasi na hili. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Ninakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, jioni hii ya leo kunipa fursa na mimi niseme maneno mawili matatu katika hotuba hii ya bajeti ya Waziri wa Fedha na Uchumi.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kuanza na mimi nimpongeze Mhe. Mariana ambaye ameteuliwa na Mhe. Rais. Kwa kweli Mhe. Rais hakufanya makosa, kamuona kama Mhe. Mariana anatufaa.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwanza ninataka nizungumze kuhusu masuala bajeti yetu. Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, maneno yaliomo katika kitabu hiki cha bajeti ni mazuri ukiangalia. Lakini sasa sisi Wazanzibari tuna tabia moja ambayo kuwa inakuwa kama mila yetu.
Mhe. Naibu Spika, Wazanzibari tuna tabia ya kupanga mambo lakini utekelezaji wake unakuwa hatufiki. Katika bajeti yetu Mhe. Waziri ametueleza jinsi ya ukuaji wa uchumi katika nchi yetu. Mimi ninakubaliana na yeye kama walivyozungumza wenzangu kama ni kweli uchumi umekua, lakini uchumi umekua katika nyanja zile ambazo zimo katika serikali tu. Lakini ukenda kwa wananchi pamoja na ukuaji wa uchumi basi watawakuta wananchi waliopo chini hawafaidiki na ukuaji huo wa uchumi.

Kama walivyozungumza wenzangu Mhe. Naibu Spika, na mimi katika maoni yangu ni kwa sababu nyanja zile zilizosababisha ukuaji katika nchi yetu, basi ni zile nyanja ambazo zaidi zimemilikiwa na wageni wasiokuwa Wazanzibari, sasa fedha zinazunguka nje ya nchi ya Zanzibar. Kwa hivyo wale wananchi wa chini hawafaidiki.

Sasa hivi mwananchi wa chini ukimwambia kuwa uchumi umekua hawezi kukubali kwa sababu anaona hali ya umaskini imezidi, hali ni ngumu kwa hivyo mwananchi wa kawaida hata ukimwambia hakuelewi kabisa kama uchumi umekua. Kwa sababu sasa hivi mwananchi wa kawaida hata chakula cha mlo mmoja ni tatizo.

Ukiangalia fedha zilizokimbia katika nchi yetu Mhe. Naibu Spika, unaona jinsi ya watu wanavyohangaika na kupata taabu. Sasa uchumi umekua lakini umekua ndani ya serikali yetu tu kwa zile nyanja ambazo hazina faida kwa wananchi.

Kwa mfano mahoteli Mhe. Naibu Spika, au mabenki mheshimiwa kajibu humu katika kijitabu chake kama benki hivi sasa zinakopesha pesa nyingi kwa wananchi, lakini wananchi wanaokopa haziwafaidishi kwa sababu

benki unakopa kuna riba na baada ya riba kuingia fedha zile zinafaidisha katika yale mabenki, wenye mabenki wanazichukua wanakwenda kuzitumia nje ya nchi ya Zanzibar.

Kwa hivyo wananchi waliopo ndani ya nchi ya Zanzibari hawafaidiki na uchumi huu unaokua. Sasa lazima hili tulione na la pili waheshimiwa tunapotunga bajetu ni lazima tuangalie wananchi wetu walio chini kwa sababu tukitunga bajeti yetu tuangalie kwamba jee bajeti hii wananchi waliopo chini au walala hoi itawafaidisha vipi, tusiangalie tu kwenye mapato ya serikali lakini na hawa wa chini tuwaangalie. Sasa wananchi walio chini hatuwaangalii. Kwa hivyo mwananchi ukimwambia kuwa uchumi umekua hakukubalii hata siku moja.

Suala la pili Mhe. Naibu Spika, katika bajeti yetu Mhe. Waziri amezungumza kuhusu ajira na akasema kwenye vijana watano basi mmoja tu ndiye aliyekuwa hana kazi au hana ajira. Mimi hili kwanza sikubaliani na yeye. Mimi ninalichukua kinyume na hivyo. Kama katika wananchi watano basi hata mmoja hana kazi. Huo ndio ukweli ulivyo. Lazima tuseme ukweli kwa sababu tukisema ukweli wananchi wetu watatuelewa kuwa tunasema nini lakini tukiwadanganya sasa hivi watu wameshakuwa macho kila mmoja anakifahamu kisema.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ambalo ninalotaka kulizungumza katika bajeti yetu ni suala la uongezaji wa kodi. Mhe. Naibu Spika, ng'ombe ukimkamua sana basi mwisho anatoka damu, badala ya kutoka maziwa basi anatoka damu. Kwa kweli ongezaji wa kodi ni kuwakamua wananchi wetu mno na hali ni ngumu mno ya kimaisha, lazima wananchi tuwahurumie. Hali ni ngumu kupita kiasi.

Leo Mhe. Naibu Spika, tungekuwa tunakusanya kodi zetu na kuzisimamia hazivuji basi serikali ingetosheka na hizi ziliopo. Lakini leo wananchi waliopo pale Darajani, wale wote wanalipia kodi zinazostahiki, kodi zinafika tatu au nne. Lakini wananchi wale pale ukiwatizama wote hapana aliyepewa leseni ya biashara. Kodi hizo zinakusanywa zinakwenda wapi? Mtu hana leseni ya biashara, halafu munakusanya kodi zinakwenda wapi bila shaka zinakwenda mifukoni mwa watu.

Kwa maana hiyo Mhe. Naibu Spika, kodi za nchi yetu zinavuja. Kila tukisema tuangalie kama watu wanachosema, tumeunda tume hii imeleta ripoti yake lakini haisimamiwi. Mhe. Naibu Spika, tunasema bado serikali yetu haijawa makini katika ukusanyaji wa kodi na kodi zinavuja. Mapato ya serikali yanavuja na kuingia kwenye watu wachache, haziendi kwenye serikali.

Kwa kweli serikali yetu ingekuwa fedha zinazokusanywa zinakwenda katika serikali basi tungeepukana na tegemezi, lakini sisi sasa hivi ukiangalia bajeti yetu hivi, jinsi tulivyokuwa wategemezi ni aibu hata kusema sisi wenyewe. Sasa ili kuepukana na haya ni kwamba serikali isimame kidete kusimamia kodi zake za serikali, yale makusanyo yanayokusanywa yasivuje. Lakini leo makusanyo yanakusanywa lakini yanavuja tu pesa hatujui zinapokwenda na kila upande unaokwenda.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ninalotaka kulizungumza katika bajeti hii kila siku tukija katika Baraza hili, tunazungumza kuhusu suala la umeme kama Zanzibar tunahitaji wa kumiliki wetu wenyewe, tusiwe wategemezi wa umeme. Kila leo tunazungumza na tunaambiwa mushakwenda kuleta waya wa umeme unaounganishwa kutoka Ubungo, Ras Kilomoni mpaka Fumba uje uje zake Mtoni. Jamani mpaka lini haya tunasema kila siku haya kuwa umeme huu hautufai tunataka tuwe na wetu. Wenzetu walitupandishia kodi hapa, ikawa siku nenda siku rudi tunapapatua kuhusu bei ya umeme, leo tunasema Zanzibar tuwe na umeme wetu wa kudumu.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri katueleza tu kuwa tuna mradi wa umeme, hajatueleza tena kuwa ule umeme kuwa nyenzo za umeme lakini zile njia hasa, serikali hasa bado haijataka kuwa na umeme Zanzibar. Kwa sababu mungetueleza ni njia gani za kuwa na umeme wa kudumu. Lakini mara munatwambia kuwa tutapata umeme wa takataka, umeme wa upepo, hatujui kwa kweli umeme upi ambao Zanzibar utakaotufaa.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri atupe hasa ni njia gani Zanzibar tutakuwa na umeme wetu wa kujitegemea, kwa sababu mpaka hivi sasa hatuzalishi hata watt moja ya umeme. Lakini yale majenereta 32 yaliopo pale hatuthubutu hata kuyagusa. Sasa ni sawa sawa na kuwa.

Mhe. Naibu Spika, wawekezaji hawawezi kuja kuekeza kwa sababu hatuna umeme wa uhakika. Hata huo umeme wa Ras Kilomoni utakuwa si wa uhakika kwa sababu umeme ule tunatoka nao mbali tena ni baharini, wakati wowote unaweza ukaleta short baharini tukaharibikiwa kama tulivyoharibiwa. Lakini tukiwa na umeme wetu wa hapa, hao waekezaji wakija wataekeza.

Mhe. Naibu Spika, tuna maeneo tunayaita maeneo huru ya vitega uchumi nako ni Micheweni na Fumba. Nani atakuja kuekeza wakati hatuna hata umeme wa uhakika? Yatakaa yale maeneo tuyaite maeneo huru mpaka dunia imalize. Lakini hatujui kama mwaka gani yatakuwa ni maeneo yanayovutia.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ambalo ninalotaka kulizungumza. Kama walivyozungumza wenzangu waliopita jamani Zanzibar kila siku tunasema ni visiwa. Kama Zanzibar ni visiwa, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inahitaji kuwa na meli zake. Hata kama kuna meli gani za matajiri lakini serikali inahitaji kuwa na meli zake.

Kwa sababu wafanyabiashara ni watu wenye hiyari zao, wanaweza wakapandisha wakati wowote bei, lakini serikali ndio mkombozi wa wananchi. Leo hapa Mhe. Naibu Spika, katika kitabu chake cha bajeti kuna matokeo ambayo yametokea ni moja ni ndugu zetu kupoteza maisha yao, akataka tuwaombee dua. Sasa baada ya kuwaombea dua lakini sasa jee hufikirii kuwa watu wale baada ya kwisha kuzima, sasa tuweke chombo ambacho watu wale wananusurika na ile hali ilivyotokea. Jamani sisi tunaelekea wapi, serikali hii kila tukisema humu tunakaa tunapiga kelele yanapita huku na kutokea huku. Kwa nini hayatekelezwi haya tunayoyasema. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, suala jengine nitakalolizungumze sasa hivi ni suala la muungano. Mhe. Naibu Spika, ninasema Wazanzibari wote au pamoja na mimi mwenyewe, mimi ninataka muungano lakini muungano sio ulivyo hivi sasa. Huu muungano ulivyo hivi sasa siutaki kwa sababu muungano huu ni muungano wa kunyonya upande mmoja. Sisi hatujaungana hivi sasa, tumeungwa hatujaungana. Wazanzibari tangu siku tuwe katika Serikali ya Muungano, leo kwa nini Wazanzibari mpaka tuwe tunagaiwa asilimia 4.5 iwe hivyo na sisi tumeungana ni nchi mbili. Nchi tumeungana ni nchi mbili sawa sawa, kwa nini tugaiwe hivyo.

Sisi baada ya kwisha kuungana zile nyenzo zote za uchumi wamezichukua Watanganyika sisi hatuna nyenzo hata moja. Mambo yote ya fedha wanazo wao. Mwisho watu wa BOT wanasema hakuna chumi mbili katika nchi moja. Kwa maana hiyo Wazanzibari sisi hakuna chumi mbili na uchumi wetu mmoja. Sasa tukiwa Zanzibar ni nchi na ina serikali tutapata wapi uchumi wa kuendesha nchi yetu na sisi tumedhibitiwa na wenzetu.

Halafu muje museme tumeungana tumeungwa. Halafu muungano huu munasema muungano umetulea, huu muungano umetugawa kwa sababu muungano unatupotugawa kwamba Wazanzibari zile nyenzo zote za kudhibiti nchi yetu, hatuna mamlaka ya kuchagua kiongozi wetu. Leo Rais wetu akiondoka Tanganyika hajulikani, akitoka hapo akenda Uganda hajulikani kama ni Rais wa Zanzibar. Anajulikana Rais wa Zanzibar kwa Zanzibar na Bara tu, Bara hiyo ya Dar es Salaam. Kwa nini jamani?

Tunasema wakati ukifika lazima mtu abadilike na upepo ulivyo. Wazanzibari hivi sasa wameshituka wanataka nchi ikomboke na sisi tunataka madaraka ya nchi yetu, tuwe na uhuru wa kujitawala, kuamua na kujulikana. Wazanzibari wamepoteza haki zao zote. Kwa hivyo mimi ninawasihi Wazanzibari wawe wastatulivu, wastahamilivu. Haki haichukuliwi kwa nguvu, twende kwa kudai haki yetu kwa taratibu na ninawasihi Wazanzibari nyote tuungane tuwe kitu kimoja tuache tofauti zotu tulizonazo, tupo mahali pabaya sana musifanya masikhara. Nchi inakwenda hii, musione sisi tukipiga kelele hapa mukafikiri tunapiga kelele tu, tunakwenda mbali, hatuna hadhi hata moja, hatuna mamlaka hata moja.

Fursa Mwenyezi Mungu ameileta hii, tuache tofauti zetu tuungane ili kuikomboa nchi hii. Zanzibar imekwisha hatuna mamlaka, tukitoka hapa madaraka yetu mwisho Chumbe tuliyo nayo Wazanzibari. Kwa hivyo tunataka tuwe na serikali yenye mamlaka. Zanzibar yenye kujitawala sio kama hivi tulivyo.

Marehemu Karume Mhe. Naibu Spika, huko nyuma alisema vipi. Muungano huu ni kama koti ukinibana nitavua lakini sisi tunakaa tunaona hasara kusema kweli. Lazima viongozi lazima tuseme ukweli na tuwe na uchungu wa hii nchi yetu. Hii ni nchi yetu, ni raslimali tumepewa na Mwenyezi Mungu ni hazina hii. Kwa hivyo lazima tuwe na uchungu na nchi yetu. Hivyo kama mtu hajajivunia nchi yake atajivunia nchi ipi? Hivi mukikosa hii Zanzibar mutapata nchi gani?

Kwa hivyo sisi tunapiga makelele kwa kuona uchungu viongozi wetu kwa kuwatetea viongozi wetu ili wawe na hadhi na maamuzi. Si kwamba tuamuliwe kila mara tunataka kuamuliwa tu sisi.
Mhe. Naibu Spika, kwa hayo machache ninaunga mkono hoja. (*Makofi*).

Mhe. Mansour Yussuf Himid (Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Naibu Spika, nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, muumba mbingu na ardhi, kwa kunijaalia

kukutana tena kwenye Baraza hili tukufu la wananchi wa Zanzibar na kutupa uwezo kushiriki katika shughuli muhimu hizi za ujenzi wa nchi yetu.

Kwanza nianzie kwa kumpongeza na kumshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein kwa umahiri na umakini wake mkubwa sana alionesha tangu achaguliwe kuwa Rais wa nchi yetu katika uongozi wa nchi hii.

Pia naomba nichukue nafasi hii adhimu kumshukuru ndugu yangu Mhe. Omar Yussuf Mzee na yeye kwa kazi yake makini anayoifanya katika uongozaji wa Wizara ya Fedha na Uchumi, Mipango ya Maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, naanza kwanza kwa kuunga mkono hoja kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kiembesamaki. Ninaamini serikali imetuletea bajeti mwanana, yenye kujenga matumaini makubwa kwa wananchi wa visiwa hivi. Mhe. Naibu Spika, tangu kipindi hiki au msimu huu wa bajeti uanze katika ukanda wetu huu wa Afrika ya Mashariki. Nimekuwa nikifuatilia kwa karibu sana bajeti ya Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi na Tanzania Bara, ili nijionee nini malengo yao, vipaumbele vyao kwenye bajeti ya mwaka huu, malengo yao ya muda mfupi na muda wa kati na nini wamedhamiria katika ile mikataba na wananchi wao na vipi watafikia malengo hayo kwa mwaka huu wa fedha, pia malengo yao ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kutizama hayo na kutizama bajeti yetu kwa makini sana, ndio nimefikia maamuzi ya kwamba bajeti tuliyokuwanayo ni bajeti iliyolenga kwenye *social justice*, inayotimiza pia malengo ya Mapinduzi matukufu ya Januari 12 mwaka 1964.

Mhe. Naibu Spika, tunapotizama bajeti ni lazima tuitizame bajeti kwa upeo wa kinchi, kwa kutizama mustakabali wa muda mrefu wa nchi yetu. Ni rahisi sana serikali kutafuta umaarufu ikakopa kushinda uwezo wake wa kukopa na ndani ya mwaka mmoja ikajijengea umaarufu mkubwa sana, lakini taathira itakayoiacha kwa tulio hai na vizazi vyetu tutashindwa kuhimili. Ndio maana waziri ametuambia hapa deni letu la taifa ni asilimia 15 tu ya GDP. Ukitizama nchi jirani wengine ni mara tatu au mara nne zaidi ya hii. Ukitizama bajeti ya Kenya wanasema wanaimudu kwa asilimia 86, lakini mtiririko wa ukopaji wao wa miaka 10 iliyopita pamoja na mwaka huu, ni zaidi ya asilimia 50 ya GDP yao. Ukitokezea mtikisiko kidogo tu, basi watashindwa kuhimili mwelekeo wa uchumi wao na ndio maana pamoja na taathira za kiuchumi duniani, bado hatujaingia k

Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa Wajumbe wengi nimewasikia wakizungumzia kodi. Mhe. Spika, njia moja tu ya serikali kujitafutia fedha ya kuendesha shughuli zake ni kodi, serikali haina biashara nyengine. Tumeondokana na zama zile za ki-*socialist* kwenye uchumi hodhi. Hivi sasa serikali inajipatia fedha zake kwa kupitia kodi. Nimelinganisha pia viwango vya kodi chache sana zilizopandishwa kwenye bajeti hii na nimelinganisha na wingi na viwango vikubwa vya kodi vilivyopandishwa na nchi jirani na sisi, huwezi kulinganisha. Bado serikali yetu imejitahidi mno kuhakikisha kwamba mzigo wa kodi kwa wananchi unaendelea kuwa mdogo. Lakini pia ni lazima tuzingatie nini mipango ya serikali katika matumizi ya kodi hizo na ndio maana nikasema, bajeti hii imewalenga kuwatengenezea unafuu na kuwajengea misingi imara wananchi walio wengi ndani ya nchi yetu.

Kwa mfano Mhe. Naibu Spika, kwa mara ya mwanzo. Maana yake mimi nimo ndani ya serikali nikiwa waziri huu mwaka wa 12. Serikali imeonesha ufundi mkubwa katika kupanga vipaumbele na hatimaye matumizi ya fedha zinazopatikana kwa kupitia kodi za wananchi wetu. Kuna ufundi mkubwa umetumika hapa na ninaendelea kumpongeza Mhe. Omar Yussuf. Kodi mahsusi zimelengwa kwenye maeneo mahsusi.

Kwa mfano, sekta ya afya ikiwemo sisi wenyewe kuanza kujitegemea kwenye masuala ya dawa za msingi na vitendea kazi vya msingi ndani ya hospitali zetu. Madeksi, serikali iliona kwamba kuendelea na mpango huu kutachukua miaka 10 au 15 zaidi hatujamaliza mahitaji yetu ya leo na bado huko mahitaji yanaongezeka, lakini serikali imepanga kodi mahsusi kwenda kwenye kutatua tatizo la madeski tulilokuwa nalo, tukiwa wawakilishi wa wananchi sote ni mashuhuda namna vijana wetu maskulini wanavyopata tabu, ikiwemo mipango maalum ya kuwaajiri walimu, hasa walimu wa sayansi.

Mhe. Naibu Spika, tumekuwa tukiwazungumza humu walemavu kwa miongo mingi sana. Lakini kwa mara ya mwanzo ndani ya historia ya nchi yetu. Wazungu wanasema *is putting the money where the mouth is*. Kwa maana sasa kwa mara ya mwanzo zinatengwa fedha kwa mipango maalum ya kuwasaidia ndugu zetu walemavu ambao ni wengi ndani ya nchi yetu, na wamekuwa kwa muda mrefu sasa wana malalamiko mengi na hawapati msaada wa kuweza kuwasaidia. Wanahitaji ushauri nasaha, wengine wanahitaji vifaa maalum vya kuweza kuwasaidia katika kurahisisha maisha yao ya kila siku. Kwa muda mrefu tumekuwa tukiyasema haya, lakini

hatua maalum zilikuwa hazipo, lakini leo tumeanza kufikia hapo. Yote haya ni ubunifu wa serikali kuweza kutumia misingi imara iliyopo ya kiuchumi ndani ya nchi yetu, ikiwemo ongezeko la ukusanyaji wa mapato na kuelekeza kwenye sehemu maalum ya vipaumbele ili tuweze kutoka hapa tulipo tusogee mbele zaidi.

Mhe. Naibu Spika, kuna kilio cha wafanyabiashara cha muda mwingi sana, cha ada ya usajili kwenye mikopo. Mhe. Waziri ametueleza hapa kwamba na amana ndani ya benki zimeongezeka, mikopo imeongezeka. Lakini kwa muda mwingi sana wengi wameshindwa kukopa kutokana na hii ada ya usajili wa asilimia moja ambayo ni kubwa mno. Lakini jambo la faraja ni kwamba serikali imeamua kwa makusudi sasa kwamba ada hiyo ya usajili itakuwa na kikomo, na ni matumaini yetu kwamba Mhe. Waziri atalisimamia hili ili kuhakikisha linafanyiwa kazi kwa haraka na linakuwa lina maslahi na tija kwa wakopaji wa nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, kwa muda mrefu sana na kwa bahati mbaya sana, unapozungumza utajiri kutokana pengine na asili yetu ya ki-*socialist* tunaanza kupiga kelele. Maneno mengi yamesemwa humu, wanaofaidika ni wenye hoteli tu. Benki inapokopesha ina vigezo na vipimo vyake, sekta ya utalii ni sekta moja inayokua kwa haraka sana na yenye uhakika wa urejeshwaji wa mapato. Kwa hivyo, ni jambo la msingi kwamba benki zitaelekea kwa wakopaji wa sekta ya utalii kwa sababu kuna uhakika na kinachopatikana, na idadi ya watalii inaongezeka na fedha ya kufanyia biashara ndani ya sekta ile ni fedha za kigeni.

Mhe. Naibu Spika, hata hivyo naamini kwa maana tumelizungumza ndani ya serikali. Nchi nyengine wana vigezo maalum kwa hizi sehemu za jamii zinazoitwa *middle class*, pengine *upper middle class*, *lower middle class*. Kwa mfano mtu kafungua duka Darajani, kaendelea Mlandege. Lakini na hawa pia wanaoshajihisha ukuaji wa uchumi katika kuekeza ndani ya nchi yao. Kwa sababu unapofungua duka utaajiri, gari zitapata biashara, wachukuzi watapata biashara, utalipa umeme, utalipa maji na utalipa kodi. Kwa hivyo, sehemu hii ya jamii inapaswa kufikiriwa, ili nayo itowe mchango mkubwa zaidi katika uwekezaji wa rasilimali ndani ya nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, lazima tunapotizama bajeti ya nchi yetu tuitizame kwa upeo wa kinchi. Tukiwa wawakilishi wa wananchi, hatupaswi kuzitizama bajeti zetu hizi kwa upeo finyu. Kama nilivyosema nchi zote jirani kwenye msimu wa bajeti ya mwaka huu wamepandisha kodi tena nyingi, na kwa viwango vikubwa zaidi kushinda hata bajeti ya Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar. Sababu ziko nyingi.

Mhe. Naibu Spika, kuna msukosuko wa uchumi duniani, kuna kitu kinaitwa *donor fatigue*, wanaotusaidia na wao wameshachoka, kwa sababu wao ndio waliokumbwa na msukosuko huu wa kiuchumi duniani. Kama hatujaanza kuelekea katika kujitegemea na tukabeba mzigo wetu sisi wenyewe, basi tusitegemee kwamba tutaendelea kupata watu wa kuendelea kutusaidia katika miongo ijayo, na ni lazima liwe jambo la faraja kwetu, serikali inapojiamini kwa kiasi ikaanza kusema kwamba sasa muelekeo, tunaelekea sasa katika kuondoka kwenye utegemezi kwenye sekta ya afya, tunaendelea kuondoka kwenye utegemezi kwenye sekta nyengine, haya ni mambo ya faraja na yanaondosha ile dhana ya kwamba serikali haina vipaumbele, haina mwelekeo wala haina malengo katika bajeti yake. Naomba nirejee tena kwamba ni muhimu tuutizame kwa upeo mkubwa na tuwe makini pale ambapo tunatizama masuala ambayo yako wazi, na pia uzalendo ni sehemu ya utekelezaji wa wajibu wetu.

Mhe. Naibu Spika, kilimo kimezungumzwa. Mkitizama kasma ya matumizi ya sekta ya kilimo, mtakuta imepanda kwa zaidi ya asilimia 100. Sio kweli kwamba sekta ya kilimo haina kipaumbele. Kipaumbele kwenye kilimo kipo, utekelezaji wake umeshaanza tangu mwaka uliopita wa bajeti, mafanikio yake tumeyaona na kasoro zake pia zimedhihirika, yalizungumzwa hapa. Naamini waziri husika atakapokuja mbele ya Baraza hili tukufu atatoa maelezo ya ufasaha zaidi.

Mhe. Naibu Spika, kuna swala moja ambalo mimi natofautiana sana na wajumbe wenzangu wa Baraza hili tukufu. Kuna dhana inajengeka ambayo nahisi italeta taathira kubwa sana katika nchi yetu na hasa kwenye utendaji wa serikali. Kuna dhana inaanza kujengeka kwamba watendaji wote wa serikali ni wabaya, wabadhirifu, wezi. Mimi naamini jambo hili sio sahihi na tukiwa wawakilishi wa wananchi wenye dhamana na dhima, basi nahisi tuna wajibu pia wa kupima na kuchunga yale tunayoyasema.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema nimekuwa waziri kwa miaka 12 ndani ya serikali hii, na nimewaona watendaji waliokuwa waadilifu, wachapakazi na wanaoipenda nchi yao. Sitaki kuwasemea, maana penye wengi pana mengi, sijasimama hapa kumtetea mtu yeyote yule. Lakini sikubaliani na mwelekeo huu wa Baraza hili tunapowazungumza watendaji wa serikali yetu, ikawa kila mmoja mbaya au wote hawana maana. Jamani nafikiri tunaipeleka nchi yetu siko, na tukiwa watu wazima wenye wajibu na dhima, naamini tunapaswa kuchunga na kupaswa kutizama tunachokisema. Tunawavunja moyo, ninawajua wengi ambao wamepewa pesa

nyingi ya kuihama hii nchi, lakini bado wapo wanaitumikia nchi hii kwa mazingira waliyokuwa nayo, na ni wazalendo wa kikweli kweli. Naamini tunapaswa kuwaunga mkono, kuwatia shime na kuwapa moyo. Mhe. Naibu Spika, bila shaka wale ambao watakiuka taratibu za sheria na kanuni za utendaji wa kazi zao, basi mkondo wa sheria utafanya kazi yake.

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo nataka nilizungumzie kwa ufupi sana ni hili la msamaha wa kodi. Suala hili mimi nahisi hatulitizami kwenye upeo wa kinchi. Rwanda *50% tax exemption*, ikiwa unawekeza katika maeneo ya Kigali na vitongoji vyake, na katika maeneo mengine maalum. Kwa sababu hawa wawekezaji ni wachache na kila nchi inawataka wawekezaji hao hao, na tumeamua kwa makusudi ili kuwakaribisha wawekezaji waje wawekeze basi tuwape fursa au unafuu maalum. Sasa tunapoanza kuzungumza kwamba hili hatulitaki tena, jamani hamuoni kwamba taathira kwa uchumi wetu na ukuaji wa uchumi wetu na wananchi wetu ni kubwa mno. Maana yake sasa tunaanza kuwafukuza wawekezaji, wakati tumekubaliana ndani ya Baraza hili hili na tukatunga sheria. Sasa kuna tofauti na ukiukwaji wa sheria na pengine utoaji wa misamaha isipo na lazima.

Lakini Mhe. Naibu Spika, naamini baada ya kusoma mtiririko wa mwaka 2008/2009, 2009/2010 nafikiri Mhe. Waziri amefanya jitihadi kubwa na tumeokoa zaidi ya bilioni 9, kama nitakosea atanisawazisha. Tumeokoa bilioni 9 alipopewa majukumu yeye ya kusimamia wizara hii. Baada ya wajumbe wa Baraza hili na serikali yenyewe kuelekeza kwamba hapana. Naamini kwa mazungumzo niliyoyasikia ndani ya serikali, bado kuna hatua nyengine mahususi zinachukuliwa, ili kuhakikisha kwamba watu wanalipa kodi na misamaha hii inakuwa maalum na inasimamiwa ipasavyo. Kwa hivyo, haya ni maeneo ambayo kuna mafanikio na wawakilishi wa wananchi nao tunapaswa kuyazingatia na kuyapima.

Mhe. Naibu Spika, kabla sijaingia katika *point* yangu ya mwisho, nataka nizungumzie hili ambalo lilizungumzwa na wengi la kamati teule. Mhe. Spika, nchi hii imekubali kuendesha shughuli zake kwa misingi ya katiba na sheria, *this is a democratic country*. Ni jambo la kushangaza na la kusikitisha wanaposimama watu wazima baada ya kuleta ripoti ya kamati teule, ikawa maoni ya kamati teule ile ndio hukumu na hakuna mwengine mwenye fursa wala haki ya kusema lolote lile, ndio mazingira yanaelekea kujengwa ndani ya Baraza lako tukufu, ambalo mimi nahisi sio jambo sahihi na tunaelekea pabaya, mlotugusa sote tupo hatujaondoka wala hatuondoki. Lakini sio vizuri wakati serikali imeshalithibitishia Baraza hili kwamba maelezo yaliyokamilika na ya kukidhi matumaini ya Baraza hili yataletwa.

Lakini kabla ya hapo Mhe. Naibu Spika, tumeshahukumiwa, hatuwezi kukubali, naamini ni lazima tufike pahali tustahiane, kwa sababu na sisi ni viongozi wa watu, tunapoendelea hivi bila ya kusema kuna taathira kubwa. Sio nafasi yangu wala si pahala pangu pa kulisema hili, lakini naona linaanza kuelekea pabaya. Kwa mana serikali yangu ilikuwa imeshasema italeta na sote tumeshatakiwa kutoa maelezo kwa kadiri ya upeo wetu na tunavyofahamu na tumeshafanya hivyo. Pale ambapo Baraza hili litataka tuwajibike tutawajibika. Lakini pale panapostahili, si hivi tunavyopelekwa.

Mhe. Spika, nikimalizia hapo nataka nizungumze suala la Muungano ambalo limezungumzwa na takriban wajumbe wako wote. Lakini awali, pia nataka niungane na kila mjumbe wa Baraza lako tukufu aliyelizungumzia amani na utulivu. Hakuna mbadala wake Mhe. Naibu Spika, hili limezungumzwa kwa vizuri sana na Mhe. Asha Bakar Makame, kwa kweli ametukonga moyo asubuhi. Amani na utulivu wetu tumeupata baada ya shida na madharuba ya miongo mingi sana na Wazanzibari wamekataa fujo, Wazanzibari wamekataa zahma na wamekubali kuunda utaratibu mpya wa utawala ndani ya nchi yetu, ili tuondokane na siasa hizi za vurugu, mivutano na kupelekeana kwenye kuumizana.

Kwa hivyo, ninawaomba Wazanzibari wenzangu tusikubali kikundi chochote kile, watu wowote wale ambao wanataka kutupeleka kwenye hoja hizi za Muungano na kuzilazimisha na kutuelekeza kwenye vurugu. Hazina tija kwetu, kwa maana tumeshaanza kushtumiana, tumeshaanza kutizamana kwa macho ya kengeza. Hao watu fulani, wamo ndani ya serikali, ndio hao. Tunaanza kidogo kidogo kurudi kule ambako tumetoka ambako sisi wenyewe tulikataa hatukutaki. Kwa sababu tu kuna kikundi cha watu wachache ambao wanahisi kuwa wao sheria za nchi hii haziwahusu.

Mhe. Naibu Spika, na Waheshimiwa Wajumbe, sote tunakubali kwamba tuna Rais muungwana, Rais binadamu anayeheshimu wenziwe na anayeheshimu misingi ya haki za binadamu, na anayeheshimu katiba ya nchi hii. Lakini ni lazima tuelewe kuwa pia ana wajibu na haki ya kuwalinda wale wasiokubaliana na vurugu hili. Hata wakiwa wawili na mimi nikawa wa tatu, kwa sababu ni haki yetu.

Kwa hivyo, ninawaomba sana Wazanzibari wenzangu, na ninaungana na wajumbe wote wa Baraza hili la Wawakilishi waliosimama na kuwaelekeza Wazanzibari kutulia, kutii sheria za nchi yetu na kuachana na vikundi hivi vya uhasama, na kuelekeza hoja zetu, maoni yetu, na nguvu zetu kwenye utaratibu wa sheria.

Mhe. Naibu Spika, ndani ya Muungano huu Zanzibar imehusika na Muungano wenyewe, kwa maana Muungano wa Jamhuri ya Tanganyika na Muungano wa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar. Ni haki ya kila Mzanzibari kuuzungumza Muungano huu, na ni dhambi kwa mtu yeyote yule hata kuashiria kumkataza Mzanzibari au Mtanganyika kuzungumza Muungano huu. Tena ana haki ya kuzungumza anavyoona yeye unafaa.

Mhe. Naibu Spika, hapa naomba nikusihini sana viongozi wenzangu wa kisiasa, ni lazima tuwe wa mwanzo katika kuhubiri kuvumiliana na kuheshimiana. Kwa maana sote hatuwezi kukubaliana mawazo yetu yakawa yanafanana.

Kwa mfano, wako wananchi wengi hivi sasa hawautaki Muungano, lakini unapoanza kuwachukia na kutaka kupambana nao hatima yake sio njema. Ukihisi kutokutaka kwao Muungano kuna taathira kwetu, basi tuna wajibu wa kuwasihi na kuwaelekeza kwenye njia sahihi. Mimi ninafanya hivyo, wanaonikabili kuniuliza ninawaambia, kwamba hapana Muungano tusiuvunje kwani Muungano sio tatizo, mfumo ndio tatizo. Kwa maoni yangu mimi. Hili nalo Mhe. Mohammedraza alilizungumza vizuri sana na sote tukakubaliana naye humu ndani.

Kwa hivyo wale ambao tunahisi mawazo yao tofauti na sisi, tuna wajibu kuwashawishi, kuwasihi na kuwavuta sio kupambana nao na kuwachukia, hivyo sivyo. Wale wanaotaka serikali mbili, pia tuna haki ya kuwasikiliza na kuheshimu mawazo yao. Wako wengine wanataka serikali tatu humu na wako wengine hawajali kabisa, unapozungumza nao wanakuambia kwamba aah; mambo hayo bwana nyinyi wanasiasa ndio mnajenga maslahi yenu huko, sisi tunapata nini. Kukiwa na serikali mbili, moja au tatu sisi tunapata nini au maslahi yetu yako wapi. Kwa hivyo, ni lazima tujenge utamaduni wa kuheshimiana, kustahamiliana na kuvutana kwa hoja.

Mhe. Spika, mimi msimamo wangu sijapata kuuficha, tangu mwaka 2009 tunayazungumza pale ambapo yalikuwa hayazungumziki tumeyazungumza. Lakini wala tusipate tabu, kwa sababu tutasema wee hatimaye kila mtu ana kura yake. Sasa na wale pia wanaopita wakisema humu kwamba wawakilishi tusiwasemee wananchi wetu. Haya mambo ya ajabu yametoka wapi. Sisi tumechaguliwa na wananchi kuja kuwasemea hapa, haiyumkiniki kwamba kila aliyekuwemo ndani ya jimbo lako atakubaliana na msimamo wako wewe kama mwakilishi. Lakini mimi Mhe. Naibu Spika, ninaweza nikakukusanyia hapo nje zaidi ya asilimia 60 ya wapiga kura wa Jimbo la Kiembesamaki wanaosema kwamba huu mfumo sio.*(Makofi)*

Kwa kweli wakati wa mageuzi ya msingi, ya maana tena ni makubwa umefika. Mhe. Naibu Spika, wapo wengine wanaosema kwamba hawaitaki kabisa, lakini hao tunaendelea kuwasihi na wala hatuwaogopi, isipokuwa tunawaambia bwana ee unapozungumza kuuvunja wakati dunia yote hivi sasa inakimbilia katika kuungana na kujenga himaya na hifadhi ya pamoja, kwa nini tukitupe hiki kitu ambacho sisi tunacho kwa miaka 48 sasa? Hilo ni jambo la msingi; kwa nini utupe kitu ambacho unacho mkononi, lakini tuna kila haki ya kusema mmm! Mfumo huu wa serikali mbili haukuwa na tija kwetu. Kwa hivyo, sasa tunataka muungano na wazungu wanasema *fair and equitable*, yaani muungano wa haki na sawa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, na wala tusiyachanganye haya mambo, kwa sababu Zanzibar ilipoungana na Jamhuri ya Tanganyika ilikuwa ni nchi yenye utaifa wake kamili, yaani *sovereign state*. Kwa hivyo, ni dhahiri kwamba Zanzibar ni yenye utaifa wake kamili inaweza kuwa ndani ya muungano. *(Makofi)*

Sasa kuna tatizo gani tukawa na utaifa wetu kamili na kuweza kujiunga na *OIC* kama alivyosema Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali, tukawa na Kiti chetu cha Umoja wa Mataifa, pia tukajiunga na *FIFA, UNDP, UNPA, IFM, World Bank* na tukawa na uwezo wa maamuzi yetu pamoja na hatima yetu ikawa mikononi mwetu. Kwa kweli hayo yote yanawezekana kwa sababu ndivyo yalivyokuwa. *(Kicheko/Makofi)*
Msingi wetu wa Muungano hasa sio Katiba ni Mkataba (*Articles of Union)*. Kwa hivyo, jambo la msingi ni amani na utulivu lazima sheria tuitii, na wala tusiwakubali watu ambao wanaotaka kutuondosha kwenye misingi yetu wakatupeleka kwenye vurugu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, bado dakika tano.

Mhe. Mansour Yussuf Himid (Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana zinanitosha sana hizo.

Kwa hivyo, tusikubali watu kutuondosha kwenye malengo yetu na wala tusiwakubali watu wanaotaka lazima wakhalifu sheria na kulazimisha sheria. Mhe. Naibu Spika, nakubaliana na Waheshimiwa Wajumbe wenzangu waliosema kwamba twende kwenye Tume ya Mhe. Jaji Warioba. Wazanzibari tukajenge hoja mwanana tena za msingi kabisa. *(Makofi)*

Vile vile nakubaliana pia na Wajumbe wa Baraza hili tukufu la wananchi wa Zanzibar kama wao, mimi pamoja na sote kwamba tutahakikisha kwamba tunasimamia matakwa ya Wazanzibari, kwa maana ya tunawajibika kwani wametuchagua kwa ajili ya kusimamia maslahi yao, hivyo tunawahakikishia tutawafanyia. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, huko nje kuna msemo wanasema wanataka kuachiwa kupumua, lakini zaidi hili wanatumia wale Uamsho na mimi si Uamsho, kwa sababu tayari nimeshaambiwa kwamba ni Uamsho na wala si Uamsho, lakini kwa hili tuachiwe kupumua nakubaliana nao. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nasema vizuri, ili nifahamike mimi si Uamsho, lakini kwa kauli hii ya tuachiwe tupumue nakubaliana nao na wala sikubaliani na vurugu zao nawaambia wasikie hasa, kwamba mimi mmoja sikubaliani na vurugu zao, lakini kwa kauli mbiu hii tuachiwe tupumue tena nakubaliana na Wazanzibari. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja na ninawaomba na kuwasihi sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tuipime Bajeti ya Serikali kwa upeo wa kinchi kwa dhamana na majukumu tuliopewa na wananchi wetu, sio kwa jazba wala upeo finyu, na tumpe silaha Mhe. Waziri kwa kumpitishia kwa kauli moja bajeti yake, ili akasimamie Bajeti hii ya Serikali ili tupumue. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, ahsante naona ulikuwa unamalizia na kuendelea tena.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia bajeti hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo Koani. Kwanza sina budi nimshukuru Mhe. Waziri kwa kuleta bajeti nzuri yenye kufahamika ambayo ni ya maendeleo kwa kipindi hiki cha sasa.

Nikianza na mchango wangu moja kwa moja niende kwenye ukurasa wa 18 kuhusu masuala ya kilimo. Mhe. Naibu Spika, kilimo ndio uti wa mgongo wa nchi yetu, ambapo hivi sasa tunaendelea vizuri sana na maendeleo yake tumeyaona hasa katika upande mmoja wa zao la karafuu.

Kwa kweli zao la karafuu hivi sasa tunashukuru tumepata mafanikio makubwa sana ya nchi yetu, hasa kwa vile tumepandisha bei nzuri sana na kwamba wananchi wetu wengi wameweza kutajirika kwa kilimo hasa kwa zao la karafuu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ni wengi sana hivi sasa wanatajika kutokana na zao la karafuu. Kwa hivyo, ninamshukuru sana Mhe. Waziri kwa kuweza kutoa ujumbe au Tume Maalum kwenda nje kwa ajili ya kutafuta bei nzuri ya karafuu na hadi sasa mwananchi kuweza kuwa na uhakika, yaani akipata kilo moja tu ya karafuu kavu basi tayari ameshapata mlo wa siku mbili kwa hilo tunashukuru sana. *(Makofi)*

Vile vile katika zao la karafuu lisiwe peke yake kwenda tume nje kwa ajili ya kutafuta bei ya mazao. Kwa hivyo, aendelee Mhe. Waziri katika bajeti yake kupanga fedha kwa ajili ya kwenda kutafuta bei nyengine za mazao ya hapa nchini. Kwa kweli hivi sasa kuna mazao mengi ambayo yanahitaji kutafutiwa bei nzuri hasa huko nje ambayo yanatoka nchini kwetu, lakini naona Mhe. Waziri hakuyasimamia sawa sawa kuyataja hasa mazao ambayo yanaweza kupata bei nzuri na yapo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri apange bajeti rasmi ya kuweza kwenda nje kwa ajili ya kutafuta bei ya mazao kama vile pilipili hoho, ambacho ni kitu kizuri sana tena kinafafana na karafuu hasa kwenye *taste* yake, kwa sababu karafuu uzuri wake inakuwa inawasha na hizi pilipili hoho ni nzuri sana, kwa sababu zinawasha na zinaweza kupata bei sawa na karafuu au kuliko karafuu.

Sasa tunajua kwamba nchi zetu zote hizi zinaendelea kutokana na kilimo, ambacho kinatoa faida hata katika mambo ya kisasa ya sayansi na teknolojia kama vile vita vya kisasa, yaani muda mwingi watu wanaweza kupanga kuweza kupata pilipili hoho, na nchi peke yake inayoweza kutoa pilipili hoho duniani ni Zanzibar. *(Makofi)*

Kwa hivyo, kama Zanzibar tutakwenda kutafuta bei katika nchi za dunia hasa Marekani pamoja na nchi nyengine ambazo wanazitumia sana pilipili kwa shughuli zao kama vile China au Japan, basi tunaweza kuhakikisha bei yetu ikawa sawa na karafuu.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri ahakikishe katika kutafuta bei asiende peke yake au Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko peke yake, ni vyema kwamba waende watu ambao wenye utaalamu kwenye majimbo yao. Kwa mfano, sisi tunayo majimbo 50 hapa Zanzibar, ni vizuri kwa sababu majimbo hayo yanayo Waheshimiwa Wawakilishi, watoke wawakilishi wao pamoja na Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, ili kuhakikisha kwamba kila jimbo linatafuta biashara nzuri kwa ajili ya wananchi wao.

Kwa kweli mimi kama nitakwenda Marekani au Japani ama China, basi nitalitetea sana Jimbo langu la Koani, kwa sababu lina hakika ya kuzalisha pilipili nyingi sana. Vile vile kama nitakwenda China nina hakika nitalitetea Jimbo langu la Koani kwa sababu lina mwani mwingi sana. Mhe. Naibu Spika, naelewa kwamba mwani ni biashara nzuri, ambayo hivi sasa inatajika sana ambapo Wachina wanakula au kufanyia dawa. *(Makofi)*

Sasa iweje mimi Mwakilishi wa Jimbo ambapo siwezi kwenda kuhakikisha kwamba jimbo langu linaweza kutoa biashara gani kwa ajili ya kupata fedha nyingi. Mhe. Naibu Spika, kumtoa Mhe. Waziri peke yake ni kuhatarisha wananchi wasipate haki zao za kupata fedha za kigeni na kuhakikisha bei nzuri katika mazao yao.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa mwani uko chini sana kwa sababu wananunua wazalendo hapa na wala hawana bei nzuri, ni kama vile zamani ilivyokuwa karafuu, yaani ilikuwa hatujui chochote kwamba karafuu ina bei. Baada ya kuondoka kwenye meza zetu maofisini wakati alipotoa nafasi Mhe. Rais kwa lengo la kutafuta bei ya karafuu, basi hapo ndio Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko alileta bei nzuri ya karafuu mpaka kufikia kilo moja ya karafuu shilingi 15,000/=. *(Makofi)*

Sasa nahakikisha kwamba kama na sisi Waheshimiwa Wawakilishi wa majimbo tutakwenda nje, basi nahakikisha kwamba mwani utakuwa bei ya shilingi 10,000/= kwa kilo badala ya shilingi 1,000/=. *(Makofi)*
Katika kilimo tunahitaji tuwe na zana za kilimo zikiwemo pembejeo kama vile mbolea. Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri katika bajeti yake ahakikishe kwamba mbolea inaletwa kwa wingi sana hapa nchini, ili wananchi wetu waweze kulima mazao yenye kutoa faida nyingi, pamoja na kupata maendeleo kwa maana ya kuwa mengi. Kwa mfano, hivi sasa kuna zao moja ambalo ni muhimu sana duniani na wala halipatikani popote katika dunia hii, ambapo ni zao la tangawizi. *(Makofi)*

Kwa kweli tangawizi za Zanzibar zinasifika dunia nzima, kwa sababu ni kama vile nilivyosema kwamba ni kali sana tena zinawasha sana na zina bei nzuri sana. Kwa hivyo, tunaomba kwamba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, atoe nafasi kwa majimbo hasa ndugu zetu wa Mkwajuni ambao wanalima tangawizi sana, pia kutoa nafasi kwa ndugu zetu wa Mkwajuni huko kuweza kulima manjano, ambapo manjano ya Zanzibar inatakiwa katika ulimwengu mzima na wala haipatikani. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, hii ni nafasi nzuri ya kuweza kuhakikisha kwamba hivi sasa nafasi inatoka majimboni na Waheshimiwa Wawakilishi wanakwenda kutafuta wenyewe bei nzuri ya bidhaa hizo, kwa ajili ya kuwasaidia wananchi wao katika majimbo. (*Makofi*)

Nikiendelea na mchango wangu sasa nizungumzie kuhusu suala la kukusanya pato la taifa, ili tuweze kuwa na fedha za kutoa ada za kulipia na tuweze kujenga skuli, hospitali zetu. Kwa hivyo, ni vizuri kuhakikisha kwamba ada za bandari zinalipwa vizuri kwa usafiri wa kwenda Dar-es-Salaam na hata Pemba, yaani lazima tuchangie ada kama ilivyo kawaida na wala isiwe tunachangia kwa Dar-es-Salaam na tukaacha Pemba tusichangie, kwa sababu msafiri yeyote ni msafiri na anaweza kuchangia pato hili na hatimaye kuweza kujenga skuli pamoja na hospitali zetu.

Kwa kweli kusema kwamba nafasi hii tuiachie kwa Mhe. Mbunge au Mwakilishi peke yake ndio achangie kwa ajili ya kujenga hospitali au skuli. Hali hiyo inaweza kuchukua muda mrefu, kwa sababu kipato chetu ni chini na fedha ambazo zinazotoka ni fedha kidogo sana na wala hazitoweza kutosha kujenga hospitali au skuli, kutia meza pamoja na viti vikawa vizuri katika skuli zetu.

Mhe. Naibu Spika, ni wazi kwamba kuchangia katika sehemu zote zinazotakiwa kulipwa ushuru hasa bandari. Kwa upande wa bandari wakati wasafiri wanaposafiri ni wasafiri tu na wala isichague anakwenda wapi, kwa mfano akiwa anakwenda Ulaya basi atatoa ada pale uwanja wa ndege, akiwa anakwenda Pemba na Dar-es-Salaam atatoa bandarini. Kwa hivyo, kuna haja ya kuchangia ada kwa sehemu zote za mapato na risiti zitoke kama kawaida, ili wananchi wachangie vizuri. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, sasa nizungumzie kuhusu amani na utulivu. Kwa kweli amani na utulivu kwa nchi yetu ni jambo muhimu sana linalotaka kutunzwa kama tulivyolikuta hapo nyuma kwa wazee waliotukabidhi madaraka

mpaka leo tukafika sehemu hii tuliopo hivi sasa katika Baraza la Wawakilishi. Kwa hivyo, tumetumwa katika Baraza hili la Wawakilishi na wananchi wetu huko majimboni kwamba tuje tuwawakilishe vizuri hasa kuhakikisha kudumisha amani na utulivu. *(Makofi)*

Sisi wawakilishi ndio wakubwa ambao wenye hatamu ya amani na utulivu, kwa sababu ndio tunaotumwa na wananchi kutoka majimboni mwetu, kwamba hapa tuje tuwasemee wao na wala sio kama itoke nafasi ya kuwasemea wananchi wetu kama vile wanavyofanya ndugu zetu wa Uamsho. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli wao hawatumwi na wananchi kutoka majimboni, isipokuwa wamejitokeza peke yao tu na kuweza kusema kuwa wao ndio wanajua kusema au kufanya. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, sisi wananchi wametutuma, ili tuje hapa katika Baraza kwa ajili ya kuja kuwasemea, sasa iweje leo yanatoka magari 50 mpaka 100 yanaingia jimboni kwenda kuwauliza wananchi wangu kwamba muungano mnautaka au hamuutaki, wakati wao wamenileta hapa Barazani kwa ajili ya kuwasemea, sasa iweje watoke watu wengine kwenda kuwasemea wananchi wangu wa Jimbo la Koani. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, sijawahi kusikia hata mara moja wananchi wa Jimbo la Koani wametoka na magari kwenda katika Jimbo la Mji Mkongwe au kwenda mjini na kuwaambia watu waseme hivi au vile. Sasa leo iweje watoke watu mjini kwenda katika majimbo yetu ya mashamba kwa sababu gani? Kwa kweli hali hii haipendezi Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*
Kwa hivyo, nadhani watu wa mjini wakae mjini na wazungumzie kuhusu Uamsho na wala wasiende mashamba, kwa ajili ya kutusemea wenyewe tupo ambao wananchi wametuchagua kwa lengo la kuja kuwasemea hapa katika Baraza. *(Makofi)*

Kwa kweli inasikitisha sana kwamba watu wanatoka na jazba, wanawapiga watu njiani, wanaponda wanyama wa watu, wanapita na vimurimuri kama Rais na hapo wewe usishtuke na kusema lolote, yaani ukisema tu unapigwa kibao au rungu kwamba umekashfu msafara wa Uamsho. Mhe. Naibu Spika, Uamsho unatupeleka pabaya. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba kuzungumzia kuhusu Viongozi wa Uamsho. Kwa mfano, mimi mwenyewe tayari nimeshakutana na Viongozi wa Uamsho pamoja na Kiongozi Farid, kwenye kamati yangu ameshakuja mara mbili kuzungumza, na mimi na nilimfahamisha vipi nchi yetu inataka na sivyo vile unavyotaka wewe. Hivyo ni vyema fanya jinsi inavyotaka nchi yetu na sio uamue wewe kama wewe, kwa sababu sisi tunaozungumza hapa ndio tuliowekwa na wananchi kwa ajili ya kuzungumza mambo ya majimbo yetu, na wala sio wewe uzungumze yale unayotaka wewe.

Vile vile nilimuuliza Sheikh Farid wewe unazungumza katika majimbo ya wenzako hivi wewe ni nani? Mhe. Naibu Spika, tunasikia kwamba ndugu yetu huyu ambaye ndiye Mkuu wa Uamsho anachojivunia sana inasemekana yeye ni askari mstaafu, kama ni askari mstaafu basi tunamhakikishia kwamba hapa Zanzibar askari wastaafu ni wengi tena wanaumwa na nchi hii kuliko yeye. *(Makofi)*

Kwa hivyo, asilete matatizo ya kugombanisha nchi au ya kusababisha ugomvi wa nchi hii, kwa sababu nchi hii inazungumza kwa amani na mkataba, na wala sio kwa jazba, yaani yale yanayozungumzwa kama yanavyopangwa katika hili Baraza. Sasa yeye anaposababisha watu kwenda kufanya fujo katika majimbo, basi ajue kwamba anahatarisha amani ya majimbo. *(Makofi)*

Kwa mfano, juzi tu katika Jimbo la Donge na hapa walikuja kunisikitikia mwenzao katika jimbo langu, juzi imesababishwa ajali watu si chini ya watu kwa sababu ya *Blood Pressure* na wengine hivi sasa ni mahututi na sijui kama watapona kutokana na hali ya mabomu, na yamesababishwa na watu kutoka katika majimbo ya mjini kwenda kwenye majimbo yetu ya mashamba na kusababisha fujo. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, tunatoa ilani kwamba hatutaki katika majimbo yetu ya mashamba kuingiliwa na majimbo kutoka mjini. Mhe. Naibu Spika, kama si hivyo basi tutatoa amri katika majimbo yetu vijana wetu ambao ni wastaafu wamdhibiti Sheikh Farid kama anavyolihangaisha taifa hili. *(Kicheko/Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba nizungumzie kuhusu muungano. Mhe. Naibu Spika, suala la muungano ni sahihi sana kulizungumzia. Lakini tunaomba kwamba wananchi wasubiri siku ambayo tumepangiwa kwa ajili ya kulizungumzia suala la muungano likoje na tulitolee uamuzi kama tulivyoambiwa na marais wetu, kwamba iko siku na saa tume itapita kila jimbo kwa ajili ya kulizungumzia suala hili la muungano na utatoa ushauri wako na utasikilizwa.

Mhe. Naibu Spika, tukikumbuka kwamba Mwenyezi Mungu ameumba watu na kuwajaalia miongoni mwao kuwa viongozi, yaani Mitume kwa ajili ya kuwafahamisha wenzao kipi kifuatwe, na sawa kwamba kila nchi ina rais na rais katika dunia ni kama Mungu wa dunia, kwa sababu yeye ndiye aliyepewa uwezo wa kutusemea sisi katika nchi yetu au binadamu yeyote anapozaliwa anaambiwa Mungu wako wa duniani ni baba yako na mama yako.

Sasa leo iweje kwamba sisi tusisikilize maagizo ya Mhe. Rais ambayo ametupangia wananchi wake, kwamba tutulie na tusubiri siku ambayo itafika, kwa ajili ya kuja kutoa maoni yake kuhusu muungano huu. Mhe. Naibu Spika, sasa leo iweje kwamba watokee watu na kusema iwe kwa nguvu na lazima tuseme muungano hivi na vile.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika sisi katika jimbo letu tunafuata ile amri ya Mhe. Rais na tunasubiri siku ambayo tumepangiwa kwa ajili ya kuzungumzia suala la muungano, na sio wakati wote kulizungumza suala la muungano na kuacha masuala ya maendeleo ya vijiji vyetu.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la kumtaja Mhe. Rais kwamba Mhe. Rais wetu hana dhamana kubwa katika nchi za nje. Kwa mfano, mimi mwenyewe pamoja na wananchi wa jimbo langu, tunaelewa nguvu za rais wetu ni kama nguvu za rais mwengine wa nchi yoyote ile, kwa sababu mara nyingi namsikia rais wangu huyo Marekani au China ama Hongkong na huko kote anaitetea Zanzibar. *(Makofi)*

Sasa iweje mtu aseme kwamba rais wangu anapofika Dar-es-Salaam hatambukili kama rais, hivi yeye rais anaogopa kutuambia sisi kwamba mimi nikifika Dar-es-Salaam si rais au yeye anapotusemea sisi kweli atashindwa kujisemea mwenyewe kuwaambia wananchi wake.
Kwa hivyo, suala hilo sio kweli kwamba rais wetu hana madaraka anapofika Dar-es-Salaam na rais ni rais tu, yaani anapokuwa Dar-es-Salaam ni Mhe. Rais wa Zanzibar kama tulivyopanga.

Vile vile anapotoka kwenda nje ni Mhe. Rais wa Zanzibar anaeleweka na tunamsikia kwenye hotuba zake kwamba yeye ni Rais kutoka Zanzibar, au amekwenda kwa ajili ya kumuwakilisha Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wala sio kama akifika nje anapunguzwa madaraka yake, isipokuwa yapo. *(Makofi)*

Sasa kama yangekuwa hayapo basi ni kweli kwamba Mhe. Rais hatuopogi kutuambia wananchi wake tumuombee. Kwa hivyo, iweje leo aje mtu aseme kwamba tumuombee rais kwamba madaraka aliyopewa sio yake na wala hayataki. Mhe. Naibu Spika, naamini kwamba madaraka aliyopewa rais wetu anayataka, anayapenda tena anayafanyia kazi. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa hayo yote niliyochangia namuomba Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwamba bajeti yake iweke kipaumbele zaidi kwenye masuala ya kutoa wawakilishi wetu kwenda nje kwa ajili ya kutafuta biashara za kilimo na wala sio kuishia hapa tu. Kwa mfano, mimi nakumbuka nimeishia Pemba na wala sijasafiri vizuri kwa hivyo huu ni wakati wangu sasa wa kwenda kutafuta soko na kuhakikisha Jimbo la Koani linaondokana kabisa na ufukara, kwamba halina fedha au wananchi wangu wanashinda kupata ajira.
Kwa kweli sisi katika jimbo letu tunashughulikia sana masuala ya kilimo pamoja na uvuvi. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwamba kwenye bajeti yake apange vizuri, kwa ajili kutoa viongozi kwenda kutafuta masoko au fedha nje. Ahsante sana naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, ahsante. Waheshimiwa Wajumbe tumebakiwa na muda mfupi kwa hivyo naomba utulivu.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi nashukuru kunipatia nafasi hii kuweza kusema machache juu ya hotuba hii ya bajeti.

Vile vile nichukue fursa hii kumshukuru Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kutuletea hotuba hii ya bajeti ambayo ina mwelekeo mzuri.

Kwanza kabisa nataka niungane na wenzangu kwa ajili ya kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein katika kutupatia msamaha akina mama katika huduma ya uzazi, yaani ametambua hali zetu na kujua jambo linalotukwaza sana akina mama. Kwa kweli tumefurahi na tunamtakia kila la heri na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atamuepushia kila la shari, na kumjaalia kuweza kutufikiria mema zaidi akina mama. *(Makofi)*

Katika huduma hii namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Mhe. Rais ametujali sana akina mama na kuona tunataka tupatiwe huduma hii katika hali nzuri kabisa.

Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, kuhakikisha huduma za akina mama wajawazito, ili ziwe zinatekelezwa ipasavyo basi ni vyema kuwe na utaratibu wa kutoa taarifa kwa atakayenyanyaswa, yaani iwepo *hot line* ambayo itakayokuwa wazi, ili akina mama waweze kutoa ripoti mara moja pale watakapopata usumbufu wowote.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu katika hotuba hii ya bajeti kwa kueleza yale ambayo Mhe. Waziri ameyapa kipaumbele. Mhe. Waziri amekizungumza, nami niungane nae kwa kweli kilimo kama tutakipa kipaumbele tutafanikiwa. Kwa sababu tunajua kilimo ndio uti wa mgongo wetu. Mara ile iliyopita Mhe. Waziri alituletea Mswada ambao ulitupa matumaini sana, wakulima vijijini tukapewa yale ambayo tuliyoahidiwa kwa kipindi kilichofuata cha ulimaji. Lakini katika kupata huduma hizi kulijitokeza matatizo mbali mbali ambayo hayo ningeomba Mhe. Waziri waweze kujipanga vizuri ili kuona vifaa vyote vinavyopatikana katika kilimo basi vinaweza kugawiwa katika utaratibu mzuri ili wakulima waweze kufaidika na kilimo.

Mhe. Waziri pia umezungumzia habari ya uvuvi. Hili nalo tunasema ndio zao letu kuu linaloweza kutuvusha kama ilivyo karafuu. Iwapo tutajipanga vizuri hasa katika uvuvi basi tunaweza tukafikia hatua nzuri kabisa. Kwanza kupatiwa wavuvi zile zana ambazo za uvuvi zinazohitajika za kisasa na kupatiwa maboti ambayo yataweza kuwafikisha katika bahari kuu.

Mhe. Waziri hivi sasa kwenye uvuvi tuna tatizo, wavuvi wetu wanatumia nyavu ambazo zimechomwa kwa sababu zinaharibu mazingira ya bahari, lakini bado kuna usumbufu wa kuwapatia zile ambazo zinahitajika kwa sasa.

Mhe. Waziri niende katika suala zima la ufugaji. Suala la ufugaji kama nalo tutalishughulikia vizuri na tutajipanga vizuri katika uwekezaji basi pia napo tunaweza tukapata faida kubwa. Lakini tukiacha tu wafugaji wetu wanafuga tu bila ya kupatiwa msaada wowote wa kitaalamu hivyo tunaona wafugaji wanakata tamaa, hata kupatiwa soko la uhakika Mhe. Waziri, hivi sasa tunaona wafugaji wa kuku soko lao linazidiwa sana na kuku wa Brazil. Kisiwa chetu kilivyo kidogo kama hatutakuwa na mipango madhubuti ya kuweza kuwapatia wafugaji wetu soko la uhakika wanaweza wakakata tamaa na hali ya umasikini ikaendelea kuwazonga.

Mhe. Waziri jengine pia nilisisitize ni suala zima la viwanda ambalo ulilizungumza. Pia viwanda ipo haja ya kurejesha uwakezaji wa viwanda vyetu ili hili tunalielewa kama litatupunguzia mzigo mkubwa wa vijana wetu katika kupata ajira. Viwanda ni muhimu vitatusaidia hata katika ukuwaji wa pato la nchi yetu.

Mhe. Waziri bajeti yako imezungumza mambo mazuri ina muelekeo mzuri lakini mimi nikuombe sana katika utekelezaji ndipo ambapo tunakwama sana. Tuombe kila yale ambayo tumejipangia basi tuyasimamie katika utekelezaji mzuri ili tuweze kupata mafaniko yale ambayo tunayatarajia. Saa nyengine tunapanga miradi mingi lakini pengine uwezo unakua ni mdogo. Lakini ni vyema tupange miradi ambayo inatekelezeka ili tuweze kuona katika hatua hiyo tumekwamuka na baadae tunakwenda hatua nyengine. Kuliko kupanga miradi mingi na hatimaye ikabaki katika makaratasi kwa kukosa utekelezaji.

Mhe. Naibu Spika, uchumi wetu unaweza ukakua vizuri iwapo tutajipanga vizuri. Kwanza kabisa tuwe waaminifu katika utendaji wetu, tuache uzembe ambao unaweza kusababisha upotevu wa fedha za serikali, tuache tamaa ya kujilimbikizia mali ambayo itawafanya wananchi wetu wabaki hohe hahe, tuchape kazi kisawa sawa na hatimaye kufikia malengo mazuri tuliyojipangia.

Mhe. Naibu Spika, niende katika kodi ambazo Mhe. Waziri ameziainisha. Kodi hizi mimi nisema zinaweza zikatuletea tija nzuri iwapo tutajipanga vizuri. Kama tutatekeleza kwa sababu tumechoka kuona bajeti hizi za utegemezi. Iwapo kodi hizi zitasimamiwa vizuri naamini tunaweza tukafanya bajeti zetu zikaondokana na hali ya utegemezi. Huu mwanzo utakuwa ni mgumu wa kuanzia suala hili kwa sababu linatubana. Lakini iwapo mtaweza kusimamia vizuri na kuona fedha hizi zinatumika kama vile ambavyo mmepanga katika bajeti hii, basi inaweza tukapata njia moja ya kutukomboa.

Mhe. Naibu Spika, sisi wenyewe tumekuwa mashahidi wa kuona miradi ya maendeleo ambayo inakwama kwa kusubiri fedha zile za wahisani. Leo tutakapokuwa wenyewe tumeweza kukusanya, tunaamini mambo mengi yanaweza yakakwamuka.

Mimi nilitaka nisende mbele sana lakini kwa kuwa wenzangu waligusia suala zima la Muungano basi na mimi sina budi kuchukua fursa hii kuzungumzia suala la Muungano. Muungano niseme kweli sisi bado tunaupenda na tuna uhitaji sana na Muungano tunaouhitaji ni ule ule wa serikali mbili.

Mhe. Naibu Spika, ndani ya suala hili la Muungano kunajitokeza kero nyingi za Muungano. Bila kutibu tatizo la kero ambazo zinajitokeza zinaweza zikazaa kero nyengine. Ni vizuri Serikali ya Muungano ikajipanga katika kutatua matatizo ili tukaweza kubaki na muungano ambao wananchi wote wataendelea kuupenda.

Mhe. Naibu Spika, maendeleo ya nchi hii hayatokuja kwa fujo au kwa jazba. Ni vizuri tukasimamia yale yote ambayo tunayahitaji katika Katiba mpya tusubiri wakati muafaka ukifika ili tukaweza kutoa maoni yote katika tume ya kuratibu maoni. Hivyo tunaweza tukafikia muafaka wa kupata lile jambo ambalo tunalikusudia.

Mhe. Naibu Spika, juu ya hili kumejitokeza wimbi la vijana ambao wanatumiliwa na hatimaye vijana hawa sisi ndio tunaowategemea kuwa watakuwa warithi wa taifa hili. Wanaposhiriki katika vitendo viovu wanajiharibia, kwa sababu wengine bado ni wanafunzi wanasoma wanashiriki katika mambo haya na baadaye wanapata hatia wanakamatwa kwa hivyo wanakosa kupata malengo waliyoyakusudia na hatimaye wanajikuta wapo mahala pabaya.

Mhe. Naibu Spika, mimi niwaombe vijana wetu watulie na wazee wetu watulie, tume ya kuratibu maoni itafika na kila mwananchi ataruhusiwa kwenda kutoa maoni yake ili kuweza kupata kitu ambacho ni kizuri tunachokikusudia. Mhe. Naibu Spika, mimi nilitaka kusema hayo machache. Baada ya kusema hayo naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia 100.

Mhe. Abdalla Moh'd Ali: Ahsante Mhe. Naibu Spika, naamini natarajia leo niwe mzungumzaji wa mwisho katika mkutano wetu huu.

Mhe. Naibu Spika, wengi wamezungumza na kwa ukweli kila aliyezungumza ana uweledi wake. Sisi tuliobakia tutayapitia yale yale ili kusisitiza kwa sababu umoja ni nguvu.

Mhe. Naibu Spika, wengi hapa wameuzungumza Muungano na kila mmoja ameuzungumza na lugha yake. Hivi sasa imekuwa ni lugha iliyokuwepo masokoni na sisi tunapokwenda hata Msikitini kusali basi anayetoa salamu akimaliza bega la kushoto anakuliza "Mheshimiwa unautaka" kwa hiyo na mimi japo kidogo nigusie suala hili.

Mhe. Naibu Spika, wengi wameona suala hilo ndilo lililosababisha kudumaa kwa uchumi wetu. Wakati huo huo ndilo lililosababisha kupotea kwa jina letu la Zanzibar. Sasa kwa hayo ndio ukawaona wananung'unika na wanasema mengi, haya hayakutokea leo. Nataka nikujulishe kwamba katika karne hizo za nyuma za Mitume basi masuala haya yalitokea. Watu walithubutu kutia uongo katika hizi hadithi ambazo tunazitumia leo kwa sababu ya kutafuta *laqab*, *kunia* na mengineyo. Hayo kwa lugha yetu ya kileo tunayaita *sovereign* kwa maana ya kuwa mamlaka.

Sisi hayo ndiyo tuliyoyakosa, hao mnaowasikia wanapiga kelele huko, wanayatafuta hayo na hayakuanza leo. Naamini kwamba wamepitia vitabu vyote ndio wakaona kwamba sasa ipo haja sisi ya kutambulikana huko ulimwenguni. Ndio ukaona wakaja wakaamsha na wakapewa jina wakaambiwa wao ni UAMSHO kwa sababu wamekuja kuamsha watu kutetea haki yao hii ambayo wameipoteza. Tunatafuta *sovereign*, njia ya kuipata tutaijua, tutaipanga na nina imani kwamba tutafikia hatua tunayoitaka.

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi kama hichi Wawakilishi wa wananchi huwa mara nyingi wanakutana kupanga namna ya kutafuta pato au namna ya kutayarisha keki na badala yake keki ile kuigawa kwa wananchi. Watafiti wa uchumi wanatueleza kwamba mara nyingi wale ambao wanachangia kikubwa katika utayarishaji wa keki hii ndio wao wanaopata kidogo katika ugawaji wake. Na wale wanaochangia kidogo katika ugawaji wa keki basi ndio wanaopata kikubwa katika mgawanyo wa keki hii.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri kaja hapa kifua mbele amesema kwamba mwaka huu wananchi wa kisiwa cha Pemba wameokoa pakubwa sana katika zao la karafuu. Na waliacha yao mengi sana katika kuliokoa zao hili, matokeo yake uchumi wetu umeboreka. Katika kuboreka huku kwa uchumi tumepunguza urari wa bei umepungua kwa sababu tumeweza ku- *export* na tukapunguza *import*. Maana yake sasa ikawa urari wa bei ukapungua kwahiyo wananchi wakapata bei zikapungua katika masoko yao. Kwa hivyo kidogo unafuu ukapatikana wa bei. Lakini wananchi hawa nashangaa kwamba tume ya mipango haikuwaona. Tume hii ilipokaa katika kuweka vipaumbe imejisahau. Kwa nini imejisahau? Nilifikiria kwamba kilio chao kikubwa au kipaumbele chao kikubwa wakati huu ni usafiri.

Mwaka jana Waziri hapa alikuja akatoa tarumbeta kubwa kwamba tuna mpango na Shirika la Saudia, tuna mpango na Shirika la Sudani, tuna mpango na Shirila la Uturuki, lakini mwaka huu hakuna neno lolote lililosemwa katika mpangilio huu. Je, hivi hawa wananchi wao hawakuonekana kwamba wana haja ya kuwa na wao wapewe kipaumbele na kipaumbele chao ni usafiri. Sijui Mhe. Waziri atakuja kutwambia nini wakati hichi ndio kilio chetu. Tumechangia pakubwa katika pato la taifa lakini hatukupewa kipaumbele ambacho sisi ndio tunakiona cha umuhimu zaidi. Labda vile ambavyo tungevipata kule kama kungelikuwa na usafiri wa uhakika basi tungezi *shift* huku na tungeona raha kuja hapa tukazitumia.

Mhe. Naibu Spika, kila mwananchi leo anajiuliza hivyo zile pesa walizopata bilioni 70 tunaona hazionekani zimekwenda wapi? Ningemuomba Waziri akaja akatupa maelezo, asije akatupa tarumbeta tupu kwamba kuna kampuni hii, kuna kampuni hii. Usafiri ni huduma, kwa vile ni huduma ni haki ya kikatiba ya raia huyu wa Zanzibar. Kwa nini hapatiwi mpaka leo, tunakuja hapa tunaambizana tu sijui itakuwa hivi, sijui tunakwenda vile, sijui kuna china, sijui kuna nani. Ni nani aliye na wajibu wa kutoa huduma ya usafiri kati ya Kisiwa cha Pemba na Unguja? Ni serikali, lakini leo haikujali chochote, imekuja hapa imetupangia sijui wazee 80 waliokuwepo pale ndio wanaotaka kulipwa. Sijui wameonekana vipi hata wapewe kipaumbele.

Mhe. Naibu Spika, mimi naendelea tena katika mchango wao kuangalia jinsi gani tunavyotoza kodi. Serikali imekuja na mpangilio mzuri sana nawashukuru kwamba wana nia lakini bado nia yao ni kumkamua yule yule mwananchi. Kwa nini nasema hivi Mhe. Spika? Hivi serikali imepanga inataka kuongeza ushuru katika mafuta asilimia 50. Ninachojua kwamba hivi sasa *item* hii ya mafuta tayari inatozwa 100 kwa ajili ya mchango wa kwenda katika barabara. Lakini asilimia nyengine inaongezwa katika hii hii ya mafuta. Hivyo hakuna kitu chengine chochote kinachoweza kuchangia huu mpango uliowekwa.

Mhe. Naibu Spika, tuna simu za mikononi ambazo kila raia wa nchi hii nina imani asilimia 80 tunazo, kwa nini angalau basi serikali isione kwamba hii asilimia 25 tuliyoipanga tuchukue katika simu, asilimia 25 twenda katika mafuta. Mafuta ndio propela ya kila kitu katika nchi hii, ikifanya kazi propela basi kila kitu kitakwenda mbele, kila kitu kitapanga, ukienda umeme, usafiri wa daladala, vyakula na bidhaa mbali mbali. Kwa nini tugande katika wazo hili la mafuta. Fikra yao sio mbaya lakini impunguzie mzigo ili mwananchi na yeye apate unafuu. Hatuna chanzo chengine isipokuwa ni mgongo wa mwananchi. Yeye ndiye kila kitu anakamuliwa kwa nini hatutafuti njia nyengine.

Mhe. Naibu Spika, hapa hapa serikali imesema imefuta kabisa njia ya STS hivyo kweli njia ya STS hakuona kwamba serikali ingeliweza kuondoa hii asilimia 50. Ni kweli vyombo vyote vya ulinzi na usalama tulivyonavyo katika nchi hii vinashindwa kuzuia magendo ya STS. Meli zinazoingia tunazijua, inakuja meli moja pale inakaa nje. Tuna KMKM waliyo na maboti, wamefanikiwa katika kusukuma meli, leo washindwe kweli STS. Ina maana kwamba mafuta tutakayoyanunua hivi sasa anaeleta ni nani? Ni Kampuni iliyoruhusiwa kutoka Bara, sio kampuni iliyoruhusika ya hapa. Kwa maana hiyo tutakwenda kununua Bara ambapo tutakutia foleni.

Kipindi kilichopita mafuta hapa yaliadimika. Ikabidi meli zetu ziingie katika Bandari ya Dar-es-Salaam. Zilipofika zikakwama kwa sababu zimekutia foleni, tukashindwa hapa kuzalisha sisi kwa sababu hatuna mafuta. Tukienda kule bei hii itaongezeka, anayefaidika ni nani? Kwa nini tushindwe ku-*maintain.* Tuna vyombo vya Dola vingi sana hapa KMKM wanalala hawana kazi, JKU wanalala hawana kazi, KVZ wanalala hawana kazi. Wanashindwa kwenda kuangalia meli pale ije hapa, ishushe pale halafu mwananchi yule yule anatakiwa atozwe tena kodi.

Mhe. Naibu Spika, hii si halali tuangalie nyenzo nyengine. Nina imani kwamba serikali inauwezo wa kuzuia magendo haya yakaondoka ili mwananchi akaondoka na kodi. Ukipandisha mafuta kila kitu kitakuja juu. Naomba serikali waliangalie na hii kodi ya 50 ya mafuta waiyondoshe, waweke hii njia ya STS iendelee kuwepo, *Ship to Ship* wanaweza wakailinda. KMKM hawana boti za kisasa, wanazo, watashindwa kwenda pale wakalinda meli inakuja pale inaonekana, kuna rada zinaona kwamba meli imeingia na ikija meli inasajili na inajulikana inakuja na tani ya kiasi gani. Tunashindwa kweli, lakini wameona aah wacha twende kwa mwananchi tukamtoa huyu huyu tena, shilingi mia inaingia, inaingia na tena. Maongezeko yote haya ya kodi yanayokuja mengine kuna mapendekezo ya kodi pia yanakuja katika mafuta, maana yake 50 linakuja na jengine 50, tutafika.

Mhe. Naibu Spika, naongezea kusema kwamba leo tumesema tena katika mapendekezo yetu haya tunakwenda kuboresha TRA. Hivi hii TRA ni chombo chetu, nilikuwa nauliza. Mhe. Naibu Spika, tunakwenda kuweka *database* tunakwenda kuweka mfumo mwengine wa kuweza *zone* kwani hili ndio tatizo? Kweli hili ndio tatizo kwamba tukiweza *zone* tutayapata mapato yetu kama kawaida. Hii *database* ninavyojua mimi ipo tayari,

ukienda Tanzania Bara wanakwambia sisi tuna *database*. Ndio mfumo huu sasa unaosababisha tukasema tunalipa kodi mara mbili. Ukitoa gari hapa tayari ipo *database* ya TRA na ukienda Bara wanakwambia *no* ulitakiwa wewe ulipe milioni 3 umelipa milioni 2.5 Zanzibar. Hatuitaki hii *database* iliyoanzishwa, hivyo viwango sisi hii si yetu pamoja. Tunauhakika kwamba tutakavyovipanga sisi hapa vitakubalika kule? Tutatumia pamoja? Leo *database* inayotumiwa ya hiyo ambayo imetungwa na TRA.

Mhe. Naibu Spika, ukija Zanzibar haikubaliki, leo wanasema sisi hatuitaki, kwa hiyo kuna mchafukoge. Kama Serikali ya Zanzibar hawaitaki wakati TRA ni ya pamoja, kuna haja gani sasa ya kusema TRA iwe na mfumo huu. Kwa nini tunaendelea kui-*maintain* kitu ambacho sisi hatuna faida nacho. Ondosha basi tunga yako ili upate kupanga unayoyataka. Uchumi wako haulingani na ule, kwa nini unaendelea kuna nayo Mhe. Naibu Spika. Nasema haya yaondoke mapema. Haya ndiyo unayoyakutia wananchi wanasema yote kwamba "hatuutaki, hatuutaki" kwa sababu hizi sio jengine.

Mhe. Naibu Spika, leo tunasema kwamba tunataka kuongeza mapato. Mapato haya yataongezeka katika mgongo wa mtu tu. Katika bajeti iliyopita tulikuja hapa tukasema tunataka kuanzisha Maeneo Huru haya yangetusaidia katika kukuza mapato. Lakini leo unakwenda maeneo huru unakutia kwamba ni Msitu wa Hifadhi ya Taifa. Sasa kweli huyo anayetoka China kuja kuwekeza hapa kweli atakuja Mhe. Naibu Spika. Tumekaa tumesema tunakwenda kwenye *basic budget* kwamba tunaandaa leo mpango tutakao uendeleza ndiyo *program*.

Mhe. Naibu spika, sasa kuna *program* gani ya kuendeleza haya maeneo ili kuvutia watega uchumi ili wakapungua wananchi wetu kulipa kodi, ipo wapi? Sasa leo tutaendelea kumtoza yule yule raia kwa sababu hatuna njia nyengine. Kiwanda kitajengwa wapi, wakati kule hujamuwekea, umeme, hujamuwekea maji, hakuna barabara, akija unakwenda kumuonesha pori. Atasema *Oh no, sorry my friend,* haji tena huyo. Kama kweli tunayo *program* basi ianze hapa, ili tutakapofika angalau miaka mitatu mwananchi apata unafuu sasa. Hayo ndiyo ya kufanya kodi, tuipeleke sehemu nyengine sio kila siku tunatoa kodi kwa raia tu.

Mhe. Naibu Spika, tuna mashirika haya tunavyoambiwa ya Serikali, tuna Shirila la Meli, Shirika la ZSTC, tuna Bima. Bima na ZSTC angalau yapo *live* unaweza ukayaona yanaendelea lakini kuna baadhi ya mashirika mfano kama Shirika la Magari tunambiwa likomahututi (ICU), halina faida yoyote. Lakini serikalini unaweza ukakutia linapewa ruzuku, lifanye nini? Tuna Shirika la Meli hivi linatoa mchango kiasi gani? Wao nilitarajia tokea walivyokabidhiwa Maendeleo na Mapinduzi 1972 au 75 lao wangelikuwa wao wakutwambia tuna mtaji kiasi hichi tunataka kuwekeza katika meli. Bado tunalo tu, hetu Mhe. Waziri mashirika haya yanafanya nini leo hapa. Twambie hao wafanyakazi wa Shirika la Meli wanafanya nini? Unaendelea kuwa *maintain* na unawapa ruzuku. Unatupandishia kodi sisi tuchangie madawati, mashirika hayo yanafanya nini na mchango wao kweli upo katika kiwango au unatuletea figa tu halafu unakuja kutwambia aah wamechangia 2.7, au wamechangia ngapi.

Mhe. Naibu Spika, hebu twambia hawa *Bank* watachangia ngapi, Shirika la Umeme watachangia ngapi. Leo Shirika la Umeme ukenda unaambiwa Shirika la Umeme linataka lisaidiwe nalo linangojea damu ya dharura, litiwe damu ili liwezesha kuja juu. Kwa maana hiyo sisi tunatakiwa hivi sasa umeme umeshapanda mara 2, 3, nani atalihami. Shirika hilo lilitarajiwa lizalishe kuingiza pesa au kuchangia katika pato la taifa, leo wao wana madeni.

Mhe. Naibu Spika, nende katika sekta inayosema kwamba sisi tunaelekea katika sense. Mpango huu unatwambia kwamba sisi tunaelekea katika sense. Sense hii anakuja kuhesabiwa nani? Wanaokuja kuhesabiwa ni wakaazi, lakini wakaazi hawa wote wamekataliwa na jamii yao. Kuna mtu anaitwa Sheha ukenda anakwambia mimi sikutambui. Hivyo leo kweli huyu raia atakuwa tayari afungue mlango ahesabiwe huyu. Mimi nitamwambia usiende kwa sababu wewe hutambuliki. Vyenginevyo basi mtambue mapema, tuna muda huo unakuja. Mheshimiwa nimekuja huyu mtu mbambue mapema. Kwa nini huyu usimpe haki yake. Siku ikifika mtu anaambiwa fungua mlango nimekuja kuhesabu sense. Atamuuliza umekuja kumuhesabu nani, mimi si mkaazi. Si unahesabu wakaazi wa Zanzibar. Atakuwa na haki kuja kukueleza kwamba mimi usinihesabu. Akija akiniuliza Mheshimiwa vipi nende, namwambia usende mpaka na wewe akupe ukaazi wako. Nitakuwa nipo sahihi.

Mjomba huu ni mchezo wa karata, mchazo wa karata mara nyengine huwa unatumia mapiku, lakini ukishindwa mapiku huwa unatumia turufu. Sasa sisi mara hii tunayo turufu. Itakapofika wakati madhali mapiku hayatumiki tena itabidi tutumie turufu.

Mhe. Naibu Spika, kwa hayo machache naomba nimalizie.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe nawashukuru kwa michango yenu mizuri naomba nitoe matangazo mawili kabla ya kuakhirisha kikao chetu.

Tangazo la kwanza Mnadhimu wa Chama cha Mapinduzi anawataka wajumbe wote wa Chama cha Mapinduzi tukiakhirisha kikao wabakie humu ndani kwa muda mfupi kuna masuala muhimu.
Tangazo la pili kesho tunategemea kumaliza michango yetu katika Bajeti hii kwa hivyo tunao *back bancher* wamebakia 9 na Mawaziri. Kwa hivyo naomba wale wote waliokuwa hawakujisikia waje mapema tutapunguza maswali ili watu wachangie wote na jioni tumwite Waziri amalize.

Baada ya matangazo hayo naakhirisha Kikao chetu hadi kesho siku ya Jumatano tarehe 20/6/2012 saa 3: 00 asubuhi.

(Saa1.45 usiku kikao kiliahirishwa hadi
tarehe 20/06/2012 saa 3.00 asubuhi)